# Nipashe

Jumatatu Januari 28, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579826

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US





UKURASA 13



## Wadau wafunguka pendekezo viongozi wa dini kuzuia kamari

UKURASA 2

# Kakobe acharuka

• **Awaonya** wanaowatukana viongozi wa dini, awataka watubu, vinginevyo... *Endelea ukurasa 2*



MKUU wa Kanisa la Full Gospel Bible Fellowship (FGBF), Askofu Zachary Kakobe.

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

### WAWEKEZAJI HIFADHI ZA BAHARI MATATANI

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, ametoa mwezi mmoja kwa wawekezaji walioingia mikataba ya uwekezaji kwenye Hifadhi ya...

UKURASA WA 3

### MAPYA KESI KUGOMBEA MAZISHI MFANYABIASHARA

KESI ya kugombea mazishi ya mfanyabiashara maarufu wa madini wa Arusha, Jubilate Benjamin Ulomi, imechukua sura mpya baada ya...

## PM aagiza wanaodai korosho kulipwa Feb. 15

UKURASA 3

## Upigaji wa kutisha mabilioni wadhibitiwa Bodi ya Mikopo

UK. 4

**MICHEZO** SIMBA YAKATISHA TAMAA VS AL AHLY UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Kakobe acharuka

**Na Gwamaka Alipipi**

MKUU wa Kanisa la Full Gospel Bible Fellowship (FGBF), Askofu Zachary Kakobe, ameeleza kuchukizwa na kitendo kilichofanywa na baadhi ya wanasiasa aliodai kuwatukana viongozi wa dini kwenye mitandao ya kijamii.

Amedai wanasiasa wote waliowatukana viongozi wa dini baada ya kufanyika kikao kati yao na Rais John Magufuli Ikulu jijini Dar es Salaam wiki iliyopita, wanapaswa kutubu, vinginevyo "wataanguka kwenye shimo refu na hawatainuka tena".

Askofu Kakobe aliyasema hayo jana wakati wa ibada iliyofanyika kwenye kanisa hilo jijini Dar es Salaam, akieleza kuwa kumekuwa na lugha za matusi zilizotolewa na baadhi ya viongozi wa kisiasa dhidi ya viongozi wa dini.

Januari 23, mwaka huu, Rais Magufuli alikutana na viongozi wa dini Ikulu jijini Dar es Salaam na kuwapa nafasi ya kuzungumzia mafanikio na changamoto zilizojitokeza katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wake.

"Viongozi wa siasa ambao wamewatukana viongozi wa dini kwenye mitandao ya kijamii, wanapaswa kutubu haraka sana, wakikaidi agizo hilo, chama chao kitatumbukia kwenye shimo refu ambao hakitainuka tena," alisema na kuongeza:

"Kuwatukana viongozi wa dini kwa sababu hawakuzungumza yale mliyotaka kuyasikia, ni utovu wa nidhamu, ni kiburi."

Askofu Kakobe alidai kuwa, baada ya kumalizika kwa mkutano kati ya Rais Magufuli na viongozi wa dini, kuna baadhi ya viongozi wa siasa, waliwatukana viongozi wa dini kupitia mitandao ya kijamii.

Alidai hajawahi kuwa mwanachama wa chama chochote cha siasa nchini, ingawa amekuwa akialikwa kushiriki shughuli mbalimbali zinazoratibiwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) wala ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

"Sijawahi kuwa mwanachama wa Chadema wala CCM," Askofu Kakobe alidai, "sina kadi ya vyama hivyo, sijawahi kuwasiliana na kiongozi yeyote wa Chadema wala kuonana nao ana kwa ana.

"Wala hawajawahi kuja ofisini kwangu, halijawahi kutokea. Naendelea kusisitiza kuwa Kanisa la Full Gospel Bible Fellowship halijawahi kuwa mwanachama wa chama chochote cha siasa. Hata Mbunge wa Jimbo ambalo Kanisa hili lipo, (Saed Kubenea - Chadema) sijawahi kuonana naye wala kuzungumza naye."

Askofu Kakobe alidai aliwahi kuitikia mwaliko wa Chadema mara moja miaka michache iliyopita wakati wa mkutano uliofanyika Mlimani City, na alienda kama "baba anayeweza kualikwa na watoto".

Alidai kuwa wakati yuko kwenye mkutano huo, hakuzungumza na kiongozi yeyote wa chama na hakuwa na mawasiliano na kiongozi aliyekuwa anawania nafasi ya urais wakati huo.

"Leo (jana) ninanena waziwazi, kanisa langu siyo Chadema wala CCM, wala chama kinginge chochote, lakini waumi wake ni wanachama wa vyama hivyo vya siasa," Askofu Kakobe alisema.

INAENDELEA UK.8



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (kulia), akimkabidhi Mkurugenzi Mtendaji aliyemaliza muda wake, Dk. Charles Kimei (wa pili kushoto), zawadi ya picha ikiwa na marais wa awamu mbalimbali wa Tanzania na Burundi katika hafla maalum ya kumuaga jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa benki hiyo, Ally Laay na (wa pili kulia) ni mke wa Dk. Kimei, Rose Kimei. **NA MPIGAPICHA WETU.**

# Wawekezaji hifadhi za bahari matatani

**Na Mwandishi Maalum**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, ametoa mwezi mmoja kwa wawekezaji walioingia mikataba ya uwekezaji kwenye Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU) kulipa deni la shilingi milioni 331.2 wanalodaiwa vinginevyo Serikali itavunja mikataba na wahusika wote watakamatwa na kutaifishwa mali zao ili kufidia fedha za umma.

Waziri Mpina ametoa agizo hilo alipokuwa akizungumza katika ziara ya kutembelea Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu kwenye Visiwa vya Mbudya na Bongoyo ambapo ilibainika kuwa baadhi ya wawekezaji waliopewa na maeneo kwenye hifadhi hizo kushindwa kuyaendeleza kwa mujibu wa mikataba sambamba na kushindwa kulipa tozo stahili za Serikali zilizowekwa kwa mujibu wa sheria.

Alisema Serikali haiwezi kukubali kuchezewa na wawekezaji ambao hawajajipanga na kuchelewesha uendelezaji wa fukwe na maeneo mengine ya urithi wa nchi yetu sambamba na kukwamisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

Waziri Mpina alisema Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu ina utajiri na urithi mkubwa wa Tanzania kwa kuwa na fukwe ndefu na nzuri za kipekee duniani, makaburi yenye historia ya kuvutia, mazalia ya samaki, matumbawe yenye mvuto wa kipekee na ndege wa aina za kipekee ambao hawapatikani maeneo mengine duniani.

Mpina alisema pamoja na kuwapo vivutio hivyo vya kipekee, bado kitengo hicho hakijaweza kuvitangaza vivutio hivyo kikamilifu ambapo hadi sasa hakuna mabango kwenye malango ya kuingia nchini ikiwamo viwanja vya ndege, bandarini na mipakani na mikoani, hakuna matangazo kwenye vyombo vya habari, hivyo kuchangia wananchi kutofahamu urithi huo na kuwapo kwa idadi ndogo ya watalii wa ndani na nje ya nchi wanaotembelea hifadhi hizo.

Kutokana na hali hiyo, aliagiza kuandaliwa mkakati wa kutangaza vivutio hivyo ili viweze kujulikana, idadi ya watalii kuongezeka pamoja na kukuza mapato ya Serikali, huku akisisitiza kuwa mkakati huo uwasilishwe wizarani kwake Februari 28, mwaka huu.

Katika hatua nyingine, alionesha kushangazwa na taasisi hiyo kushindwa kujiendesha na kuendelea kutegemea ruzuku ya Serikali

INAENDELEA UK.8

# Wafunguka pendekezo viongozi wa dini kuzuia kamari

**Na Enock Charles**

SIKU chache baada ya viongozi wa dini kumwomba Rais John Magufuli kupiga marufuku michezo ya kubahatisha nchini, wadau wa michezo hiyo wametoa maoni, wakiunga mkono na wengine kupinga pendekezo hilo.

Katika kikao cha Rais na viongozi wa dini Ikulu jijini Dar es Salaam Jumatano, baadhi ya viongozi hao wa kiroho walionyesha kukerwa na kukua kwa kasi kwa michezo ya kubahatisha nchini.

Walidai michezo hiyo inakua kwa kasi kutokana na kushamiri kwa matangazo kupitia vyombo vya habari kuhamasisha watu kuicheza.

Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mabohora Tanzania, Zainuddin Adamjee, alimweleza Rais Magufuli kuwa, michezo ya kubahatisha imekuwa ikishika kasi nchini bila ya kudhibitiwa.

Alisema vijana wengi ambao ni nguvu kazi ya taifa, wamekuwa wakijihusisha na kucheza kamari na imewafanya wengi kushindwa kufanya kazi kwa kutegemea michezo hiyo.

**WADAU**

Akizungumza na Nipashe iliyotembelea ofisini kwake jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Meneja wa Uhusiano wa Vodacom Tanzania, Alex Bitekeye, alisema michezo ya kubahatisha iko kwa mujibu wa sheria.

Kutokana na michezo hiyo kutambulika kisheria, Bitekeye alisema haoni kosa kwa mtu yeyote kujihusisha nayo.

Meneja wa Uhusiano wa Airtel Tanzania, Jackson Mmbando, akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, alisema kuna haja watu kutofautisha kamari na bahati nasibu.

Alisema: "Kuna tofauti kati ya 'gambling' (kucheza kamari) na bahati nasibu, sisi (Airtel) tunatoa huduma 'then' (kisha) mtu anapata zawadi kutokana na huduma, hata leseni yetu ni tofauti kabisa," alisema.

Ezron Charles, mmoja wa wanaocheza kamari za kutabiri matokeo ya soka, alidai michezo hiyo haoni haja kuzuia kamari kwa kuwa ni moja vyanzo vya mapato kwa serikali na watu binafsi.

"Mimi kuna vitu nimenunua kutokana na hii michezo ya kubahatisha, kwa hiyo naichukulia kama moja ya vyanzo vyangu vya mapato," alisema mfanyabiashara huyo wa Kariakoo jijini Dar es Salaam.

Nipashe pia ilizungumza na Waziri Mkuu wa Serikali ya Wanafunzi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Goodluck Paul, ambaye aliunga mkono pendekezo la viongozi wa dini kupiga marufuku michezo ya kamari nchini.

Alidai michezo hiyo inatengeneza jamii ya watu wavivu na wasiopenda kufanya kazi, hivyo kutegemea njia rahisi ya kujipatia kipato.

"Hii 'gambling' (kamari) inatengeneza jamii ya watu wavivu, mtu anakuwa tegemezi wa njia rahisi za kumpatia kipato, mtu huyo baadaye anaweza kuwa mla rushwa," alisema.

Mwishoni mwa wiki, serikali kupitia Bodi ya Michezo ya Kubahatisha (GBT) ilitangaza kuzuia matangazo ya michezo hiyo kupitia redio na televisheni, ikieleza kuwa kumekuwa na ongezeko la malalamiko kutoka kwa umma juu ya kukithiri kwa matangazo ya michezo hiyo.

HABARI KITAIFA

# Utunzaji majalada wamtibua waziri Ardhi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula, amekasirishwa na jinsi Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma inavyotunza majalada ya ardhi.

Mabula alikutana na kadhia hiyo mwishoni mwa wiki alipotembelea masijala ya ardhi katika halmashauri hiyo akiwa katika mfululizo wa ziara zake kutembelea halmashauri nchini kuhamasisha ukusanyaji maduhuli ya serikali kupitia kodi ya ardhi.

Mabula alisema utunzaji wa majalada ya ardhi katika Halmashauri ya Chamwino hauzingatii taratibu za kutunza majalada, jambo linaloweza kutoa nafasi kwa baadhi ya nyaraka kupotea na wakati mwingine watumishi wasiokuwa waaminifu kuyahujumu.

Wakati wa ukaguzi wa majalada ya ardhi katika halmashauri hiyo, Mabula alibaini majalada mengi yakiwa hayana maelekezo kutoka kwa afisa mmoja kwenda kwa mwingine, jambo linaloonyesha kuwa utendaji kazi katika sekta hiyo hauna maelekezo yoyote.

"Mawasiliano ya ofisi lazima yaonekane kutoka kwa ofisa mmoja kwenda kwa mwingine na hapa kuna index namba, lakini haitumiki na huwezi kujua aliyepokea nyaraka kwa mara ya kwanza nani, hapo lazima migogoro haiwezo kwisha," alisema.

Alisema utunzaji majalada ya ardhi usiozingatia taratibu kwa kiasi kikubwa ndiyo chanzo cha migogoro mingi ya ardhi katika maeneo mbalimbali kwa kuwa ni rahisi kucheza na majalada kwa nia ya kufanya udanganyifu.

Akumuagiza Mkuu wa Idara ya Ardhi, Christopher Sanga na Afisa Ardhi Mteule wa halmashauri hiyo ambaye anahudumu pia wilaya ya Kongwa, Letare Shoo, kuhakikisha mapungufu yaliopo katika majalada ya ardhi yanarekebishwa kabla ya Machi mwaka huu na ukifika muda huo atarajea kuona kama maagizo yake yametekelezwa.

Aidha, Mabula aliagiza kufikia Machi viwanja vyote vya Halmashauri ya Chamwino viwe vimepimwa na kupatiwa hati na Mkurugenzi wake ahakikishe halmashauri inalipa kodi ya pango la ardhi kwa viwanja inavyomiliki.

# PM aagiza mpaka Feb. 15 korosho zote zilipwe

**Na Abdallah Bakari,** MTWARA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amewaagiza wakuu wa mikoa na wilaya kuhakikisha malipo yote ya fedha za korosho yawe yamelipwa ifikapo Februari 15, mwaka huu.

Aidha, amesema serikali haitarajii kufikia Februari 5, kuendelea kusikia neno la uhakiki.

Aliagiza akaunti za benki 191 za wakulima zilizokuwa na mkanganyiko, taarifa zitolewe kwa wahusika ili waweze kuzirekebisha na wakulima walipwe fedha zao kwa wakati na kuzima malalamiko huku akitaka kuboresha mfumo wa upashanaji habari.

Agizo hilo la Waziri Mkuu, linafuatilia kauli aliyoitoa Rais John Magufuli hivi karibuni kwamba haelewi kwanini wakulima wa korosho hadi sasa hawajalipwa fedha zao ilhali fedha za malipo hayo zipo.

Waziri Mkuu Majaliwa aliondoka jana kwenda Mtwara kutafuta suluhu ya mkwamo huo kwa kukutana na viongozi wa mikoa inayozalisha zao hilo.

Lengo la kwenda huko ni kupata taarifa za uhakiki wa mashamba ya wakulima wa korosho na kukutana na wakuu wa mikoa, wilaya, warajisi na baadhi ya viongozi wa vyama vikuu wa mikoa ya Lindi, Mtwara, Tanga, Pwani na Ruvuma.

"Hapa majuzi mheshimwa rais ameweka msisitizo tena korosho ziondoke haraka kwa wakulima, zindoke haraka kwa vyama vya msingi, ziondoke haraka kutoka kwenye vyama vikuu ili ziingie kwenye maghala ambayo serikali inamiliki kwa ajili ya hatua nyingine," alisema Majaliwa na kuongeza:

"Nimelazimika nije Mtwara kukutana na wadau wa korosho ambao ndio watendaji wetu wakuu ili niweze kupata taarifa ya hatua mliyofikia...baada ya kuwasikiliza wadau wote hatutarajii kufikia tarehe 5 Februari tuendelee kusikia neno la uhakiki na hadi kufikia tarehe 15, malipo yote yawe yamekamilika...waheshimiwa wakuu wa wilaya zoezi ni lenu, wakuu wa mikoa simamieni," alisema Majaliwa.

Aidha, aliagiza akaunti za benki 191 za wakulima zilizokuwa na mkanganyiko, taarifa zitolewe kwa wahusika ili waweze kuzirekebisha na wakulima walipwe fedha zao kwa wakati na kuzima malalamiko huku akitaka kuboresha mfumo wa upashanaji habari.

"Tumeambiwa hapa wakulima 7,888 wamelipwa, lakini hawafahamu kama wamelipwa, ni kutokana na kukosa 'information' (taarifa) mkulima hajui, Amcos hajui...wakulima hawa hawajawahi kwenda benki hata kungalia salio, hii ni ishara mfumo wa upashanaji habari haupo sawa," alisema na kuongeza:

"Nimekuja huku nikiwa na taarifa kuwa kwenye zoezi hilo la uhakiki kuna mazingira ya rushwa...kusiwe na mazingira ya rushwa, tusiwaingize wakulima katika mazingira ya rushwa...lazima tujiridhishe katika 'process' (mchakato) hiyo kusiwe na rushwa, kamati za ulinzi zisimamiwe.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, alisema mpaka juzi zaidi ya Sh. bilioni 792 zimetengwa kwa ajili ya malipo na tayari kiasi cha Sh. bilioni 416 zimeshalipwa.

Alisema Wilaya ya Tandahimba, mkoani Mtwara, inayoongoza kwa uzalishaji wa tani 37,000, katika uhakiki wamefikia asilimia 96.

"Matarajio yetu kama wilaya inayoongoza kwa kilimo cha korosho imefikia asilimia 96 basi wilaya zote nchini zitakuwa zinaelekea kumaliza hivi karibuni," alifafanua Mgumba

Alisema malipo yote yaliyohakikiwa

INAENDELEA UK. 8



Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) Zanzibar, Salum Mwalimu (kulia), akizungumza na waandishi wahabari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu miezi sita iliyotolewa kwa ajili ya mjadala wa Muswada wa Sheria ya Vyama vya Siasa. Kushoto ni Mwanyekiti wa Chama Cha Ukombozi wa Umma (CHAUMA), Hashim Rungwe. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mapya yaibuka kesi kugombea mazishi ya mfanyabiashara

**Na Mwandishi Wetu**

KESI ya kugombea mazishi ya mfanyabiashara maarufu wa madini wa Arusha, Jubilate Benjamin Ulomi, imechukua sura mpya baada ya ndugu zake wa karibu kupinga anayedaiwa kuwa mke wa marehemu, Zainabu Rashid, kufanya sherehe ya mazishi kwamba si mke wa ndoa.

Jubilate alikufa Januari 15, mwaka huu zaidi ya siku kumi zilizopita katika Hospitali ya Aga Khan Nairobi, nchini Kenya na baadaye kuhamishiwa kwa huduma ya mazishi Mkoa wa Kilimanjaro, Tanzania, lakini mazishi yake hayakuweza kufanyika kutokana na mke huyo kufungua kesi mahakamani.

Awali kabla mke huyo kwenda mahakamani, Mkuu wa Wilaya ya Hai, Ole Sabaya, alitoa ushauri kwamba suala hilo lipelekwe mahakamani ili wapate ufumbuzi wa nani ana haki ya kumzika mfanyabiashara huyo.

Mahakama ya Wilaya ya Hai, ilitoa amri ya kuzuia ndugu wa marehemu kufanya mazishi mpaka hapo kifo hicho kitakapochunguzwa kwa kina na maofisa wa jeshi la polisi na madaktari.

Pia Mahakama hiyo ilizuia ndugu wa marehemu kufanya chochote kuhusiana na mali za marehemu hadi shauri mama litakaposikilizwa na kutolewa maamuzi.

Hata hivyo, katika hati yake kinzani kupinga kesi iliyopo mahakamani, mmoja wa ndugu wa marehemu, Onesy Benjamin Ulomi, amekanusha Zainabu Rashid, ambaye ndiye mwombaji katika kesi hiyo kuwa mke wa kisheria wa marehemu na amemtaka athibitishe ukweli huo.

"Jubilate Benjamin Ulomi alikuwa mdogo wangu ninavyofahamu hakuwahi kufunga ndoa kisheria na mlalamikaji," Onesy, ambaye ni miongoni mwa walalamikiwa

INAENDELEA UK. 8

MAHOJIANO MAALUM

# Mbinu chafu upigaji mabilioni zilivyodhibitiwa Bodi ya Mikopo

**Na Enock Charles**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imesema imefanikiwa kudhibiti matumizi mabaya ya fedha, iliyokuwa changamoto kubwa na ya muda mrefu katika bodi hiyo.

Katika mahojiano maalum na Nipashe jijini Dar es Salaam wiki iliyopita, Mkurugenzi wa Habari, Elimu na Mawasiliano wa bodi hiyo, Omega Ngole, alisema changamoto hiyo imefanyiwa kazi na wamefanikiwa kupata hati safi kwa miaka miwili mfululizo kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG).

"Mwaka huu, tuna hati safi kutoka kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na mwaka jana pia, sasa sijui ni lini hiyo (changamoto ya matumizi mabaya ya fedha zinazorejeshwa na wanufaika ya mikopo). Mimi nazungumzia sasa hivi, wewe unaniambia habari za mwaka juzi ha ha ha!" alisema Ngole.

**UPIGAJI ULIOKUWAPO**

Agosti 31, mwaka 2017, wakati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), ikipitia taarifa za fedha za bodi hiyo kwa mwaka wa fedha 2014/15, ilibainika Sh. bilioni 15 zilitumika kwa shughuli za uendeshaji huku kiasi kikubwa kikiwa ni posho.

Katika kikao cha kupitia hesabu za HESLB, baadhi ya wajumbe walionekana kuwa wakali wakisema wakati wananchi wanaumia kulipia kusomesha watoto wao, bodi hiyo ambayo kipindi hicho ilikuwa na watumishi 144 pekee, inatumia mabilioni ya shilingi kufanya mambo yasiyo ya msingi.

Baadhi ya posho zilizowakera wabunge hao ni pamoja na ile iliyopewa jina la posho nyinginezo (other payroll allowance) ambayo mwaka 2014/15 ilikuwa Sh. milioni 999.45 kutoka Sh. milioni 762.96 mwaka 2013/14.

Posho nyingine inayoitwa posho maalum (special allowance) kwa mwaka 2014/15 ilikuwa Sh. milioni 582.05 kutoka Sh. milioni 463.96 mwaka uliotangulia.

Kwa upande wa safari za ndani ya nchi, kwa mwaka 2014/15 Sh. milioni 979.5 zilitumiwa na bodi hiyo huku mwaka 2013/14 zikitumika Sh. milioni 665.09.

Safari za nje ya nchi kwa mwaka 2014/15 zilitumia Sh. 697.38 na mwaka 2013/14 zilitumia Sh. milioi 564.22. Posho nyingine iliyowashatua wabunge hao ni ile ya uhusiano na ukarimu (relationship and hospitality allowance) ambayo kwa mwaka 2014/15 ilikuwa Sh. milioni 296.77 kutoka Sh. milioni 243.64 mwaka 2013/14.

Walihoji pia sababu za ada ya ukaguzi kupanda kutoka Sh. milioni 61.7 mwaka 2013/14 mpaka Sh. milioni 330.56 mwaka uliofuata.

Jambo jingine lililowashatua wabunge hao ni matumizi makubwa ya bodi ya wakurugenzi ya HESLB, ambayo kwa mwaka 2013/14 yaligharimu Sh. bilioni 1.16 na mwaka uliofuata ikawa Sh. milioni 832.52.



Mkurugenzi wa Habari, Elimu na Mawasiliano wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Omega Ngole. **PICHA: MAKTABA**

Pia kitabu cha hesabu za bodi hiyo kiliionyesha fedha kwa ajili ya likizo kwa mwaka 2014/15 ni Sh. milioni 294.21 na mwaka 2013/14 Sh. milioni 311.35.

Kwa upande wa fedha za maziko na rambirambi kwa wafanyakazi na watu wao wa karibu, kwa mwaka 2014/15 Sh. milioni 45.2 na mwaka 2013/14 Sh. milioni 54.46.

Wabunge hao pia walihoji matumizi ya kawaida ya menejimenti ya bodi kuwa Sh. milioni 526.71 mwaka 2014/15 na Sh. milioni 684.3 mwaka 2013/14.

Vilevile walihoji sababu ya matumizi ya jumla ya bodi hiyo kupanda kutoka Sh. bilioni 1.06 mpaka Sh. bilioni 1.15 mwaka 2014/15 ambalo ni ongezeko la takribani Sh. milioni 90.

Kabla ya kupitiwa kwa taarifa za fedha za bodi hiyo na PAC, Februari 16, 2017, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alitangaza kusitisha mkataba wa ajira ya aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, George Nyatega, pamoja na kuwasimamisha kazi wakurugenzi watatu kutokana na kile alichokieleza siku hiyo kuwa, ni matatizo ya kiutendaji na matumizi mabaya ya fedha za umma yanayofanyika ndani ya bodi hiyo.

Prof. Ndalichako alisema taasisi hiyo imeonyesha utendaji usioridhisha kiasi kwamba kumekuwa na matatizo mengi na yanayojirudiarudia kwa wateja wao.

Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano ya Nipashe na Mkurugenzi huyo:-

**SWALI: Kuna kitu mnakiita mdaiwa sugu. Sifa za kuwa mdaiwa sugu wa HESLB ni zipi?**

**NGOLE:** Mdaiwa sugu ni mnufaika yeyote wa mkopo, ambaye hajaanza kurejesha deni lake lililomsaidia kupata hiyo elimu.

Sasa, sheria inaelekeza ukimaliza masomo, una miezi 24, inaitwa 'grace period' uanze kurejesha. Kwa mfano, kama umemaliza Novemba 2018, inatakiwa Novemba 2020 uanze kurejesha, baada ya hapo, 'system' (mfumo) yetu huku inaanza kupiga 'penalty' (adhabu) hata kama hujajitokeza, sasa sisi kuanzia hapo wewe kwetu ni sugu.

Lakini, ukimaliza halafu ukaajiriwa wewe, hiyo 'grace period; haikuhusu, inatakiwa uanze kurejesha mara moja. Kwa hiyo, ukimaliza chuo, mwezi wa Novemba, halafu Januari ukapata kazi au Desemba ukapata kazi, inatakiwa uanze kurejesha.

Sasa, watu wanatofautiana usugu, kuna walioanza kulipa 'then' (kisha) wakatokomea katikati, huyu naye ni sugu. Kwa hiyo, sugu ni wale wote waliokiuka masharti ya sheria na hatuna msaliamtume.

**SWALI: Ni wadaiwa sugu wangapi waliofikishwa mahakamani tangu kutangazwa kwa msako wa watu hao mwaka juzi?**

**NGOLE:** Kwanza, operesheni yetu iliisha kwa mafanikio, lakini ile ilikuwa ni operesheni. Kazi iliyokuwa inafanyika inaendelea kufanyika kwa sababu kwenye operesheni unafanya ukaguzi kwa waajiri, unaenda kwa mwajiri, unamwambia naomba orodha ya waajiriwa wako, akishakupa, ukakuta wanufaika wapo na wana 'bill' anakulipa.

Sasa, tulisema ni operesheni kwa sababu tuna ofisi kwenye mikoa mitano; Mwanza, Dodoma, Arusha, Dar es Salaam na Zanzibar. Kwa mfano, mtaenda Kigoma sawa, mahali ambapo hamna ofisi, mtaenda kupiga kambi katika ofisi ya Mwanza, meneja wetu anasimamia zoezi, mnaenda Kigoma mahali ambapo hamna ofisi na watu tuliowapata wakati ule unakuta mwajiri anakata, lakini haleti fedha kwetu.

Na pengine kwa sababu ya kutokuelewa au mwingine anakata chini ya kiwango kwa sababu inatakiwa kukatwa asilimia 15 ya mshahara ghafi, sasa mwingine anakata asilimia 10, kwa hiyo tunakutana na watu wasiolewa na wengine wanaoelewa, lakini wakorofi.

Kwa hiyo, cha kwanza ni hela na mkielewana, hakuna haja ya kwenda kwenye sheria. Miaka ya nyuma tuliwafikisha waajiri kama 11 mahakamani, lakini baada ya kufika mahakamani, wakasema tuyamalize nje ya mahakama, tukaelewana na wakalipa.

Kwa hiyo, tunadhani kwa sasa, 'approach' (mbinu) nzuri ni kuwaelimisha na kuwaelewesha watoe kwa hiari.

**SWALI: Fedha inayorejeshwa, hupelekwa wapi ikizingatiwa kuwa kila mwaka serikali huwapa fungu jipya kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wanafunzi?**

**NGOLE:** Serikali ileile inayopanga, ndiyo inayochukua. Ngoja nikwambie, bajeti ya mikopo kwa mwaka huu ni Sh. bilioni 425.7, sisi (HESLB) fedha tunazokusanya kutoka kwa wadaiwa wetu, zote zinakwenda serikalini kama ambavyo taasisi yoyote inakusanya mapato yake.

Kwa hiyo, sisi tunakusanya zinarudishwa serikalini, halafu tunapewa zingine.

**SWALI: Changamoto kubwa ni ipi katika ukusanyaji wa fedha kutoka kwa wadaiwa?**

**NGOLE:** Baadhi ya waajiri hawatoi ushirikiano kama sheria inavyoelekeza, hiyo niliyokwambia kwamba sheria inasema akate asilimia 15 ya 'basic salary' yeye anakata asilimia 10.

Kuna waajiri wanakata, mfanyakazi anaona kwenye 'salary slip' (stakabadhi ya malipo ya mshahara) fedha imekatwa, lakini fedha hizo hazijafika kwetu.

Lakini kuna wanufaika wengine ambao unakuta amejiajiri yupo mtaani, tunaendelea kufanya mashauriano na taasisi nyingine za serikali kama TRA (Mamlaka ya Mapato) na mifuko ya hifadhi za jamii ili mifumo yetu iwe inaongea, ili hata ukijificha sehemu halafu ukaenda 'ku-renew' leseni yako ya udereva tunakupata.

**SWALI: Kuna changamoto ya watu kudaiwa mara mbili na wengine kudaiwa wakati hajawahi kunufaika na mikopo yenu. Kulikoni mkurugenzi?**

**NGOLE:** Unakuta kwa mfano, Enock umeomba Chuo Mlimani (UDSM) na IFM kupitia TCU (Tume ya Vyuo Vikuu), sisi ukipata mkopo hatukupi mpaka tupate uthibitisho kutoka huko.

TCU wanatuletea huyu amepata usajili IFM, wewe katikati wazazi wanakwambia achana na IFM, nenda Udom kwa sababu mbalimbali tu, labda kozi uliyopata tunadhani hailipi sana, nenda chuo hiki.

Sasa, unakuta sisi fedha tulishapeleka kule maana tusingepeleka kule na ukaenda usingezikuta. Kwa hiyo, ni vyema unapobadilisha tupate taarifa.

Kwa hiyo, ni muhimu sana mwanafunzi anapokwenda chuo awe ameshafanya maamuzi ya mwisho, siyo unakiambia chuo nakuja chuoni kwenu, halafu katikati unabadilisha, utapishana na fedha au unakuta hapo katikati mtu anaacha kusoma.

## Serikali yaomba taasisi za dini mimba utotoni

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

SERIKALI mkoani Rukwa imeziomba tasisi za kidini kujikita katika kusimamia maadili ili kumaliza tatizo la mimba za utotoni zilizoshamiri mkoani hapa..

Akizungumza jana mjini Sumbawanga katika sherehe za uzinduzi wa Jimbo la Lake Tanganyika Field Kanisa la Waadventista Wasabato, mwakilishi wa mkuu wa mkoa wa Rukwa, David Kilonzo, alisema miongoni mwa tasisi ambazo zinajukumu kubwa ni za dini katika kusimamia maadili.

Alisema mkoa huo una changamoto kubwa ya wanafunzi kukatisha masomo kutokana na mimba za utotoni, hivyo makanisa yana jukumu kubwa la kusimamia na si kuiachia serikali pekee.

"Katika kipindi cha Julai hadi Septemba mwaka jana, jumla ya wanafunzi 72 walipata ujauzito, na watuhumiwa wa vitendo hivyo hawapatikani kutokana na wazazi kumalizana na watuhumiwa nje ya sheria, hali ambayo inasumbua kulikomesha tatizo," alisema.

Kilonzo alisema wapo baadhi ya watoto wanaopata ujauzito wanadai waliowapa ni wageni kutoka nchi jirani, na wamekimbia baada ya kuwapa mimba, wengine wanadai waliowapa ujauzito wamefariki dunia mradi tu kuwaficha watuhumiwa wa vitendo hivyo, hali ambayo inasababisha ugumu katika kutokomeza mimba hizo.

Alisema kama kanisa litawajenga kimaadili watoto hao watakuwa na hofu ya Mungu na kuepuka kushiriki vitendo vya ngono, sambamba na kuacha kusema uongo kwa nia ya kuwaficha wanaume wanaowapa mimba ili sheria iweze kuwashughulikia.

Aidha, alisema pia kanisa lina nafasi kubwa ya kuwekeza katika kilimo ambapo litapata mafanikio kwa kuwa Mkoa wa Rukwa unafaa kwa kilimo, na kuwahimiza waumini wake walipe kodi kwa sababu serikali inahitaji kodi ili iweze kuwapatia maendeleo.

Awali akisoma risala ya kanisa hilo Katibu wa jimbo wa kanisa hilo, Rabson Nkoko, aliishukuru serikali ya awamu ya tano kwa mafanikio makubwa ikiwamo vita dhidi ya rushwa.

Alisema kuwa pia serikali imekuwa ikiheshimu uhuru wa kuabudu na wananchi wanafurahia uhuru huo.

Alisema kanisa hilo tangu lianzishwe nchini mwaka 1903 limekuwa likitoa huduma mbalimbali kama elimu, afya na mawasiliano na aliahidi kuwa litaendelea kufanya hivyo kwa ustawi wa wakazi wa Jimbo la Lake Tanganyika Field linaloundwa na mikoa ya Songwe, Rukwa na Katavi ili wananchi wazidi kufaidi matunda ya uwapo wake.

# Buzwagi yaporomosha mapato ya halmashauri

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

KUSIMAMISHA shughuli za uchimbaji wa madini katika mgodi wa dhahabu wa Buzwagi wilayani Kahama Mkoa wa Shinyanga unaomilikiwa na Kampuni ya Acacia, kumechangia kwa kiasi kikubwa kushuka kwa makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri ya Mji wa Kahama.

Halmashauri ya Mji wa Kahama ilikuwa inategemea mapato makubwa kwenye mgodi huo, ambayo yalikuwa yanatokana na ushuru wa huduma zilizokuwa zikitolewa na makampuni madogo yaliyokuwa yakifanya kazi ndani ya mgodi huo.

Hayo yalibainishwa na Ofisa Mipango wa halmashauri, Flora Sangiwa, kwa niaba ya mkurugenzi wakati akisoma taarifa ya makusanyo ya mapato ya ndani kwenye kikao cha baraza la madiwani cha kupitisha rasimu ya bajeti ya mwaka 2019/20, alisema kipindi cha mwaka 2018/2019 mapato ya ndani ya halmashauri yalikuwa shilingi bilioni 7.10, lakini yameshuka hadi shilingi bilioni 6 kwa mwaka 2019/2020.

Alisema Mgodi wa Buzwagi ulikuwa unategemewa na Halmashauri ya mji kwa kiasi kikubwa katika kulipa ushuru wa huduma kwa sababu ulikuwa ukitoa fedha nyingi kutokana na wingi wa makampuni madogo yaliyokuwa yakifanya kazi ndani ya mgodi.

Halmashauri ya Mji ilipitisha mapendekezo ya kukusanya na kutumia kiasi cha shilingi bilioni 43.02 kwa mwaka 2019/2020 likiwa ni ongezeko la asilimia 10.

Pia Sangiwa alisema ongezeko la asilimia 10 limetokana na wengi wa watumishi wa Halmashauri hiyo kupandishwa vyeo (madaraja), hivyo kufanya mishahara yao ipande pamoja na ajira mpya za watumishi.

Aidha, alisema kuwa, Halmashauri imejipanga kuboresha ukusanyaji wa mapato kwa uwazi na kutoa elimu kwa wananchi juu ya ulipaji wa kodi kwa wakati, hatua ambayo itasaidia kutoa huduma kwa wananchi kwa muda ulipangwa.

Katika hatua nyingine, Sangiwa alisema Halmashauri imeiomba serikali kiasi cha shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vya madarasa 50, matundu ya vyoo 60, pamoja na nyumba za walimu 10 katika shule za sekondari zilizo katika Halmashauri hiyo.



Dereva wa bodaboda akiwa amebeba mzigo wa mkaa huku abiria akiwa juu bila kujali usalama wake katika eneo la Bonga Mengwa mkoani Pwani, mwishoni mwa wiki. **PICHA: HALIMA KAMBI**

## Tanesco yalalamikia kuhujumiwa miundombinu

**Na Joseph Mwendapole,** ARUSHA

SHIRIKA la Umeme Nchini (Tanesco), limewahimiza Watanzania kuwa na uzalendo kwa kuwafichua watu wanaohujumu miundombinu ya shirika hilo ili wachukuliwe hatua za kisheria.

Wito huo ulitolewa jana jijini Arusha na Meneja Uhusiano wa Shirika hilo, Leila Muhaji, wakati wa ziara ya wahariri na waandishi waandamizi wa habari wanaotembelea miradi mbalimbali inayotekelezwa na shirika hilo mkoani hapa.

Akizungumza kwenye kituo cha kupoza umeme cha Njiro, Leila alisema wananchi ni wanufaika wakubwa wa nishati inayozalishwa na Shirika hilo hivyo kwa kuwa wanakaa jirani na miundombinu hiyo na wana wajibu wa kutoa taarifa kila wanapoona mtu anataka kuihujumu.

"Tunawaomba wananchi wakimuona mtu yeyote anataka kuharibu miundombinu ya shirika atoe taarifa mapema ili wahusika wachukuliwe hatua, miundombinu hii imegharimu nchi fedha nyingi sana hivyo lazima tuilinde kwa gharama yoyote kwasababu ni kwa manufaa yetu sote," alisema.

Alisema wananchi wanapaswa kujua kuwa serikali inawekeza fedha nyingi ili wananchi na wenye viwanda wawe na uhakika wa umeme hivyo kuna umuhimu mkubwa wa kuitunza miundombinu ili idumu muda mrefu.

Alisema kupitia mradi wa kuboresha na kuimarisha miundombinu ya Shirika hilo (TEDAP), serikali imetumia mabilioni ya fedha kukarabati na kuweka mitambo mipya ya kisasa ambayo lazima ilindwe ili iwe endelevu.

"Vituo vya kupoza umeme viko karibu na wananchi hivyo sisi Tanesco tunaamini hawa ndio walinzi wa kwanza wakiona mambo ambayo yanaonekana kutaka kuhujumu miundombinu watuambie mapema," alisema.

Meneja wa Tanesco Mkoa wa Arusha, Herini Mhina, alisema kulikuwa na baadhi ya watu wanaojaribu kuhujumu miundombinu ya shirika hilo kwa kuiba nyaya, lakini hivi sasa wamejitahidi kuimarisha ulinzi.

Alisema kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama wamefanikiwa kuwakamata watu wanaojihusisha na vitendo hivyo na kuwafikisha kwenye mamlaka husika kwaajili ya hatua zaidi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba iandaliwe kucheza kutafuta matokeo Caf

**KWA** mara nyingine wawakilishi pekee wa Afrika Mashabiki na Kati kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba watashuka uwanjani jiji Cairo, Misri Jumamosi kucheza mechi yao ya pili ugenini dhidi ya Al Ahly.

Mechi hiyo ya hatua ya makundi ni ya tatu kwa Simba, lakini kwa ugenini ni ya pili baada ya kupoteza ya kwanza DR Congo kwa mabao 5-0 dhidi ya AS Vita. Katika Kundi lao la D, Simba ilianzia nyumbani kwa ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya JS Saoura ya Algeria kabla ya kwenda kukutana na kipigo hicho cha aibu nchini DR Congo.

Hata hivyo, sasa Simba itaifuata Al Ahly ikitoka kufanya vibaya kwenye michuano ya Kombe la SportPesa baada ya kutolewa na Bandari FC ya Kenya katika hatua ya nusu fainali kwa mabao 2-1 kabla ya jana kujipoza kwa kuitoa Mbao FC kwa mikwaju ya penalti 5-3 kufuatia sare tasa katika mechi ya kutafuta mshindi wa tatu. Katika michuano hiyo ambayo mwaka huu ilianzia moja kwa moja hatua ya robo fainali, Simba ilianza kwa kuitoa AFC Leopards ya Kenya kwa mabao 2-1 kabla ya kukutana na kipigo kama hicho kutoka kwa Bandari FC.

Kama ilivyokuwa katika mchezo dhidi ya AS Vita kwa Simba kutoonyesha kupigania ushindi ndivyo ilivyokuwa katika mechi dhidi ya Bandari FC na hata dhidi ya Mbao.

Kadhalika, licha ya kuibuka na ushindi kwenye mechi dhidi ya AFC Leopards, Simba haikucheza soka la kiushindani kama ilivyotarajiwa kwani kwa tathimini yetu ilishinda mechi hiyo kwa bahati tu. Tunatambua timu ikitoka kupoteza, mechi inayofuata kwa asilimia kubwa wachezaji hukosa kujiamini, hivyo kinachotakiwa kwa bechi la ufundi Simba kwa sasa ni kuwaandaa zaidi kisaikolojia. Ikumbukwe Simba itashuka dimbani kukutana na Al Ahly ambao watakuwa na morali wa ushindi kwa asilimia 100 kutokana na kupata matokeo mazuri kwenye mchezo uliopita.

Al Ahly ambayo itakuwa mbele ya mashabiki wake Jumamosi dhidi ya Simba, ikumbukwe licha ya kutoka kupata sare ya bao 1-1 ugenini dhidi ya JS Saoura katika mechi ya Ligi ya Mabingwa, lakini pia Alhamisi ilishinda 3-0 kwenye mchezo wa Ligi Kuu Misri ikiwa ugenini dhidi ya Misr El-Maqasa.

Hivyo, benchi la ufundi Simba linapaswa kufanya kazi ya ziada kwa sasa kuiandaa Simba kucheza soka la kiushindani zaidi kwa kusaka matokeo na si kuishia tu soka la kuburudisha kwa kumiliki mpira zaidi. Ni kweli mashabiki wa soka wanahitaji burudani, lakini mwisho wa siku mafanikio yote hayo ni kupata matokeo na kuweza kusonga mbele, kwani hamna maana yoyote kumiliki mpira kama ilivyotokea kwenye mchezo dhidi ya Bandari FC na mwisho wa mechi kushindwa kupata matokeo.

Kuanzia mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya AS Vita hadi katika michuano ya SportPesa, wachezaji wa Simba walikuwa wanaingia uwanjani wakionekana tayari wamechoka jambo ambalo hali hiyo ikijitokeza dhidi ya Al Ahly watarejea na kipigo kikubwa kuliko walichokipata DR Congo.

Nipashe tunashindwa kuelewa tatizo lililopo kikosini nini, hivyo tunashauri kufanyika maandalizi makubwa kiufundi na kisaikolojia ili timu kuweza kurejea mchezoni na kuanza kupata matokeo. Wachezaji wa Simba wanapaswa kuona thamani ya jezi zao na kutambua kuonyesha uwezo katika michuano hiyo mikubwa kwa ngazi ya klabu Afrika ni kujitangazia soko lao binafsi.

Mafanikio aliyoyapata mchezaji kama Mbwana Samatta, yalianzia katika michuano hiyo akiwa na Simba ilipocheza dhidi ya TP Mazembe, hivyo ni wakati sasa kwa kila mmoja kutambua haipigani klabu hiyo tu, bali pia mafanikio yake binafsi.


Pamoja na soka la Afrika kutawaliwa na fitina, ujanja na mbinu nyingi nje ya uwanja, katika idara hiyo hatuna shaka na uongozi wa Simba kwani mbinu zote wanazijua, hivyo ni wakati wa benchi la ufundi na wachezaji kuhakikisha wanatekeleza vema jukumu lao uwanjani. Tunaitakia Simba maandalizi mema katika kuipeperusha bendera ya Tanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mhariri Wikiendi:** Epson Luhwago
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

**BUSARA**

**UMASIKINI UNAPOJENGA HEMA KICHWANI**

**UMASKINI HAUJI TU KAMA UYOGA. SIKU ZOTE UNASTAWI PALE AMBAPO MAZINGIRA YANATOA FURSA. UBAYA ZAIDI UMASKINI UKITAFUTA KIWANJA CHA KUJENGA HEMA KICHWANI KAZI INAKUWA KUBWA ZAIDI. TUUPIGE VITA UMASIKINI KUANZIA KICHWANI – ELIMU. NA BALOZI CHRISTOPHER LIUNDI**




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Kindoki asigeuzwe kimbilio la udhaifu wa Yanga

**WASWAHILI** wana msemo unaosema 'mnyonge myongeni lakini haki yake mpeni.'

Maana ya msemo huo ni kwamba inawezekana kwamba kuna mtu ana matatizo, lakini wakati mwingine anapofanya vizuri hasifiwi kutokana na mara kwa mara amekuwa anaharibu au ni wa matatizo tu.

Kuna wakati kosa linakuwa la mtu mwingine, lakini anatupiwa yule aliyezoeleka kuwa ni mkosaji wa siku zote.

Hilo ndilo lililopo kwenye kikosi cha Yanga kwa sasa. Baada ya ushindi mfululizo na kutopoteza mechi yoyote ya Ligi Kuu, Yanga ilipoteza mechi kwa mara ya kwanza wiki iliyopita kwa kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Stand United.

Mbali na hilo, Yanga ilikutana na kipigo kingine cha mabao 3-2 dhidi ya Kariobangi Sharks ya Kenya kwenye michuano ya SportPesa. Kinachoonekana ni kwamba wanachama na mashabiki wengi wa Yanga wanamlaumu kipa Claus Kindoki kuwa ndiye aliyesababisha timu kupoteza mechi hizo.

Ni ukweli usiopingika kuwa Kindoki wakati mwingine amekuwa akifungwa mabao mepesi, huku akiwa haaminiki kwa Wanayanga wengi, lakini kwenye mechi hizi mbili alizokaa kwa kiasi kikubwa mabao aliyofungwa yalitokana na makosa ya mabeki na si yeye.

Ni kwa sababu nilizozieleza hapo juu, basi Kindoki amekuwa ndiye kama jalala la kutupiwa uchafu wote. Yanga ikipoteza kama golini yupo Kindoki, basi lawama zote anatupiwa yeye.

Cha ajabu huyu huyu Kindoki kuna mechi nyingi za Ligi Kuu amekaa golini na Yanga imeibuka na ushindi, hapo wanachama na mashabiki wanamsifia na kumuona kiwango chake kimeimarika, lakini ikipoteza lawama inamundea yeye pekee yake.

Tumeona kwenye mechi dhidi ya Stand, mchezaji akipiga krosi akiwa hajakabwa na beki yeyote wa Yanga, huku Jacob Massawe akiachwa huru kupiga kichwa katikati ya mabeki wawili ambao, achilia mbali kuokoa kwa kupiga kichwa, walishindwa kabisa japo kumsumbua asiruke akiwa huru. Kindoki asingeweza kuondoka golini wakati straika huyo bado alikuwa na mabeki wawili ambao wangeweza kumdhibiti.

Kwenye mechi dhidi ya Kariobangi sijaona bao lolote ambalo ni uzembe wa Kindoki, zaidi ya kuona straika akiwapindua-pindua mabeki wa Yanga hadi wakawa wanaanguka chini, kabla ya kuuweka mpira wavuni. Hapa kweli utamlaumu Kindoki?

Sikatai kuwa kipa huyo raia wa DR Congo amekuwa na mapungufu fulani akiwa golini, lakini asifanywe sasa kama kimbilio la wachezaji wengine au viongozi wa klabu hiyo kuficha udhaifu wao.

Kama kipa huyo hafai, unajiuliza ni nani alimleta? Na alifanyiwa majaribio sawasawa kuonekana anafaa?

Na mbona kuna baadhi ya mechi ambazo Yanga inashinda Kindoki akiwa golini, lakini hapewi pongezi zake na badala yake inasubiriwa hadi timu isifanye vizuri ndiyo alaumiwe?

Na nani anayewazuia viongozi wa Yanga kukaa na kumalizana na kipa wao tegemeo, Benno Kakolanya, ambaye yeye anachotaka atimiziwe maslahi yake tu ili arejee na kukaa golini?

Na kama wanashindwa kufanya hivyo, halafu golini anakaa Kindoki timu inafungwa nani alaumiwe kati ya kipa huyo au viongozi ambao hawataki kutimiza majukumu yao?

Kocha Mkuu Mwinyi Zahera tangu zamani alishasema hamtaki Kakolanya, wanachama na mashabiki wa Yanga walikubaliana naye, wengine kukaa kimya kwa sababu timu ilikuwa inashinda, lakini kwa sasa imeanza kupoteza wanaonekana kumuogopa kocha huyo kumwambia ukweli, badala yake mzigo wote anatupiwa Kindoki. Huu ni uonevu na unasababisha kipa huyo kuendelea kutojiamini kila anapokaa golini.

## MJADALA

# Viongozi wa dini wanapochanganya 'kubeti' na kamari

Na Michael Eneza



Rais John Magufuli akiongea na viongozi wa dini. **PICHA: MTANDAO**

**MOJA** ya vikwazo muhimu katika maisha ya jamii tangu zamani ni tofauti za hisia, mawazo na mwelekeo kati ya vijana na wazee wao, kwani waliotangulia kuona dunia wana mtazamo unaoendana na mazingira ya maisha ya kipindi kilichotangulia. Waliofuata baadaye wanaona mambo kwa njia tofauti ambayo waliotangulia wanaona kama kuvurugwa kwa maadili au nidhamu, kwa mfano masikitiko makubwa yaliyowafikia wahenga miaka ya 1980 mashine za kufanya hesabu (kujumlisha na kutoa) zilipoanza kuzagaa. Ikawa hakuna haja tena ya kijana kujifunza hesabu kwa nguvu shuleni kuwa ndiyo msingi wa maisha, kumudu biashara na kutodanganywa kazini.

Kuna mazingira kama hayo katika wakati huu, ambako dunia imetawaliwa kwa kiwango fulani na mchezo wa soka barani Ulaya, wenye mipangilio ya ushindani na kuunganisha mashindano ya nchi zote kana kwamba ni ya nchi moja. Halafu kuna mashindano ya pamoja ya Kombe la Ligi ya Mabingwa barani humo, mashindano yenye sifa kuliko yote duniani, nje kidogo ya Kombe la Dunia ambalo ni kila miaka minne, sawasawa na Kombe la Mataifa ya Ulaya. Kutokana na kusambaa kwa televisheni na vipindi hivyo kupatikana moja kwa moja kila mechi inapochezwa, hata matangazo yake na mashindano ya kubuni nani atashinda, pia ni ya dunia nzima sasa.

Ni ushindani huu wa kujua au kutazamia nani atashinda mechi inayofuata, kwa kuangalia alipopitia hadi wakati huo kujua uwezo wake na udhaifu wake, na jinsi mpinzani wake alivyo, na anavyoweza kutumia nyufa hizo, ndiyo 'kubeti.' Ni kuwa tayari kuacha 'vijisenti' mahali fulani kwa ubishi tu kuwa timu fulani itashinda, na hata kwenda mbali zaidi kujaribu kupambanua mfumo wa matokeo unaowezekana. Wako wachambuzi katika nchi tofauti ambao wamefaulu katika uchambuzi huo wakakusanya pesa nyingi kiasi kwa haraka, na mara kadhaa hao wanaoendesha mashindano ya kubuni nani atashinda wamewaajiri kama wachambuzi, washiriki 'kubeti.'

Badala ya kutengeneza pesa kwa kubeti, mtaalamu kama huyo anakuwa sasa ndiyo anayeandaa mpangilio wa mtego wa nani atashinda pamoja na viwango vya malipo, kuondoa urahisi na kampuni husika kulipa zaidi ya kile ambacho lazima ilipe kutokana na mpangilio wa matokeo. Ni utaalamu wa kuweza kujua mlingano wa nguvu katika mchezo tarajiwa, ambako kuutumia ufahamu au uwezo huo wa kuchambua kunachangia katika kuleta hamasa ya kufuatilia michuano, mechi tofauti. Halafu inajenga mshikamano mpya kati ya mashabiki wa timu tofauti waliotawanyika kote duniani, jambo ambalo lilikuwa halifikiriki wakati 'wahenga' wakiwa vijana tu.

Matokeo yake ni kuwa kila wiki kuna 'chemsha bongo' inayokumba maelfu ya vijana kutafakari nani atashinda mechi hii au ile, shughuli ambayo ni tofauti na michezo halisi ya kubahatisha inayobuniwa na vituo tofauti vya kutoa huduma hasa za simu za mkononi, kupitia redio na televisheni.

Hapa hakuna viwango halisi vya uwezo wa kuchambua na zaidi ni kubahatisha kupatikana kwa namba tatu zenye mtiririko fulani unaotakiwa, kile kinachoitwa 'tatu mzuka,' kana kwamba mtu anaopoa lipepo kwa kuzipatia hizo namba. Kwa utamaduni wa Tanzania, na hasa kwa nyimbo za msanii wa zamani Mbaraka Mwinshehe, 'mzuka' siyo dhana ya kutisha watu.

Inaelekea kuwa ni kundi hili la pili ambalo baadhi ya viongozi wa dini waliokutana Ikulu na Rais John Magufuli hivi majuzi walikuwa wanafikiria, walipotoa rai kuwa licha ya kamari kuwa haramu katika mafundisho ya dini, imekuwa ndiyo shughuli ya kila siku kwa vijana nchini. Ni kweli kuwa kuna mashine nyingi za kamari za hapa na pale, ambazo hadi hivi karibuni zilikuwa zinazuiwa zisionekane wakati wa kazi (hadi ifike saa kumi jioni) na pia ni kweli watu wanajipatia vijisenti vya hapa na pale kwa kutumbukiza, kuchagua namba hii au ile kwa mpangilio wa aina moja au nyingine. Hata hivyo, kamari inafilisi, na ni mchezo unaopendwa zaidi na wenye fedha, kwani inakuwa ni njia ya kutumia fedha kwa starehe changamshi, ya wasiwasi wa kupata au kukosa, si walalahoi zaidi.

> **Ni kweli kuwa hakuna kitu chenye mantiki cha kulipwa kwa kupatilia vizuri matokeo ya mchezo wa mpira wa timu za Ulaya, kuwa kwa mtu mwenye hisia ya uzalendo ya kihafidhina, jambo hilo ni kama halina maana.**

Ambacho labda viongozi wa dini hawakukumbuka ni kuwa tofauti na hapo awali, ambako kijana akitaka ajiunge na fani fulani anafanya hivyo bila vizuizi, hivi sasa inatakiwa kijana awe na sifa za ziada ili ajiunge na fani fulani, kwa mfano siyo tu awe ana vyeti ila anafahamiana na mwendeshaji.

Kupata kazi ni kusaidiana, siyo tu kuwa na uwezo wa kufanya kazi hiyo, na katika kutoa upendeleo kila mtu anaanza na wanaomhusu zaidi, ndiyo kawaida. Suala hapa ni kuwa viongozi wa dini hawana haja ya kuwa na wasiwasi na kubeti kwani ni chemsha bongo, na siyo sawa na kamari, na unaweza kusema havina uhusiano. Mtu hapati katika kamari kwa kuweka namba katika mpangilio sahihi kimantiki au kwa daraja la aina fulani, ila kwa kubahatisha, achague akilini nini kinawezekana.

Ni wazi pia kuwa viongozi wetu wa dini wana kila sababu ya kuwa na wasiwasi na muda unaotumiwa katika chemsha bongo za michezo na hata michezo ya kubahatisha ya kushiriki katika mawasiliano ya mitandao ya makampuni ya simu.

Ni kweli kuwa hakuna kitu chenye mantiki cha kulipwa kwa kupatilia vizuri matokeo ya mchezo wa mpira wa timu za Ulaya, kuwa kwa mtu mwenye hisia ya uzalendo ya kihafidhina, jambo hilo ni kama halina maana.

Wanachosahau ni kuwa Afrika ni sehemu ya soko la dunia na hata soko la ushabiki kwa timu hizi, ununuzi wa jezi na uenezi wa bidhaa ambazo zinafuatana na ushabiki kwa timu hizi.

Pia, Afrika ni bara linalokuwa kwa kasi kwa wingi wa watu na kupanuka kwa soko, hivyo makampuni ya Ulaya yana kila sababu kuunda vivutio tofauti Waafrika waingie zaidi katika dira hiyo. Siyo jambo la kujadili hapa kama hali hiyo ni njema au ni mbaya, kama ufahamu wa soka kwa kina kwa vijana wetu ni njema au siyo, ila tuseme tu kuwa tumeanza kufanana na Ulaya. Kazi za kuajiriwa zimepungua, na vijana wanaishi kwa ushiriki wa hapa na pale wa kazi ndogo ndogo za huduma, hivyo hawafanyi kosa kutumia muda wao kutafakari michezo na hata kufikia aina fulani ya utaalamu wa kujua uwezo na udhaifu wa timu. Na hata kama ingekuwa ni mchezo wa kubahatisha tu kama sehemu ya mtiririko wa tangazo la biashara la bidhaa au huduma fulani, huo siyo wizi.

**WASILIANA NASI:**
TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU
mhariri@nipashe.co.tz

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed



# Kakobe acharuka

INATOKA UK.2

Kiongozi huyo wa kiroho alidai kuwa wakati wa vuguvugu la katiba, aliwahi kwenda kwenye mkutano wa Chadema uliokuwa unafanyika kwenye Viwanja vya Jangwani jijini na alizungumza na John Mnyika (mmoja wa viongozi na wabunge wa Chadema) kwa simu kuhusu kuhudhuria mkutano huo, na aliitikia wito.

Askofu Kakobe alidai amewahi kuhudhuria mikutano mingi ya CCM kuliko Chadema wakati Yusuph Makamba alipokuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, na hakuwa na kadi ya CCM wala TANU. Alisema alikuwa anakwenda kwenye mikutano kutokana na uswahiba uliokuwapo kati yake na Makamba.

"Nakumbuka wakati mmoja niliwahi kuhudhuria mkutano wa wazee kumuaga Rais Benjamin Mkapa pale Diamond Jubilee, na nilialikwa na Yusuph Makamba. Wakati wa uongozi wake hapa Dar es Salaam, nilihudhuria mikutano mingi kwa sababu Makamba alikuwa rafiki yangu," alidai Askofu Kakobe.



Kiongozi huyo wa kanisa alisema kuhudhuria kwake kwenye sherehe za kiserikali ambazo Rais Magufuli anakuwa mgeni rasmi, haimaanishi kuwa yeye ni mwanachama wa CCM, bali anaitikia wito anaoalikwa.

**HATAKI UTEUZI**

Askofu Kakobe alidai kuwa hata Rais Magufuli akimteua kushika nafasi ya uongozi ndani ya nchi, hawezi kukubali kwa kuwa ana kazi maalum ya kumtumikia Mungu.

Alisema kuhudhuria kwake mikutano ya Rais Magufuli kumeibua mitazamo tofauti, wengine wakieleza amehaidiwa ubunge na wengine wakidai amenunuliwa.

"Siwezi kuwa mbunge wala waziri, na hata siku ikitokea nimeteuliwa na Rais, nitasema asante, lakini sitakubali," alisisitiza.

"Waumini wangu si mnajua nina pesa, si mnafahamu nilisema mimi ni tajiri kuliko serikali, si TRA wanajua walikuta fedha nzuri tu benki, si walikuta akiba nzuri katika akaunti ya kanisa, utaninunua kwa bei gani? Sina bei mimi," Askofu Kakobe alitamba.

Alidai kuwa miaka 20 iliyopita, aliwahi kuwa na kadi ya Chama cha TLP kilichokuwa kinaongozwa na Augustine Mrema, na aliamua kukata kadi ya chama hicho "kwa uchokozi" ambao baada ya kuufanya, aliichama kadi hiyo mbele ya waandishi wa habari.

"Niliamua kuchukua kadi ya TLP kwa sababu CCM wakati ule ilikuwa inabagua makanisa ya Pentekoste, lakini kwa sasa Rais Magufuli siyo mbaguzi wa madhehebu wala dini, anawapenda watu wote," Askofu Kakobe alisema.



Gari likiwa limetumbukia kwenye mtaro wakati likirudi nyuma katika Barabara ya Siwa, eneo la Viwandani, Mikocheni, jijini Dar es Salaa mwishoni mwa wiki. **PICHA: JOHN BADI**

# Wawekezaji hifadhi za bahari

INATOKA UK.2

licha ya kuwapo fursa nyingi na vyanzo vingi vya mapato, hivyo alitoa mwezi mmoja kuandaliwa mkakati wa kuongeza ukusanyaji wa mapato na kuifanya taasisi hiyo kujitegemea kuanzia mwaka ujao wa fedha wa 2019/2020.

Kuhusu kile kinachodaiwa kuwapo baadhi ya viongozi kuingilia na kuhujumu majukumu ya kitengo hicho kwa kuwaeleza uongo wananchi, Mpina amewataka watumishi wa taasisi hiyo kushikilia msimamo wa Sheria iliyoanzisha taasisi na kwamba kama kuna maelezo na mawazo ya kisera basi malalamiko hayo yawasilishwe kwa viongozi wakuu wa wizara.

Aidha, aliwahimiza watendaji wa kitengo hicho kubuni miradi mingine ya kiuchumi hasa katika maeneo ambayo zamani yalikuwa yakitumika kwa shughuli za uvuvi ili kuwawezesha wananchi wa maeneo hayo kujiongezea kipato na kuona thamani ya uwapo wa hifadhi hizo.

Pia aliagiza kufanyike tathmini ya ubora wa miundombinu na vifaa muhimu katika shughuli ya uhifadhi ili kuboresha utendaji kazi wa kitengo hicho. Vile vile ameagiza kuandaliwa kwa mpango biashara utakaowezesha kitengo kujiendesha kibiashara zaidi.

Kwa upande wake Meneja wa MPRU, John Komakoma, alimhakikishia Waziri kuwa maagizo yote aliyoyatoa atayasimamia kikamilifu kuona yanatekelezwa kwa wakati ili kuiwesha taasisi hiyo kutoa mchango unaostahili kwa pato la Taifa.

Komakoma alisema ili kuleta ufanisi wa kazi kitengo hicho kiko kwenye hatua ya mwisho ya mapitio ya Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Namba 29 ya mwaka 1994 ili kuiwezesha taasisi hiyo kuhifadhi maeneo tengefu yaliyoko kwenye mito mikubwa, mabwawa na maziwa kote nchini .

Pia alisema katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 kitengo hicho kimepokea watalii 45,000 ambapo kati ya hao 26,000 ni watalii wa ndani 19,000 ni wa nje na kuingiza kiasi cha wastani wa shilingi bilioni 1.6 kwa mwaka ambapo idadi ya watalii na mapato yanatarajia kuongezeka katika kipindi cha mwaka 2018/2019.

## PM aagiza mpaka Feb. 15 korosho

INATOKA UK.3

Mtwara wameshalipa zaidi ya asilimia 83, Lindi zaidi ya asilimia 84, Ruvuma zaidi ya asilimia 73 na Pwani asilimia 13.

"Pwani ndio tuna changamoto kubwa kwa sababu korosho nyingi zinazozalishwa ukanda wa kaskazini kwa maana ya Pwani na Tanga ni korosho za daraja la pili kwa zaidi ya asilimia 75," alisema na kuongeza:

"Korosho daraja la pili inatakiwa kuwa asilimia 80 ya bei ya daraja la kwanza, baadhi ya watendaji walijisahau nakiri, badala ya kwenda kulipa kwa kuzingatia sheria na kanuni inavyotaka wakaendelea kusubiri maelekezo yatoke juu ama wizarani au kwa wakubwa wetu zaidi kitu ambacho tumeendelea kuchelewa kulipa wakulima."

Alisema hadi sasa serikali imekusanya zaidi ya tani 212,000 katika maghala kati ya 240,000 zilizokadiriwa kuvunwa msimu huu wa kilimo. Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, alimweleza Waziri Mkuu kuwa uhakiki umekumbwa na changamoto nyingi zikiwamo wakulima kutoa taarifa za uongo.

## Mapya yaibuka kesi kugombea mazishi

INATOKA UK.3

wanne katika kesi hiyo anaeleza katika kiapo chake kilichowasilishwa mahakamani na wakili wake, Mhandisi Joseph Ngiloi kutoka kampuni ya uwakili wa Makoa Attoneys.

Walalamikiwa wengine katika mgogoro huo ni Werandumi Benjamin Ulomi, Awadi Ulomi na Abdulrasul Ulomi.

Kadhalika alidai: "Jubilate ambaye alikuwa ametengana na kanisa lake kwa kuwa na watoto wengi na wanawake tofauti bila kufuata mwongozo wake wa kiroho, aliungana tena katika kanisa lake baada ya toba mbele ya Mchungaji Chambulila wa Kanisa la Msamaria Mwema (Good Samaritan) na akasema kuwa hakuwahi kuwa na ndoa yoyote iliyosajiliwa."

Onesy alidai kuwa baada ya kupitia maombi yaliyopo mahakamani amebaini kuwa maombi yaliyoletwa hayana mashiko yoyote kwa vile hayajaungwa mkono na maombi yoyote ya awali ambayo yanaweza kuongeza ushahidi wa masuala ya msingi ili kuthibitisha amri hizo zitatolewa kabla ya kesi mama itakaposikilizwa.

"Matumizi kama haya ya mahakama katika mfumo tofauti wa kisheria ni kujaribu mlalamikaji kupotosha na kutumia njia ya mahakama kuzuia mazishi ya ndugu yangu na kusababisha zaidi maumivu kwa waombolezaji wa marehemu. Amri zilizotolewa zinapaswa kupuuzwa kwa kuzuia unyanyasaji wa mchakato wa mahakama," alidai mlalamikiwa huyo.

Baada ya kutoa zuio hilo, Mahakama hiyo iliamuru shauri hilo litajwe Februari 7, 2019. Katika hati yake ya kuunga mkono maombi yake, mlalamikaji anasema kwamba alikuwa mke halali na wa kisheria wa Jubilate ambaye wameishi pamoja kama mume na mke kwa miaka 12.

Alisema kuwa walibarikiwa kuwa na watoto wawili na walitengana kwa muda isivyo halali, lakini alibakia kuwa mke wa kisheria wa marehemu hadi tarehe ya kufa kwake. Mlalamikaji ameeleza kuwa baada ya kufariki mume wake, Januari 18, 2019, pande zote mbili zilikutana ili kukubaliana juu ya njia bora za mazishi..

Alisema kuwa Onesy alitoa maelekezo kwa watumishi wa sehemu ya kuhifadhia miili ya marehemu kwamba hakuna mtu anayepaswa kuruhusiwa kuona mwili huo, hali ambayo ilimlazimisha kuandika barua kwa Mkuu wa Wilaya kuomba msaada wake.

HABARI KITAIFA

# Watano kortini tuhuma rushwa

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), mkoani Ruvuma, imewafikisha mahakamani watuhumiwa watano katika matukio matatu tofauti kwa kipindi cha Januari, mwaka huu.

Akitoa taarifa ya utendaji kazi wa taasisi hiyo, Naibu Mkuu wa Takukuru mkoani humo, Owen Jasson, alisema katika tukio la kwanza Shaibu Ngolonje, ambaye ni Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Huria na Charles Yona, mtoa huduma wa Tasaf, walipandishwa kizimbani kwenye Mahakama ya Wilaya hiyo kwa tuhuma za rushwa.

Jasson alifafanua kuwa watuhumiwa hao wamefunguliwa kesi kwa makosa ya kujihusisha na vitendo vya rushwa katika usimamizi wa fedha za Tasaf zilizotolewa kusaidia kaya maskini kwenye kijiji hicho na kesi hiyo ilifunguliwa Januari 14, mwaka huu kwenye Mahakama ya Wilaya ya Tunduru.

Aidha, alisema Januari 22, mwaka huu, Asante Komba, ambaye ni mwalimu wa Shule ya Sekondari Nandembo na Vicent Nkili ambaye ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Kidodoma, walifunguliwa kesi katika Mahakama ya Wilaya ya Tunduru kwa kujihusisha na vitendo vya rushwa wakati wa usimamizi wa mitihani ya kitado cha nne ya mwaka 2018.

Alisema inadaiwa watuhumiwa hao walikuwa wakisimamia mitihani ya kitato cha nne kwenye Shule ya Sekondari ya Mngomba na kutenda vitendo vya makosa chini ya kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2017. Naibu Mkuu wa Takukuru, alisema kuwa Eleterius Chawala, ambaye ni Katibu wa Kamati ya Ulinzi wa Kijiji cha Maweso, wilayani Songea na Juma Mada, ambaye ni Kaimu Ofisa Mtendaji wa kijiji cha Maweso, wilayani Songea, walifikishwa kwenye Mahakama ya Wilaya hiyo na kufunguliwa kesi kwa makosa ya kujihusisha na vitendo vya rushwa.

Alisema watuhumiwa hao wanadaiwa walikuwa wanashughulikia shauri la mwananchi aliyekuwa amepeleka shauri lake kwenye ofisi hiyo.

# Kamuzora ahamasisha biashara za mipakani

**Na Mwandishi Wetu,** KAGERA

KATIBU Tawala wa Mkoa wa Kagera, Prof. Faustin Kamuzora, amewaonya watumishi wa serikali wanaokuwa kikwazo kwa wananchi wanaofanya biashara kwenye maeneo ya mipaka ya mkoa huo na Uganda.

Prof. Kamuzora ambaye aliteuliwa hivi karibuni kushika nafasi hiyo, aliyasema hayo katika ziara yake ya kukagua shughuli za maendeleo kwenye maeneo ya mipaka ya mkoa huo na Uganda ambapo pia aliwataka wananchi wa mipakani kutumia fursa zilizopo kufanya biashara halali na kukuza vipato vyao.

"Mipaka kati ya nchi moja na nyingine ni fursa ya kiuchumi kwa wananchi wanaoishi katika maeneo hayo. Wananchi wanaoishi katika mipaka wanatakiwa kutumia mipaka kufanya biashara na kutajirika kwa kufuata sheria za nchi na jukumu letu Serikali ni kuhakikisha wananchi hawa wananufaika na siyo kuwa kikwazo kwao na mipaka kuonekana si mahala pazuri pa kuishi," alisema Prof. Kamuzora.

**Lazima Serikali iyajue matatizo wanayokumbana nayo wafanyabiashara na kuyafanyia kazi ili wananchi wanufaike na fursa zilizopo katika mazingira yao na serikali iweze kukusanya kodi kwa maendeleo.**

Kiongozi huyo alitembelea mipaka ya Tanzania na Uganda iliyopo mkoani Kagera Wilayani Missenyi (Kabindi-Kashenye, Mtukula na Bugango) pamoja na Murongo wilayani Kyerwa na kukutana na wananchi na watumishi katika mipaka hiyo ili kuona namna bora ya wananchi wanaoishi mipakani kunufaika na mipaka hiyo huku Serikali ikiwawekea mazingira mazuri ya kibiashara.

Ziara hii imefanyika wakati ambapo Mkoa wa Kagera umeweka malengo ya kuufanya mwaka 2019 kuwa mwaka wa kodi kwa wafanyabiashara wote wakubwa na wadogo kuhakikisha wanalipa kodi stahiki na rafiki ambayo itawafanya kuendelea kufanya biashara zao na kunufaika.

"Lazima Serikali iyajue matatizo wanayokumbana nayo wafanyabiashara na kuyafanyia kazi ili wananchi wanufaike na fursa zilizopo katika mazingira yao na serikali iweze kukusanya kodi kwa maendeleo," alisema.

Wavuvi wa Wilaya ya Misenyi walimueleza Prof. Kamuzora kwamba wanakumbwa na ukosefu wa soko la samaki na kulazimika kuuza samaki kwa bei ya hasara ili hali nchi jirani ya Uganda ina soko kubwa na zuri lakini hawaruhusiwi kuuza huko.

Prof. Kamuzora aliwaeleza wavuvi hao kuwa Serikali itaangalia namna bora ya kuona nchi jirani Uganda kama kuna bei nzuri ya samaki wavuvi waruhusiwe kuuza huko kwa kufuata sheria na kulipa ushuru wa Serikali na akavitaka viwanda vya ndani vitoe bei nzuri kwa wavuvi.

Alisisitiza kuwa wananchi wanaokaa mipakani wanatakiwa kunufaika na mipaka hiyo kwa kuwa kwa asili wana muingiliano mkubwa na wenzao wa nchi jirani kijamii na kwa hiyo kiuchumi pia lazima wanufaike.

Akizungumza na watumishi wa idara zote za Serikali zinazotoa huduma katika mpaka wa Mtukula, Prof. Kamuzora aliwaeleza watumishi hao kuwa wanatakiwa kutokuwa kikwazo kwa wananchi wanaojishughulisha na biashara katika mpaka huo bali wawe wabunifu katika kazi zao na kutatua changamoto mbalimbali za kuwasaidia wananchi kutumia fursa ya mpaka kufanya biashara.

"Ukienda nchi nyingine wananchi wa mipakani ndiyo matajiri kwa sababu wamepewa fursa ya kufanya biashara katika pande zote mbili, lakini kwa kuzingatia matakwa ya sheria. Sisi tuwe mwangaza na njia kwao badala ya kuwa vikwazo ili tuinue uchumi wao," Prof. Kamuzora liwaasa watumishi wa Mtukula.



Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera, Prof. Faustin Kamuzora (kushoto), akifafanua jambo kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, jijini Dodoma jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima, wafugaji wapewa neno kupatana

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

WAKULIMA kutoka vijiji vya Panzuo, Bupu na Chamgoi Wilayani Mkuranga mkoani Pwani, wametakiwa kuondoa tofauti zao na wafugaji,ili kuondoa migogoro ya mara kwa mara.

Hayo yalisemwa na Katibu Mkuu wa Chama cha Wafugaji Tanzania. Magembe Makoye, ambaye pia ni mjumbe kamati ya usuluhishi migogoro kati ya wakulima na wafugaji nchini katika mkutano wa hadhara na kuzungumza na wafugaji.

"Kuna kila sababu ya wakulima ndani ya vijiji hivyo kuacha kuwachukia wafugaji, kinachotakiwa ni kushirikiana kuleta maendeleo," alisema.

Aliongeza kuwa uwapo wa wafugaji katika vijiji hivyo, ni moja ya kupata fursa mbalimbali kupitia mifugo hiyo.

"Vijana wa Chamgoi tuanze kujiuliza kwanini wenzetu wafugaji wana pesa mwaka mzima. Basi tuiangalie hiyo kama fursa, mifugo ni pesa, kama una eneo la ekari kadhaa unaweza kulizungushia na kukodisha kama eneo la malisho kwa wafugaji, hiyo ni pesa tayari," alisema Makoye.

Aliwashauri wafugaji kufuata taratibu sahihi za kuingia katika vijiji hivyo ili waishi kwa mfumo sahihi tofauti na sasa wanavyojitenga, hali inayohatarisha maisha yao.

# Mfumo wa kongani wainua wakulima

**Na Mwandishi Wetu**

KITUO cha Kuendeleza Kilimo Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania (SAGCOT) kimesema katika salamu zake za mwaka mpya kwa Watanzania kwamba mafanikio ya taifa katika kuinua kilimo na kupunguza umaskini katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini yametokana na mfumo wa kongani unaotumika katika mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya na Songwe.

Akiwasilisha salamu hizo kwa Watanzania, Afisa Mtendaji Mkuu wa SAGCOT, Geoffrey Kirenga, alisema, taasisi yake mwaka 2010 ilipewa jukumu la kuboresha maisha ya wakulima na kuongeza tija katika kilimo ili kuirudishia mikoa ya nyanda za juu kusini hadhi yake kuzalisha chakula kwa ajili ya taifa na hata kuuza nje.

**Sekta ya kilimo ndio mzalishaji mkuu wa malighafi ambazo zitachagiza uanzishwaji wa viwanda katika maeneo mengi nchini.**

Ili kufikia lengo hilo, Kirenga aliwaeleza waandishi wa habari jijini Dar es Salaam kuwa Sagcot ilibuni ya mfumo wa kongani ambao umesaidia sana kuwakomboa wakulima kwa kuainisha mazao ya kipaumbele na kuyafanyia kazi kwa kuinua tija katika uzalishaji.

"Siri ya mageuzi makubwa yaliyopatikana ni mfumo wa kongani ambao tumeubuni na kuusimamia kwa karibu sana kwa sababu ni mfumo shirikishi. Iwapo utatumika katika maeneo mengine ya nchi kama wanavyohitaji wananchi wengi, sekta ya kilimo nchini itapiga hatua katika uzalishaji," alibaini Kirenga.

Kongani zinazofanyakazi Nyanda za Juu Kusini ni Kongani ya Ihemi (mikoa ya Iringa na Njombe), Kogani ya Mbarali (Mbeya na Songwe) na Kongani ya Kilomberoa ambayo ilizinduliwa mwishoni mwa mwaka jana itahudumia wananchi wa Mkoa wa Morogoro na wilaya zake zote.

Alisema SAGCOT ina nia ya kufungua kongani nyingine ndani ya ukanda wa Nyanda za Juu Kusini ili kunufaisha wananchi katika maeneo ya Ludewa, Rufiji na Sumbawanga na kuikuza sekta ya kilimo ambayo ndiyo kichocheo cha uanzishwaji wa viwanda.

"Sekta ya kilimo ndio mzalishaji mkuu wa malighafi ambazo zitachagiza uanzishwaji wa viwanda katika maeneo mengi nchini. Ni wajibu wa kila mdau katika kilimo kuendelea kutoa mchango utakaosaidia kukuza uzalishaji katika sekta hii," alisisitiza Kirenga.

Kirenga alieleza kuwa katika Kongani ya Ihemi uzalishaji wa nyanya umeongezeka, hivyo Tanzania haiagizi tena nyanya kutoka nje, viwanda viwili vikubwa vya kusindika nyanya vya Dabaga na Darsh Industries vimeanzishwa mkoani Iringa na sasa lipo soko la uhakika la zao la nyanya.

Viwanda hivyo vina uwezo wa kusindika tani mia mbili za nyanya kila siku na kutengeneza bidhaa mbalimbali zinazotokana na nyanya.

Alieleza kuwa SAGCOT ina shauku ya kuona mikoa mingine inaitumia mikoa yenye kongani tayari kama darasa kujifunza namna mfumo huu unavyofanya kazi na kuutumia ili kuchochea ukuaji wa sekta ya kilimo.

"Uhitaji wa elimu kupitia mfumo wa kongani ni mkubwa katika kanda nyingine za nchi yetu, hivyo tutaendelea kutoa elimu kwa kushirikiana na serikali pamoja na sekta binafsi ili kuongeza tija katika kilimo na kuyaboresha maisha ya wananchi," alisema Kirenga.



Msukuma mkokoteni akiwa ameusheheni mzigo wa mbao, katika Barabara ya Mandela, eneo la Buguruni Chama, jijini Dar es Salaam, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JOHN BADI**

## Agizo kutenga eneo viwanda vya dhahabu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MADIWANI wa Halmashauri ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga, wamemtaka Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Anderson Msumba, kutenga eneo kwa ajili ya viwanda vya uchomaji wa kaboni za dhahabu ambavyo vimejengwa katikati ya maeneo ya makazi.

Walitoa maelekezo hayo katika kikao malumu cha baraza la madiwani kilichojadili na kupitisha rasimu ya bajeti ya Halmashauri ya Mji wa kahama kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/ 2020 ambapo jumla ya shilingi bilioni 43.02 zilipitishwa.

Diwani wa Majengo, Bernard Mahongo, alisema viwanda vya uchomaji wa kaboni za dhahabu vimejengwa kwenye makazi na vimekuwa vikitililisha maji yenye sumu, hali ambayo inaweza ikaleta madhara kwa wananchi hapo baadae.

Alisema viwanda hivyo vimejengwa kiholela bila kufuata utaratibu, huku baadhi vimejengwa kwenye maghala ambayo mengine yanatumika katika kuhifadhi chakula.

"Tunafahamu viwanda hivi ni moja ya vyanzo vyetu vya mapato ya ndani, lakini inatakiwa kuangalia kwanza afya za wananchi wetu ambao pia wamekuwa wakichangia pato kwenye Halmashauri. Viwanda vimejengwa kwenye makazi ya watu na vimekuwa vikitililisha maji yenye sumu na kwenda kwenye makazi," lisema Mahongo.

Mkurugenzi Msumba, alisema kati ya viwanda 17 zilivyopo, viwanda 11 ndivyo vinavyofanya kazi na kwamba asilimia kubwa ya viwanda hivyo vimejengwa kwenye maghala.

Hata hivyo alisema Halmashauri imeshatenga eneo kwa ajili ya viwanda hivyo na liko katika kata ya Zongomela na kuongeza kuwa viwanda hivyo vitahamia huko hivi karibuni.

## Wanafunzi sasa wapata ukombozi

**Na Lilian Lugakingira,** MULEBA

Wanafunzi wa shule ya msingi Kabuleme Tarafa ya Izigo wilayani Muleba mkoani Kagera ambao baadhi yao wamekuwa wakisomea chini ya mti wameepukana na adha hiyo, baada ya shirika la kimataifa la World Vision Tanzania, kuwajengea vyumba vitatu vya madarasa.

Wakizungumza wakati wa kukabidhiwa kwa vyumba hivyo na shirika hilo, baadhi ya wanafunzi akiwamo Shadia Mswadiku wa darasa la saba, alisema awali baadhi yao walibanana katika vyumba vya madarasa vilivyo huku wengine wakisomea chini ya miti.

"Walimu wamekuwa wakichukua ubao na kuutundika katika mti na kuanza kutufundisha huku tukiwa tumekalia nyasi, wanafunzi wa darasa la kwanza mpaka la nne ndio walijifunzia chini ya miti, mara nyingi mvua ziliponyesha walimu walituruhusu kurudi nyumbani," alisema.

Dativa Johanes wa darasa la tano, alisema waliteseka sana maana hata waliokuwa wakisomea darasani walibanana mno, na kuwa baadhi yao walikaa katika madawati huku wengine wakijifunza wamesimama na kulazimika kuandikia katika kuta.

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo, mwalimu mkuu wa shule hiyo Godfrey Speratus, alisema shule hiyo iliyojengwa mwaka 1979 inakabiliwa na upungufu wa vyumba 12 vya madarasa.

"Shule hii ina wanafunzi 970 ambao walitumia vyumba tisa vya madarasa kabla hatujakabidhiwa hivi leo na kutimiza vyumba vya madarasa 11, lakini upungufu ni mkubwa, tunahitaji vingine 12, tunaomba tusaidiwe maana kwa sasa chumba kimoja cha darasa kinachukua wanafunzi 168, bado ni wengi," Speratus.

Meneja wa World Vision kanda ya Kagera, Juliana Charles, alisema baada ya kupata changamoto hiyo waliandika andiko la mradi na kupeleka kwa wafadhili, na kufanikiwa kupata shilingi milioni 76.

# Aweso aonya wakandarasi, wahandisi ubabaishaji

**Na Cynthia Mwilolezi,** MONDULI

NAIBU Waziri wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Jumaa Aweso (pichani), amewaonya wahandisi na wataalamu wa sekta ya maji mikoani na wilayani, kuacha ubabaishaji katika kazi na badala yake amewataka kutanguliza mbele weledi na uchapakazi.

Alitoa onyo hilo wakati akifanya majumuisho ya ziara yake katika wilaya ya Monduli na Karatu mwishoni mwa wiki na kusema ameshuhudia ubabaishaji na uongo katika utekelezaji wa miradi ya maji.

Alisema ni vema wataalamu na wahandisi wakashirikiana kurekebishana na kusimamia ili kazi ziende kama zinavyotakiwa ili wasijikute kwenye matatizo makubwa.

"Lazima mkubali kubadilika na kuacha ubabaishaji pamoja na kuchekeana sababu nitakayemkuta na shida sitasita kumfukuza kazi na kuajiri vijana ambao wapo wengi wasio na kazi," alisema.

Akitoa mfano alisema alipoanza ziara yake wilayani Monduli, Januari 25, mwaka huu, alijionea kazi mbovu zilizofanywa na mkandarasi wa Kampuni ya Meero Construction Ltd,



Ayo Jeremiah, kwenye mradi wa maji wa Kijiji cha Lendikinya, Kata ya Sepeko.

"Huyu ameweka bomba za plastiki kwenye makorongo badala ya bomba za chuma kama mkataba unavyosema, lakini Mhandisi wa Maji Wilaya ya Monduli, Charles Saidea, anaona uhuni huo wakati yeye ndiye msimamizi wa serikali, wala hakatai anachekelea huu uhuni, sitakubali tena, nikija kila mmoja ajitathimini," alisema.

Alisema kutokana na hilo aliamua kuwalaza ndani toka Januari 25 hadi 26, mwaka huu, mkandarasi na mhandisi huyo ili wapate somo na kuwaonya wasirudie kufanya kosa kama hilo.

Alisema wao waliandika andiko kuomba mradi huo uongezewe fedha kutoka Sh. milioni 700 hadi kufikia Shilingi bilioni moja, ili waweze kuweka bomba za chuma kwenye makorongo ambayo ni mengi kijijini humo, lakini wakafanya kinyume na mkataba.

Katika Wilaya ya Karatu, alisema nako kuna uhuni umefanywa kwenye mradi wa vijiji 10 na zaidi ya Shilingi bilioni tati zimetumika, lakini bomba zimewekwa chini ya kiwango zimepasuka na wananchi hawapati maji.

Alisema kutokana na uzembe unaofanywa na wataalamu hao ameahidi kurudi mara moja baada ya Bunge kuisha muda wake ili aje kuchukua hatua stahili kwa wahusika.

# Madiwani wawajia juu wataalamu wa H'shauri

**Na Allan Isack,** ARRUMERU

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Arusha Vijijini, wamewajia juu wataalamu wa halmashauri, wakiwataka kukamilisha mradi wa maji wa Likamba ili kuwanusuru maisha ya wakazi wanaokabiliwa na ukosefu wa maji kwa kipindi kirefu.

**Serikali imewataka wananchi wanapoanzisha miradi ya maendeleo wahakikishe wanaikamilisha na siyo kuiachia njiani.**

Akizungumza katika baraza hilo mwishoni mwa wiki baada ya kupitisha rasimu ya mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/20, Diwani wa Kata ya Mwandeti, Boniface Tarakwa, alisema kucheleshwa kukamilika kwa mradi wa maji wa Likamba, kumeongeza changamoto kubwa inayowakabili wananchi kwa kukosa huduma ya maji kwa kipindi kirefu.

Alisema wananchi waeneo hilo, wamekuwa wakiteseka kwa kukosa huduma hiyo, hivyo ni jukumu la halmashauri kwa kushirikiana na wataalamu wake kukamilisha mradi huo kwa wakati.

Mradi huo ukikamilika utawahudumia wakazi wa vijiji na kata zake ambazo ni kata za Musa, Olorieni, Matevezi, Olmotonyi, Mwandeti pamoja na vijiji vya Likamba na Nangungu. Akitoa ufafanuzi kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Dk. Wilson Mahera, Ofisa Mipango wa halmashauri hiyo, Anastazia Tutuba, alisema serikali haiwaungi tena mkono wananchi wanapoianzisha miradi na kuiachia njiani bila ya kuikamilisha.

Aidha, alisema serikali imewataka wananchi wanapoanzisha miradi ya maendeleo wahakikishe wanaikamilisha na siyo kuiachia njiani.

Hata hiyo, alieleza serikali haiwezi kutekeleza miradi yote kwa wakati, kutokana na kuwa na majukumu mengi ya kiutendaji ikilinganishwa na kiasi ya fedha cha Sh bilioni 50.8, kilichotengwa katika bajeti ya mwaka 2019/20, kutotoshelezi kutekeleza mahitaji yote.

"Serikali ina miradi mingi sana ukilinganisha na makadirio yetu ya bajeti ya mwaka wa fedha 2019/20, ya Sh.bilioni 50.8, ni vigumu sana kutekeleza miradi yote kwa wakati," alisema.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti (kushoto), akiwasili Mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, kuhudhuria kikao cha wadau wa madini juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wana apolo waruhusiwa kuingia bure

**Na Mwandishi Wetu,** MIRERANI

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, ameagiza wachimbaji wadogo wa madini ya Tanzanite (wana apolo) wapite bure kwenye lango la kuingia ndani ya ukuta unaozunguka migodi ya madini hayo hadi hapo utaratibu wa kulipia Sh. 70,000 ili wapatiwe vitambulisho vya kupita utakapofanyika.

Alitoa agizo hilo wakati akizungumza na wadau wa madini mwishoni mwa wiki.

Uamuzi huo ulipokelewa kwa shangwe na wananchi wa mji mdogo wa Mirerani kwa kuwa awali waliokuwa wanaruhusiwa ni wale wenye mkataba wa kulipwa mshahara pekee.

Alisema wamekubaliana kwenye kikao cha wamiliki wa migodi na wana apolo kuwa suala la malipo ya mishahara au asilimia 10 pindi madini yakitoka wataamua wao wenyewe.

"Baada ya serikali kukubaliana na pendekezo lenu la kuachana na suala la mishahara ambalo lipo kisheria inabidi ikusanye kodi ya mshahara na tozo ya uendelezaji ufundi stadi," alisema.

Mbunge wa Jimbo la Simanjiro, James ole Millya, alisema uamuzi huo utawanufaisha watu wengi.

Aliwataka wamiliki wa migodi na wachimbaji wote kutimiza wajibu wao huku wakitilia mkazo suala la ulipaji wa kodi kwa ajili ya maendeleo.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa chama cha wachimbaji madini Mkoa wa Manyara, (Marema), Justin Nyari, alisema, tamko hilo limeweka historia kwa kuwa baadhi ya wachimbaji waliondoka sasa watarudi.

Katibu wa Marema tawi la Mirerani, Omary Mandari, alisema, wanampongeza Rais John Magufuli kwa kujenga ukuta huo na Mkuu wa Mkoa kwa uamuzi wake wa kuruhusu watu kupita.

Makamu Mwenyekiti wa Usalama, Afya na Mazingira wa Shirikisho la Wachimbaji madini nchini, (Femata), Dk. Bernard Joseph, alisema wamejipanga kuhakikisha utunzaji mazingira na afya za wafanyakazi.

# Mwanafunzi aliyeajiriwa 'u-house girl' aokolewa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KAMATI ya ulinzi wa wanawake na watoto ya Kijiji cha Mikocheni, Kata ya Arusha Chini iliyopo Moshi Vijijini, imemwokoa mwanafunzi wa darasa la sita aliyeachishwa masomo kwa lazima na jirani yao na kuajiriwa kama 'house girl.'

Mwanafunzi huyo wa Shule ya Msingi Mikocheni ambaye alikatisha masomo tangu mwaka jana kwa ajili ya kufanya kazi za ndani na kufanyishwa biashara ya kuuza genge, tayari amerejeshwa shuleni mwanzoni mwa mwaka huu kutimiza ndoto yake ya kupata elimu.

Akitoa mrejesho wa utekelezaji wa kamati zilizoundwa na Shirika la Tusonge kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto (Mtakuwwa), Mjumbe wa kamati hiyo Evarest Komba, alisema wamefanikiwa kumuondoa katika ajira ya watoto mwanafunzi huyo, baada ya mwanamke aliyemwajiri kubanwa.

**Kwa mantiki hiyo, sisi kama wanakamati baada ya kujengewa uwezo na kupewa miongozo, tulimfuata huyo mwanafunzi na kumrudisha shule na sasa anaendelea darasa la saba mwaka huu na mwajiri tumempa elimu kuhusu Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009.**

"Watoto wanaathiriwa na udhalilishaji ama unyayashaji unaoweza kuwa wa kiuchumi, ubaguzi wa kijinsia, elimu au huduma za afya. Kwa mantiki hiyo, sisi kama wanakamati baada ya kujengewa uwezo na kupewa miongozo, tulimfuata huyo mwanafunzi na kumrudisha shule na sasa anaendelea darasa la saba mwaka huu na mwajiri tumempa elimu kuhusu Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009,"alisema Komba.

Pia, kamati hiyo imefanikiwa kumwokoa mwanafunzi mwingine aliyechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka huu katika Shule ya Sekondari Mangoto, ambaye shangazi yake (jina limehifadhiwa), alikataa asiendelee na elimu ya sekondari, akidai ukoo wao ni masikini na hauna fedha za kumwendeleza mke wa mtu.

Akiwa katika kikao hicho, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Mwanzo, Arusha Chini, Annarose Hayata alisema kuna adhabu kwa mtu atakayeajiri watoto kinyume cha Sheria ya Ajira na Mahusiano ya Kazi ya Mwaka 2004, kwa kuwa ni kosa kuajiri watoto kinyume na sheria inavyotamka.

Kwa mujibu wa Hakimu huyo, adhabu yake hutolewa chini ya Kifungu cha 102 (2) ambacho kinampa mamlaka ya kutoa adhabu sawa na faini isiyozidi Shilingi milioni tano au kifungo cha mwaka mmoja au adhabu zote kwa pamoja kama mahakama itavyoona inafaa, kutegemea na mazingira ya kesi yenyewe.

Akizungumzia kamati hizo za ulinzi wa wanawake na watoto katika Kata ya Arusha Chini, Mratibu wa mradi wa kupinga ukatili wa kijinsia na ukeketaji dhidi ya wanawake na watoto wa Shirika la Tusonge, Joyce Kessy, alisema kuripotiwa kwa matukio hayo na kutafutiwa ufumbuzi baadhi ya changamoto, kunatokana na kukamilika kwa zoezi la kuundwa na kujengewa uwezo wanakamati hao.

Mradi wa kupinga ukatili wa kijinsia na ukeketaji dhidi ya wanawake na watoto katika Kata ya Arusha Chini katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, unatekelezwa na Shirika la Tusonge kwa ufadhili wa Foundation For Civil Society.



Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini (CCM), AbdulAziz Abood (wa pili kushoto), akisaidiana na wananchi wa Kata ya Sultani, kuchimba msingi wa ujenzi wa zahanati ya kata hiyo, katika Manispaa ya Morogoro jana. Mbunge huyo alichangia Sh. milioni 5, pamoja na mifuko ya saruji na mchanga. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# Vijana wenye ulemavu wasuasua kuchukua mikopo

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

IDADI ndogo ya vijana na wenye ulemavu wanaojitokeza kuchukua mikopo ya uwezeshaji kiuchumi makundi maalumu, inaitesa Manispaa ya Moshi.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii, Rose Minja, alimweleza hayo juzi Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kippi Warioba, wakati wa kukabidhi mikopo yenye thamani ya Sh. milioni 200 kwa vikundi 40.

"Mpaka sasa vikundi ambavyo tumevipatia mikopo vinarejesha kwa asilimia kubwa, tofauti na kipindi cha nyuma ambacho urejeshaji ulikuwa una suasua. Mheshimiwa DC, pamoja na uhamasishaji tunaofanya katika wilaya yako, bado kuna idadi ndogo ya vijana na walemavu wanaojitokeza kwa ajili ya kuomba mikopo hii," alisema

Mikopo hiyo hutolewa kutokana na makusanyo ya fedha za ndani, na kwa mabadiliko ya sasa, kila halmashauri hutenga asilimia nne kwenda kwa vijana, asilimia nne nyingine kwa wanawake na asilimia mbili kwa wenye ulemavu.

Kutolewa kwa mikopo hiyo kunaifanya Manispaa ya Moshi, iwe imetoa mikopo ya jumla ya Sh. milioni 534 kwa vikundi 104 katika miezi 24.

Akikabidhi mikopo hiyo, Mkuu wa Wilaya hiyo, Warioba aliwataka wajasiriamali waliokopeshwa fedha hizo, kurejesha kulingana na taratibu walizowekewa ili kuweza kuitumia fursa hiyo kukopa kwa awamu nyingine na kuleta mabadiliko ya kiuchumi kwao.

Muda mfupi baada ya kumalizika kwa zoezi hilo, Meya wa Manispaa hiyo, Raymond Mboya aliagiza utoaji wa mikopo hiyo ufuate vigezo vilivyowekwa na kuwaomba watendaji kutoingiza siasa.

Dafrosa Kimaro, ambaye ni mjasiriamali kutoka kikundi cha Kirashi kilichopo Kata ya Longuo B, Manispaa ya Moshi, aliishukuru serikali kwa kuwajali na kuwapatia mikopo ambayo haina riba na inayolenga kuwainua kiuchumi na kuondokana na utegemezi.

# Majosho mawili pekee yafanyakazi Mwanga kati ya 16

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KATI ya majosho 16 ya kuogeshea mifugo yaliyojengwa kwa gharama kubwa na serikali katika Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga, mkoani Kilimanjaro, mawili pekee ndiyo yenye uwezo wa kufanya kazi hiyo kwa sasa.

Uchunguzi uliofanywa na Nipashe katika sekta hiyo na baadaye kuthibitishwa na Ofisa Mifugo na Uvuvi wa Wilaya ya Mwanga, Emmanuel Sindiyo, unaonyesha kuwa majosho hayo hayawezi kukidhi mahitaji ya wafugaji.

Kuogesha mifugo kwenye majosho ya umma yaliyojengwa mahususi kwa ajili ya uogeshaji huo, kuna faida kubwa kwa wafugaji walio wengi kuogesha ng'ombe au mifugo yao kila mara bila gharama kubwa ambazo zingehitajika kwa ununuzi wa dawa na bomba au pampu ya kuogeshea.

Sindiyo ameeleza: "Ni kweli halmashauri ina jumla ya majosho 16 na majosho ambayo ni mazima ni mawili tu. Hata hivyo, kwa mwaka mpya wa fedha 2019/2020, halmashauri itatenga bajeti kwa ajili ya kuboresha majosho, ingawa kwa sasa siwezi kusema ni kiasi gani.

"Zoezi hili la kuogesha mifugo ni endelevu na la lazima. Kila mwananchi ambaye ni mfugaji ahakikishe kuwa anapeleka mifugo ili iogeshwe, hii ni kwa mujibu wa Sheria ya Mifugo ya Mwaka 203."

Changamoto kuhusu uhai wa majosho hayo inajitokeza, huku zoezi la lazima la kuogesha mifugo likiwa limezinduliwa na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Ezekiel Mwasumbi, katika Kata ya Kileo. Jumla ya ng'ombe 577 walipatiwa huduma hiyo ya kuogeshwa.

Aidha, wakati kukiwa na upungufu huo wa majosho yanayofanya kazi, tayari Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga imetangaza kuwa gharama za kuogesha ng'ombe mmoja katika majosho yake itakuwa Sh. 600 na Sh. 100 kwa mbuzi mmoja.

Pamoja na changamoto hiyo, idara ya mifugo ya wilaya hiyo imeeleza kwamba baadhi ya wafugaji pia hukwepa moja kwa moja gharama za uogeshaji na kubaki kujiandaa vyema kwa ajili ya kutibu mifugo yao, mara tu wanapoona dalili za maradhi kwa mifugo yao.

Hata hivyo, kwa mujibu wa wataalamu wa mifugo, utaratibu huo si mzuri kwa kuwa mara nyingine huweza kusababisha kutokea kwa vifo vya wanyama kwa wingi na kwa ghafla kutokana na gharama za dawa na hata malipo kwa wataalamu wa mifugo watakaotumika kutibu mifugo hiyo.

Nipashe
# Spotika
NIPASHE JUMATATU JANUARI 28, 2019



TIMU 5 HATARI ZIKICHEZA NYUMBANI UK.15

## TOBO...





Kiungo wa Manchester City, Kevin De Bruyne, akimpiga tobo beki wa Burnley, Stephen Ward, kwenye mechi ya Kombe la FA iliyopigwa Uwanja wa Etihad juzi na City kushinda 5-0. **PICHA: MTANDAO**

### ISIKUPITE

KATI ya penalti 10 zilizopita Ligi Kuu England ambazo zilipigwa kwa kutumia mguu wa kushoto, sita zilishindwa kuzamishwa nyavuni- na zingine nne zilizojaa kimyani zote zilifungwa na mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah.

# ARSENAL INAMHITAJI RAMSEY KULIKO OZIL



**LONDON,** England

KUNA vitu vingi kwa sasa vinatokea katika klabu ya Arsenal, vitu ambavyo mwisho wa siku vinabakiza maswali mengi kwa mashabiki wake.

Arsenal kwa sasa wako katika kipindi cha mpito, kipindi ambacho kinahusisha mabadiliko mengi ndani ya timu.

Baada ya miaka 22 ya utawala wa kocha Arsene Wenger, ililazimika muda umpe nafasi Unai Emery avae viatu vya mzee huyo raia wa Ufaransa.

Mzee ambaye amefanya vingi vikubwa ndani ya Arsenal. Hawezi kudharaulika kirahisi kutokana na mwisho wake pale Arsenal.

Sawa mwisho wake ulikuwa mbaya pale Arsenal ukilinganisha na kipindi cha nyuma ambacho alikuwa anahudumu katika timu hii. Kwenye kipindi chake alifanya vingi, aliwapa nafasi vijana, akawaamini na kwa kiasi kikubwa hawakumwangusha.

Kuna wakati alikuwa anasimama kama baba mzazi kwa baadhi ya wachezaji ambao alikuwa anawaamini zaidi. Wakati ambao mashabiki wanarusha makombora kwa mchezaji fulani, Wenger alisimama kama mlinzi.

Alihakikisha mchezaji husika asiathirike na kitu chochote kibaya, alitaka mchezaji husika afikirie kuhusu kucheza mpira tu. Moja ya wachezaji ambao walikuwa kipenzi kikubwa cha Wenger hasa hasa kwenye siku zake za mwisho za utawala wake walikuwa ni Mesut Ozil na Aaron Ramsey.

Hawa aliwalea kama mayai, aliwatetea na kuwaamini. Alikuwa anaamini kupitia miguu yao. Kuna wakati walikuwa wanafanya vibaya uwanjani, lakini yeye alisimama kifua mbele kuwakinga na kila mashambulizi yaliyokuwa yanakuja kwao.

Aliwapa nafasi kila muda, na aliwapa majukumu makubwa ndani ya uwanja. Kuna wakati Ramsey akikuwa anaandaliwa kuwa nahodha. Huyu ndiye alikuwa Wenger, kocha ambaye alikuwa na malezi ya babu kwa wachezaji wake. Malezi ambayo wachezaji walikosa hamasa ya kushinda.

Wachezaji wengi walibweteka ndani ya mikono ya Wenger. Hakukuwapo na ile hamasa ya mchezaji kupigana, hata alipokosea hakukemewa. Nyakati kwa sasa zimebadilika, Wenger hayupo tena, Emery ndiye kiongozi wa jahazi la Arsenal.

Kiongozi ambaye anaonekana hana masihara hata kidogo, kwake yeye ukicheza vibaya ni jambo la kawaida kukurudisha benchi. Tangu amekuja wachezaji hawa wawili (Ozil na Ramsey) wamekuwa na wakati mgumu zaidi chini ya Emery.

Hajawapa nafasi kubwa, na ni kitu cha kawaida kwake yeye kuwaweka benchi. Haogopi wala kuhofia kitu chochote. Ndiyo maana unamuona hakuwa hata na haraka ya kumshawishi Ramsey kusaini mkataba mpya, haogopi kuondoka kwake.

Hana hofu yoyote kuhusu kumweka benchi Ozil. Utaanzaje kumweka benchi mchezaji anayelipwa zaidi kuliko wachezaji wote kwenye ligi ya juu England? Kwake yeye ni jambo la kawaida. Tena sana, Ozil anakaa benchi, Ramsey anakaa benchi pia.

Lakini wote kwa pamoja wanatuachia swali moja tu, nani anastahili kuendelea kuwapo Arsenal?

Licha ya kwamba Ramsey tayari amefikia makubaliano ya kwenda Juventus wakati wa kipindi kijacho cha majira ya joto, lakini ukweli ni kwamba yeye ndiye alikuwa mtu sahihi kubaki kwenye kikosi cha Emery. Kwa nini? Emery hutaka timu yake icheze kwa kukabia juu, na inapopoteza mpira kila mchezaji afanye mgandamizo wa kupata mpira.

Kufanikisha hili lazima uwe na mchezaji ambaye ana kasi, na mwenye uwezo wa kukimbia umbali mrefu ndani ya uwanja. Ramsey ana uwezo mkubwa wa kukabia juu pia na kufanya mgandamizo kwa timu pinzani kipindi timu yake imepoteza mpira.

Hachoki, ana nguvu ya kukimbia umbali mrefu ndani ya uwanja. Kitu ambacho hakipo kabisa kwa Ozil. Ni wazi, Ozil ni mzuri zaidi akiwa na mpira kwa kutengeneza nafasi, tofauti na Ramsey ambaye ana faida kubwa akiwa na mpira na akiwa hana mpira.

Pia Ramsey ana uwezo wa kuunganisha safu ya ushambuliaji na safu ya kiungo. Kwa kuwa na uwezo wa kutokea katikati kwenda mbele. Hata timu ikiwa chini, Ramsey ana uwezo mkubwa wa kukimbia kutoka juu kwenda chini na kutoka chini kwenda juu.

Hii ni tofauti kabisa na kwa Ozil. Kwa hiyo Ramsey ana manufaa makubwa kwenye mfumo wa Unai kuzidi Ozil. Lakini mwisho wa siku mwenye maamuzi ni kocha mwenyewe, na tayari inaonekana wazi kwamba msimu ujao Arsenal haitakuwa na Ramsey, na bado haijulikani hatima ya Ozil.

**JE, WAJUA?**

ARSENAL imevuna pointi nyingi katika mechi saba dhidi ya timu sita kubwa ('big six') msimu huu(pointi nane) kuliko ilizovuna msimu mzima wa 2017-18 uliopita (pointi sita).



# MICHEZO

## NJE YA UWANJA



## DILI OZIL, PERISIC KUPISHANA LAFA

**LONDON,** England

KLABU ya Inter Milan imekataa ofa ya Arsenal ya kubadilishana wachezaji, Mjerumani Mesut Ozil na kiungo Mcroatia Ivan Perisic.

'The Gunners' wamepiga hatua katika mazungumzo ya kumnasa nyota huyo wa kimataifa wa Croatia katika dirisha hili dogo.

Arsenal ilitoa ofa kiasi cha euro milioni 40, ama kumjumuisha Ozil kama sehemu ya kubadilishana, ilieleza Sky Italia.

Hata hivyo, Inter ipo tayari kukubali fedha taslimu pekee kumwachia Mcroatia huyo.

"Kila mmoja anamthaminisha Perisic kama tunavyomthaminisha sisi. Kama kuna anayevutiwa naye, masharti ni kulipa thamani yake, kwa sababu ni mchezaji imara," kocha wa Inter, Luciano Spalletti alisema juzi.

"Kama kuna mtu anataka kumsajili, lazima watengeneze mazingira ya kulipa kwa ajili yake, kwa sababu huyu ni mchezaji imara sana."



Straika wa Yanga, Ibrahim Ajibu akijaribu kuwalamba chenga wachezaji wa JKT Tanzania kwenye moja ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara katika Uwanja wa Taifa ambayo walishinda kwa mabao 3-0.

# TIMU TANO HATARI ZIKICHEZA NYUMBANI

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara ikifikisha raundi ya 23 kwa baadhi ya timu, zipo timu kadhaa zimeonekana kuwa ni hatari zaidi zikicheza kwenye uwanja wao wa nyumbani.

Kwa maana hiyo timu zingine zinazokwenda kucheza na timu hizo inabidi ziende kwa tahadhari kubwa, vinginevyo zitakula za uso...

**1. Yanga**

Timu ya Yanga ndiyo inayoongoza kwa kushinda idadi ya mechi nyingi ikiwa kwenye uwanja wake wa nyumbani, wa Taifa inaoutumia.

Imeshinda mechi 11 kwenye uwanja huo kati ya hizo, 12 ilizocheza kama uwanja wa nyumbani, ikiwa ni idadi kubwa zaidi kwani hakuna timu yoyote ile kwenye Ligi Kuu mpaka sasa iliyoweza kufikisha ushindi kama huo ikicheza nyumbani.

Ilizichapa timu za Mtibwa na Biashara mabao 2-1 kila moja, Coastal Union na Lipuli zenyewe zilipokea kipigo cha bao 1-0 kila moja, huku Singida United na Mbao FC zikipigwa mabao 2-0 kila moja.

Stand United ilishindiliwa mabao 4-3 kwenye Uwanja wa Taifa, Alliance FC na JKT Ruvu zilibamizwa mabao 3-0 kila moja, Mwadui ikachapwa mabao 3-1 na Ruvu Shooting ikafungwa mabao 3-2.

**2. Azam FC**

'Wanalambalamba', Azam FC nao wameonyesha kuwa timu yoyote itakayokanyaga kwenye uwanja wa Azam Complex inakula za uso.

Katika mechi 11 ilizocheza kwenye uwanja huo, Azam imeshinda 10 na kukamata nafasi ya pili kwa timu inayotumia vema uwanja wa nyumbani mpaka sasa.

Timu zilizokanyaga Chamazi na kukipata cha mtema kuni ni Mbeya City iliyochapa mabao 2-0, Coastal Union nayo ikichapwa idadi kama hiyo ya mabao.

Timu za Mwadui FC na Prisons kila moja ilichapwa bao 1-0, huku African Lyon, Ruvu Shooting na Biashara FC kila moja akitembezewa kichapo cha mabao 2-1.

Ndanda ilikutana na kisago cha mabao 3-0, Stand ikatandikwa mabao 3-1 na Mbao FC ikachakazwa mabao 4-0.

**3. KMC**

Timu hii inayomilikiwa na Manispaa ya Kinondoni imeonekana kushangaza wengi, kwani pamoja na kupanda Ligi Kuu msimu huu imekuwa ikifanya vema na inashika nafasi ya tatu mpaka sasa kwenye msimamo ikiwa na pointi 34, lakini pia inashika namba tatu kwa timu zinazotumia vema uwanja wa nyumbani.

Kwa michezo 12 iliyocheza imeshinda mara nane ikicheza uwanja wa nyumbani. KMC inautumia Uwanja wa Uhuru kama uwanja wake wa nyumbani.

Ushindi wake na kuzichapa timu za Ruvu Shooting, JKT Ruvu na Mbeya City bao 1-0 kila moja, African Lyon na Stand United kila moja ilichapwa mabao 2-0, Coastal Union ilifungwa 5-2, Ndanda ikabamizwa mabao 5-1 na Singida United ikachapwa 3-0.

**4. Simba**

Mabingwa watetezi Simba wanashika nafasi ya nne kwa timu zinazotumia vema uwanja wa nyumbani. Imecheza mechi tisa ikiwa Uwanja wa Taifa ambao ndiyo wa nyumbani na imeshinda saba mpaka sasa.

Simba ilizitandika timu za Prisons bao 1-0, Mbeya City mabao 2-0, African Lyon na KMC mabao 2-1 kila moja, Stand United na Singida United mabao 3-0 kila moja, na Alliance mabao 5-1.

**5. Mtibwa Sugar**

Kwenye tano bora ya timu zinazotumia vema uwanja wa nyumbani, Mtibwa Sugar inafunga dimba kwa kuwa kwenye nafasi ya mwisho.

Inashika namba tano. Mtibwa Sugar imekuwa ikiutumia vema Uwanja wa Manungu Complex ulioko Turiani mkoani Morogoro. Katika mechi tisa ilizocheza imeshinda mechi saba kama Simba.

Mechi zake za ushindi Manungu ni kuichapa Mbao FC, Mwadui FC na Kagera Sugar bao 1-0 kila moja. Ikaibamiza Mbeya City na Biashara mabao 2-1 kila moja, Ruvu Shooting yenyewe ikifungwa mabao 4-0 na Azam FC ilikumbana na kipigo cha mabao 2-0.

# Safu 5-Bora za watatu zinazokimbiza zaidi EPL

**LONDON,** England

LIGI Kuu England (EPL), tayari imefikia nusu ya msimu na mambo yanaonekana kwenda sawa. Kwenye kilele cha msimamo, Liverpool imeendelea kujikita kileleni mwa msimamo huo ingawa Manchester City ipo jirani na visigino vyake.

Pointi saba pekee zinazitenganisha timu nne zikiwa kwenye mashindano ya kumaliza katika nne-bora ili ziweze kupata nafasi ya kufuzu kucheza michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Katika mafanikio ya timu hizo msimu huu, safu zao za ushambuliaji zimekuwa nguzo muhimu zaidi. Katika mechi 230 zilizochezwa hadi sasa, mabao 651 yamefungwa, sawa na wastani wa mabao 2.83 kwa mchezo.

Hapa tunazichambua safu za ushambuliaji za timu tano zinazofanya vizuri zaidi kwenye Ligi Kuu msimu huu. Hawa ni wachezaji ambao miongoni mwao ndio vinara wa ufungaji kwa klabu zao na wamekuwa chanzo cha mabao kwa timu zao msimu huu.

Kwa heshima ya kuwataja, wakiwa na jumla ya mabao 22 kwa pamoja, safu ya ushambuliaji ya Chelsea inayoundwa na Eden Hazard, Pedro na Alvaro Morata haipo kwenye orodha hii, twende sasa...

**5. Pogba - Martial - Rashford (Man United): Mabao 24**

Ukweli ni kwamba safu ya ushambuliaji ya Manchester United imeipiku ile ya Chelsea na wameonyesha kuimarika zaidi baada ya ujio wa Ole Gunnar Solskjaer. United imeimarika kama timu, na wameshinda mechi nane kwenye mashindano yote hadi sasa chini ya kocha huyo wa muda.

'Mashetani Wekundu' hao safu yao ya ushambuliaji inaongozwa na wachezaji watatu, Paul Pogba, Anthony Martial, Marcus Rashford chini ya Solskjaer, wakati Lukaku amekuwa akitokea benchi. Pogba amekuwa ndiye akiilisha safu ya ushambuliaji akitokea kwenye kiungo na kuisaidia kwa kiasi kikubwa United kuwa kwenye kiwango kizuri cha kufunga mabao.

Wote watatu wamefunga mabao 24, kila mmoja akitupia mara nane kwenye Ligi Kuu, na huku Pogba na Rashford wakifanya hivyo katika mechi 20, Martial amefikia idadi hiyo kwa mechi 18.

Pia Romelu Lukaku amefunga mabao nane kwenye Ligi Kuu, ingawa hajahusishwa kwa kiwango kikubwa kwenye mechi za hivi karibuni. Ukweli ni kwamba tayari United ina wachezaji zaidi ya wanne wenye mabao nane na hii inatoa ishara kwamba United wanaweza kuwa bora zaidi msimu huu.

Kuwa na jumla ya mabao 24 kwa washambuliaji hawa watatu Pogba, Rashford na Martial wanajikuta wakishika nafasi ya tano, lakini kuna mengi zaidi yanaweza kuja kutoka kwenye safu hiyo hadi mwishoni mwa msimu huu.

**4. Lacazette - Aubameyang - Mkhitaryan (Arsenal): Mabao 26**

Arsenal imekuwa na safu imara ya ufungaji wa mabao huku ikiongozwa na mshambuliaji wake anayevaa jezi namba 14, ambaye sasa ameanza kuwakumbusha mashabiki wake kuwa anafuata nyayo za gwiji aliyekuwa akivaa jezi hiyo, Thierry Henry.

Pierre-Emerick Aubameyang amekuwa kwenye kiwango bora kabisa kwa Arsenal msimu huu, na tarari amefunga mabao 14 kutoka katika mechi 23 alizocheza. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Gabon kwa sasa anashindana na Mohamed Salah kwenye mbio za kuwania Kiatu cha Dhahabu na inatarajiwa kwamba ataendelea kumkimbiza mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri hadi mwisho wa msimu huu.

Alexandre Lacazette naye amekuwa akitoa sapoti kubwa kwa mchezaji mwenzake huyo, akiwa ametikisa nyavu mara nane katika mechi 22 za Ligi Kuu msimu huu. Kiwango cha Mfaransa huyo kwenye kufunga mabao kimeimarika zaidi, na amefunga mabao mawili katika mechi tatu zilizopita za Ligi Kuu na amekuwa akifiti vizuri kwenye mfumo wa kocha Emery.

Maisha ya Henrikh Mkhitaryan hapo Arsenal bado hayajafikia katika kiwango ambaco kilitarajiwa, lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa Armenia amefunga mabao manne kwenye mechi 14 alizocheza kabla ya kukumbwa na majeraha Desemba mwaka jana. Anatarajiwa kwamba atakuwa nje ya dimba kwa kipindi cha miezi miwili, kitu ambacho ni pigo kubwa kwa 'Washika Bunduki' hao.

Wakiwa na jumla ya mabao 26, safu hii ya ushambuliaji ya Arsenal inashika nafasi ya nne.

**3. Son - Kane - Moura (Tottenham): Mabao 28**

Hakuna mshangao kwamba timu ambayo mbele yupo Harry Kane itakuwa na safu hatari zaidi ya ushambuliaji kwenye Ligi Kuu, hata hivyo, Heung-min Son ameibuka katikati yake na kuwa nyota hapo Tottenham.

Mchezaji huyo raia wa Korea Kusini amefunga mabao nane katika mechi 17 alizocheza kwenye Ligi Kuu hadi sasa. Muunganiko wake na Kane umekuwa wa kuvutia zaidi kwa Spurs msimu huu.

Ukimuacha yeye, Lucas Moura pia amekuwa na mchango mkubwa wa kufumania nyavu kwa klabu yake. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil, amefunga mabao sita katika mechi 19 alizocheza msimu huu, lakini kwa sasa anauguza jeraha la goti, kitu kilichomfanya kukosa mechi tano hadi sasa.

Ingawa wote Son na Moura wamekuwa wazuri zaidi mbele ya goli, ni vigumu kumuacha Kane hapo Tottenham. Muingereza huyu amefunga mabao 14 katika mechi 22 alizocheza hadi sasa huku pia akiwa kwenye mbio za kuwania Kiatu cha Dahabu. Hata hivyo, kwa sasa Kane yupo nje ya dimba kutokana na majeraha aliyopata katika mchezo dhidi ya United.

Ingawa wote hao watatu wanaweza kutokuwa dimbani kwa sasa, bado wanatengeneza safu bora zaidi ya ushambuliaji kwenye Ligi Kuu msimu huu.

**2. Aguero - Sane - Sterling (Man City): Mabao 28**

Manchester City imendelea kuwa kwenye kiwango cha juu msimu huu, ikiwa tayari imefunga mabao 62 katika mechi 23 kwenye Ligi Kuu hadi sasa.

Wakati wachezaji wengi wamefunga mabao kama kawaida yao. Wachezaji saba wamefunga mabao matano msimu huu kwenye Ligi Kuu, lakini nyota wao Sergio Aguero, Leroy Sane na Raheem Sterling wamekuwa bora zaidi hadi sasa.

Aguero amefunga mabao 10 kutoka katika mechi 19 kwenye Ligi Kuu. Alikuwa nje kwa mechi tatu kutokana na maumivu ya nyonga, lakini tangu amerudi dimbani ameweza kufunga mabao mawili katika mechi sita.

Sane amefunga mabao nane katika mechi 21 na Januari pekee amefunga mabao mawili katika mechi tatu. Na pia ametoa pasi za mwisho 10 na kumfanya kuwa mmoja wa wachezaji muhimu zaidi kwenye kikosi hicho.

Sterling amefunga mabao 10 na kutoa pasi za mwisho nane katika mechi 20 hadi sasa kwenye Ligi Kuu na ni moja ya silaha muhimu zaidi ya Guardiola.

Watatu hao kwa pamoja wamefunga jumla ya mabao 28 na kushika nafasi ya pili kwa kuwa safu bora ya ufungaji mabao msimu huu kwenye Ligi Kuu.

**1. Salah - Firmino - Mane (Liverpool): Mabao 34**

Kama Liverpool itatwaa ubingwa wa Ligi Kuu msimu huu, safu yao ya ulinzi inapaswa kupewa shukrani kubwa zaidi. Hata hivyo, Jurgen Klopp ana safu bora zaidi ya kufunga mabao msimu huu.

Muunganiko wa Mohamed Salah, Roberto Firmino na Sadio Mane umeifanya Liverpool kuwa kwenye kiwango kizuri zaidi na kufunga jumla ya mabao 34 hadi sasa.

Sadio Mane amefunga mabao tisa katika mechi 21 alizocheza hadi sasa, lakini kiwango chake kuna wakati kimekuwa kikiyumba. Amefunga mabao matatu katika mechi 12 zilizopita. Roberto Firmino, kwa upande mwingine ana mabao tisa katika mechi 23, na yupo kwenye kiwango cha juu zaidi. Raia huyo wa Brazil amefunga mabao matano katika mechi zake nne zilizopita na kuwa mmoja wa wachezaji muhimu zaidi kwenye mbinu za Klopp.

Hata hivyo, Salah amekuwa ndio msukani wa kufumania nyavu kwa timu hiyo, kwani hadi sasa amefunga mabao 16 katika mechi 23 alizocheza na anaonekana anakiwania Kiatu cha Dhahabu kwa udi na uvumba.








## NUKUU


"Kama tupo tayari, tupo fiti, na kisha tunapambana, natumai tutasonga raundi inayofuata na bila shaka hii ni ndoto yetu kuichapa Liverpool. Tunajua itakuwa vigumu sana na kuanzia dakika ya kwanza hadi 90 tunapaswa kuwa na mtazamo kwa asilimia 100, ni wazi utakuwa mchezo mgumu na pia wakuvutia," **mshambuliaji wa Bayern Munich, Robert Lewandowski akizungumzia mechi ya 16-Bora Februari 19, mwaka huu dhidi ya Liverpool.**



"Mambo haya ni kwa busara ya kocha, ni nani anayejua ubora wa wachezaji na anajua jinsi walivyo, Ninaweza kusema kidogo zaidi. Data nilizo nazo za wachezaji, hakuna mtu [mwingine] yeyote anazo- ni wale tu waliopo ndani yetu [klabuni]. Ninafanya kile ninachodhani ni bora kwetu na kundi. Kuna minong'ono [inaibuka] kuhusu kuwachezesha wachezaji kwa mzunguko wakati tunapopoteza," **Kocha wa Barcelona, Ernesto Valverde akifunguka kufuatia kukosolewa kwa uamuzi wake wa kumpumzisha Lionel Messi kwenye mechi ya Kombe la Mfalme na timu hiyo kuchapwa 2-0 na Sevilla.**



"Wakati kukiwa hakuna matarajio wala matumaini makubwa ya kumpata akiwa hai, tunaomba mchakato wa kumtafuta uendelee, Emiliano Sala na familia yake yote niko pamoja na nyinyi katika kipindi hiki kigumu, " **aliandika Lionel Messi kwenye ukurasa wake wa mtandao wa Instagram na huku Diego Maradona pia naye akiandika kuhusu Sala aliyepotea na ndege wakati akitoka Ufaransa kwenda England kujiunga na Cardiff City akisema: "Kamwe matumaini hayafi."**






Kipa wa Simba, Aishi Manula, akidaka mpira wakati wa mechi ya nusu fainali dhidi ya Bandari FC ya Kenya, ambayo walichapwa 2-1.

# SABABU 5 SIMBA, YANGA KUPISHANA NA MIL. 70/-

**Na Adam Fungamwango**

KWA mara ya tatu mfululizo timu za Tanzania zimekuwa wasindikizaji kwenye michuano ya SportPesa.

Michuano hiyo huzishikirisha timu za Tanzania na Kenya, lakini inaonekana Kenya imeendelea kutawala michuano hiyo, baada ya timu za Simba, Yanga, Mbao FC na Singida United kusukumizwa nje ya michuano hiyo.

Tangu mwaka 2017, michuano hiyo ilipoanzishwa, hakuna timu yoyote ya Bongo iliyotwaa ubingwa na hata mwaka huu kombe hilo limerudi tena nchini Kenya kufuatia Bandari na Kariobangi Sharks kupepetana fainali jana.

Timu za Bongo zimeshindwa kabisa kutwaa kiasi cha Dola za Marekani 30,000 sawa na Sh, milioni 69.2 za Tanzania kwa mechi tatu tu, huku Ligi Kuu ya Tanzania inayokadiriwa kuwa na kiasi hicho cha pesa kwa bingwa ikicheza mechi 38, pia mpaka sasa kukiwa hakuna uhakika wa kupata pesa hizo kwa kukosekana mdhamini.

Mwaka 2017 michuano hiyo ilifanyika nchini Tanzania na Gor Mahia ikatwaa kombe hilo kwa kuwachapa mahasimu wao wa jadi AFC Leopards mabao 3-0 kwenye mechi ya fainali.

Kwenye michuano hiyo Simba ilitolewa hatua ya robo fainali kwa mikwaju ya penalti 5-4 dhidi ya Nakuru All Stars ya Kenya, huku Yanga ikitolewa nusu fainali pia kwa mikwaju ya penalti 4-2, habari ikaishia hapo.

Mwaka uliofuata 2018 ilifanyika nchini Kenya na kwa mara nyingine tena Gor Mahia ilitwaa ubingwa kwa kuichapa Simba mabao 2-0 yaliyofungwa na Meddie Kagere ambaye kwa sasa anaichezea timu hiyo aliyoifunga na Jacques Tuyisenge.

Yanga iliyaaga mashindano hayo mapema ilipopigwa mabao 3-1 na Kakamega Home Boyz, Singida ikapigwa na Gor Mahia mabao 2-0.

Mwaka huu mambo ni yale yale. Safari ya Simba iliishia kwa Bandari hatua ya nusu fainali ikapigwa mabao 2-1, wakati huo Yanga ilishaondolewa mapema tu kwa mabao 3-2 dhidi ya Kariobangi Sharks, Singida United nayo ikitoka mapema, Mbao FC baada ya kuweka rekodi ya kuwatoa mabingwa mara mbili Gor Mahia, ikaondolewa kwa mikwaju ya penalti nusu fainali dhidi ya Kariobangi.

Cha kujiuliza ni mkosi gani kwa timu za Tanzania kushindwa kutwaa kombe hilo kwa miaka mitatu mfululizo?

Hizi ni sababu tano zinazosababisha timu za Bongo kuwa nyanya kwenye michuano hiyo...

**Ligi dhaifu ya Tanzania.**

Ligi ya Tanzania ina kelele nyingi za vyombo vya habari na pesa, huku ikiwa na mashabiki wengi wanaoifuatilia, lakini haina mvuto na wala si bora. Ni dhaifu kwa maana halisi ya udhaifu.

Ratiba mbovu isiyoeleweka. Kuna baadhi ya timu hazina kabisa wazo la kuusaka ubingwa, badala yake zinatafuta pointi kwa ajili ya kubaki Ligi Kuu tu. Timu zinazoonekana kuusaka ubingwa kwa maneno na vitendo ni Simba, Yanga na Azam tu, zingine zote ni wasindikizaji. Hapa huwezi kupata ligi bora.

Kuwapo kwa waamuzi wabovu, waamuzi wenye maamuzi yanayotia shaka, upendeleo, rushwa, kuwapo kwa tetesi za baadhi ya viongozi kununua mechi, baadhi ya wachezaji wa timu kupokea pesa kwa ajili ya kuziachia timu zingine ushindi, haya yote yanasababisha timu za Tanzania zishindwe kupata ushindi zinapokwenda kucheza mechi halisi, zenye waamuzi bora na timu bora zenye wachezaji wanaojitambua.

***Wachezaji kuchagua mechi***

Sifa zilizopitiliza za kwenye magazeti ya michezo, mitandao ya kijamii na kwenye vijiwe wanazopewa wachezaji wa Kibongo mara nyingi zinawavimbisha kichwa na kuona wao ni zaidi kuliko wachezaji wa timu nyingine.

Matokeo yake wachezaji wanacheza wanapojisikia. Wanaamua ni mechi gani ya kucheza kwa bidii na nyingine wanacheza kama wako kwenye mazoezi. Wanachagua michuano ya kucheza, mingine wanaiona kama vile haina maana. Hawaitilii maanani. Kisa wao ni mastaa. Hii inawafanya washindwe kucheza vema wanapokutana na timu zenye wachezaji wanaojitambua na kujituma kisawasawa kama tunavyozishuhudia kwenye SportPesa Cup.

**Kukosa nguvu**

Ukiondoa timu ya Mbao FC, timu zilizobaki za Tanzania pia zinatatizwa na wachezaji wao kutokuwa na nguvu au stamina za kutosha wanapopambana na timu za Kenya ambazo msingi wao namba moja wa soka ni nguvu.

Wachezaji wa Tanzania wanapata tabu sana wanapokutana na timu ambazo hutumia zaidi nguvu.

Ukiangalia ni wachezaji wachache sana hasa wanaotoka nje ya nchi ndiyo utaona wana stamina, lakini wengi wao hutegemea vipaji vyao tu, hivyo timu za Kenya hutumia udhaifu huo kuziadhibu timu za Tanzania ambazo huwaambukiza hata wachezaji wa kigeni aina yao ya uchezaji.

Ni Mbao pekee inayoonekana kuwa na wachezaji wanaotumia nguvu na ndiyo maana waliwatoa Gor Mahia na hata kutolewa wametoka kwa mikwaju ya penalti kwa sababu walifanana na timu za Kenya.

Wachezaji hawajitumi, hawapambani

Ukiangalia timu za Tanzania utakuta kuna baadhi ya wachezaji hawatekelezi majukumu yao.

Ukiziangalia timu za Kenya na hata Mbao FC, utakutana na aina fulani ya soka la upambanaji na kujituma. Kila mchezaji anamsaidia mwenzake na kufika kwenye eneo kwa wakati husika. Yaani wanacheza kitimu zaidi.

**Soka lisilo na malengo**

Timu za Kenya pamoja na kwamba wachezaji wake wanaonekana hawana vipaji vikubwa, lakini wanacheza kwa malengo.

Wanapocheza unaona kuna kitu wanatafuta. Kuna wakati wanacheza pasi fupi fupi na wakati mwingine pasi ndefu kutokana na mechi jinsi inavyoendelea. Timu za Tanzania zinaonekana kama vile zinafanya shoo ya kucheza soka uwanjani na si kutafuta ushindi kwa hali na mali, tofauti na wenzake Wakenya ambao pamoja na kwamba wanaonekana kupata nafasi chache, lakini wanakuwa nazo makini na kuzitumia.

**NAJUA WAJUA**

MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Mohamed Salah, amefunga bao la kwanza katika mechi tisa za Ligi Kuu msimu huu; takriban mabao matatu zaidi ya mchezaji yeyote.



## MAKALA



# CR7 VS MESSI NANI MKALI WA PENALTI?

**MADRID,** Hispania

CRISTIANO Ronaldo alipangwa kwenye kikosi cha Juventus kwa ajili ya kuendelea kupambana uwanjani katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, dhidi ya Chievo inayoshika nafasi ya tatu kutoka mkiani, Jumatatu ya Januari 21.

Kama ilivyotarajiwa, vinara Juventus waliondoka na ushindi mzuri wa 3-0. Hata hivyo, kitu kisicho cha kawaida kilitokea, wakati Ronaldo aliposhindwa kufunga penalti katika dakika ya saba ya kipindi cha pili.

Ni mara chache mno kwa wachezaji wakongwe kama yeye kushindwa kufunga penalti katika eneo la umbali wa yadi 18 kutoka lango la goli.

Mreno huyo alipiga mpira kwa nguvu kuelekea kona ya chini ya kulia ya goli na golikipa, Stefano Sorrentino akaokoa kiurahisi.

Golikipa huyo mwenye umri wa miaka 39, aliuokoa mpira huo kwa urahisi na kumnyima Ronaldo goli kwenye mchezo huo, ambao aliondoka bila kutikisa nyavu.

Akiwa na rekodi ya kufunga jumla ya penalti 114 kwenye maisha yake ya uchezaji soka, hiyo ilikuwa ni penalti yake ya 25 kukosa na ikiwa imeokolewa na golikipa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 ana asilimia 82% ya kufunga penalti kwa kipindi chote alichocheza.

Ronaldo wakati akicheza pale kwenye mji mkuu wa Hispania akiwa na Real Madrid wakati wote ambao timu yake ilipopata penalti yeye hakuwahi kuwaangusha na ndiye alikuwa mpigaji wao mkuu.

Ikumbukwe kwamba, penalti walizokosa Sergio Ramos na Ronaldo ndio zilizosababisha wakose kutinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2011/12 dhidi ya Bayern Munich.

Hata hivyo, wote wawili wameendelea kupewa jukumu la kupiga penalti kwenye timu zao, kwani licha ya kuwa anacheza nafasi ya ulinzi, Ramos ndiye mpiga mkubwa wa penalti kwa Real Madrid tangu kuondoka kwa Ronaldo aliyetua kule Turin.

Takwimu ambazo zinawaridhisha wote kwa pamoja Ronaldo na mashabiki wake ni kuhusu mpinzani wake mkubwa dimbani, Lionel Messi, kwani hadi sasa wote wanalingana kwa idadi sawa ya kukosa penalti.

Kwani wawili hao kila mmoja amekosa jumla ya penalti 31 katika kipindi chake cha uchezaji.

Messi amefunga jumla ya mabao ya penalti 83 na amekosa kama ilivyo kwa Ronaldo penalti 25 kila mmoja kwa ngazi ya Klabu.

Kwa mafanikio ya penalti 83 alizofunga kati ya 108 alizopiga ana uwiano wa asilimia 77.

Ukichukulia kwa tofauti ya mafanikio, Mreno huyo yupo juu ya Lionel Messi, kwani yeye amepiga penalti nyingi zaidi.

Mara zote kunakuwa na vitu vidogo vinavyowatofautisha magwiji hawa kwenye soka la kizazi chao cha soka.

Utawala wao wa kushinda tuzo ya Ballon d'Or ulimalizwa hivi karibuni na nahodha wa Croatia, Luka Modric.

Ingawa wawili hao hawajaonyesha ishara ya kukata tamaa, kwani wote wawili wanaongoza kwa ufungaji wa mabao kwenye ligi zao.

Ronaldo ana mabao 14 kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, wakati Messi ana mabao 18 kwenye Ligi Kuu ya Hispania, La Liga.

Na ni wazi kwamba kila mmoja ana malengo ya kumaliza msimu huu akiwa kinara wa ufungaji mabao kwenye ligi yake.

Akizungumzia kiwango cha Cristiano Ronaldo kwenye mchezo huo, kocha wa Juventus, Allegri alisema, "Nadhani kama si mara ya kwanza kwa Ronaldo kukosa penalti katika maisha yake ya soka.

"Jambo la msingi ni kwamba mwisho wa siku timu ilishinda mchezo. Yeye (Ronaldo) alitaka kufunga na kiufundi katika kipindi cha pili alicheza vizuri zaidi.

"Katika kipindi cha kwanza alikuwa na haraka ya kutaka kufunga mara kwa mara. Lakini katika kipindi cha pili alicheza kwa utulivu, na timu ilicheza mpira wa kuvutia na alikuwa na nafasi ya kufunga mabao kama mara mbili au tatu."

**NDANI YA 18**

MANCHESTER United ndiyo pekee kwenye Ligi Kuu England hadi sasa ambayo imeshashinda penalti nyingi (saba) wakati Brighton ndiyo imeruhusu penalti nyingi kujaa kimyani (saba) kuliko klabu nyingine za Ligi Kuu England msimu huu.





LIGI Kuu England (EPL), tayari imefikia nusu ya msimu na mambo yanaonekana kwenda sawa. Kwenye kilele cha msimamo, Liverpool imeendelea kujikita kileleni mwa msimamo huo ingawa Manchester City ipo jirani na visigino vyake.
**Uk. 16-17**

# 10- BORA USAJILI GHALI WA JANUARI ENGLAND



Van Dijk

**LONDON,** England

USAJILI wa dirisha dogo la Januari unaweza kuwa wa majaribu kwa klabu nyingine kufanya uhamisho, lakini kuna kiasi kikubwa cha fedha kilichotumiwa kwenye Ligi Kuu England katika miaka ya hivi karibuni.

Liverpool ilivunja rekodi wakati wa usajili wa Januari mwaka jana ilimpomsajili, Virgil van Dijk kutoka Southampton kwa pauni milioni 75.

Hapa tunakuchambulia 10 bora ya usajili wa fedha nyingi zaidi uliofanywa wakati wa dirisha la Januari kwenye Ligi Kuu England.

**1. Van Dijk - Pauni milioni 75, Southampton kwenda Liverpool**

Zilikuwa fedha nyingi, lakini Virgil van Dijk ameonyesha thamani yake hadi sasa. Beki huyo ameisaidia kuimarisha safu ya ulinzi ya Liverpool na kuifanya kuwa moja ya ngome ngumu zaidi kwenye Ligi Kuu ya England. Van Dijk alikamilisha usajili wake wa kutoka Southampton Januari Mosi, mwaka 2018, akiwa mara kadhaa alikaribia kutua hapo kwenye dimba la Anfield. Alitajwa kuwa mchezaji bora wa Ligi Kuu Desemba mwaka jana baada ya Liverpool kuruhusu mabao matatu tu kwenye mechi saba.

**2. Aubameyang - Pauni milioni 60, Borussia Dortmund kwenda Arsenal**

Arsenal ilivunja rekodi yake ya usajili kwa kumsajili, Pierre-Emerick Aubameyang kutoka Dortmund mwaka jana. Hakuchukua muda mrefu kuweza kuzoea mazingira na kufunga mabao 10 katika mechi 12 alizoanza kwenye Ligi Kuu ikiwa ni nusu ya pili ya msimu uliopita. Amekuwa na msimu wa kufurahisha zaidi 2018/19 na ni mmoja wa wachezaji anayeongoza kwa kuzifumania nyavu kwenye Ligi Kuu akiwa na mabao 14.

**3. Pulisic - Pauni milioni 57.6, Borussia Dortmund kwenda Chelsea**

Ingawa Christian Pulisic hatajiunga na Chelsea hadi kipindi cha majira ya joto, uhamisho wake kutoka Dortmund umethibitishwa mwezi huu. Mchezaji huyu wa kimataifa wa Marekani amekuwa mchezaji wa pili ghali zaidi katika historia ya Chelsea, baada ya Alvaro Morata. Klabu kadhaa za Ligi Kuu ya England zilikuwa zikimuwania Pulisic, ambaye msimu huu amekuwa hachezi mara kwa mara kwenye kikosi cha kwanza, baada ya Jadon Sancho kumzidi kete pale Dortmund.

**4. Laporte - Pauni milioni 57, Athletic Bilbao kwenda Ma City**

Aymeric Laporte alikuwa hachezeshwi mara kwa mara kwenye kikosi cha Man City kilichotwaa ubingwa wa Ligi Kuu baada ya kujiunga nao Januari mwaka 2017, lakini msimu huu amekuwa akichezeshwa mara kwa mara na kuwa mmoja wa mabeki wa kati bora zaidi kwenye hiyo. Ameanza katika mechi 21 kati ya 22 kwenye Ligi Kuu na Pep Guardiola ameimba wimbo wa kumsifia. "Mwisho wa siku kukiondoa kikosi, lakini wakati mchezaji mmoja anapocheza vizuri, vizuri na vizuri, inanipa mimi imani na kumpa nafasi nyingine. "

**5. Torres - Pauni milioni 50, Liverpool kwenda Chelsea**

Chelsea walipora mshambuliaji wa Liverpool kipindi cha usajili wa Januari mwaka 2011 na ilionekana kama, Fernando Torres angekuwa na mafanikio makubwa zaidi baada ya kuwa na kiwango cha kuvutia pale Stamford Bridge. Baada ya kufunga mabao 65 kwenye Ligi katika misimu mitatu na nusu hapo, Mhispania huyo aliweza kufunga mabao 20 kwa muda kama huo wakati akiwa Chelsea. Bao lake linalokumbukwa ni nile la nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Barcelona.

**6. Mata - Pauni milioni 37.1, Chelsea kwenda Man United**

Mchezaji bora wa mwaka mara mbili wa Chelsea aliuzwa kwa Manchester United wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari 2014, wakati Mhispania huyo alipoonekana kutokuwa kwenye mipango ya kocha, Jose Mourinho. Wakati Juan Mata alichukua muda mrefu kuweza kuwa kwenye kiwango alichokionyesha kule Stamford Bridge, aliufurahia msimu wa 2014/15 ambapo alifunga bao la adhabu ndogo dhidi ya Liverpool. Tangu hapo ameichezea Man United mechi 300, ingawa mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu.

**7. Carroll - Pauni milioni 35, Newcastle kwenda Liverpool**

Moja katika ya usajili unaokumbukwa zaidi kufanywa siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la usajili ni ule wa Andy Carroll wakati anajiunga na Liverpool Januari mwaka 2011. Baada ya kuwa na kiwango cha kuvutia Newcastle na kufunga mabao 11 kwenye nusu ya kwanza ya msimu, Carroll alisajiliwa na kocha Kenny Dalglish. Hata hivyo, kutokana na kukumbwa na majeraha ya mara kwa mara, kipindi cha Carroll kucheza hapo Liverpool kilihitimishwa Mei 2013 na akajiunga na West Ham, ambako aliwahi pia kukaa huko kwa mkopo. Carroll amekuwa akisumbuliwa na majeraha na atakuwa hana mkataba mwishoni mwa msimu.

**8. Dzeko - Pauni milioni 32.5, Wolfsburg kwenda Man City**

Mchezaji huyu wa kimataifa wa Bosnia alifunga mabao 66 katika mechi 111 alizocheza nchini Ujerumani na kuisaidia Wolfsburg kushinda taji la Ligi Kuu ya Bundesliga mwaka 2009 na kocha Roberto Mancini alimchukua mwaka 2011. Licha ya kuwa mfungaji wa mara kwa mara kwa City na kutwaa mara mbili taji la Ligi Kuu, Edin Dzeko alijikuta akishindwa kupata namba ya kudumu chini ya makocha Mancini na Manuel Pellegrini. Aliondoka na kujiunga na AS Roma wakati wa kipindi cha majira ya joto mwaka 2016 na alikuwa na wakati mzuri, hadi msimu huu kujikuta akishindwa kupenya kwenye kikosi cha kwanza.

**9. Bony - Pauni milioni 28, Swansea City kwenda Man City**

Moja ya sababu kubwa ya Dzeko kufunguliwa mlango wa kuondoka pale Man City ni ujio wa Wilfried Bony mwaka 2015 wakati wa dirisha dogo la Januari. Usajili huo ulimfanya kuwa mmoja wa wachezaji wa Afrika waliosajiliwa kwa fedha nyingi zaidi wa wakati wote. Na mchezaji huyo wa zamani wa Vitesse Arnhem alikwenda Man City na kuwa mfungaji bora wa kikosi hicho akiwa na mabao 20. Hata hivyo, kama ilivyokuwa kwa Dzeko, Bony alishindwa kupenya kwenye kikosi cha kwanza dhidi ya Sergio Aguero. Alitumia msimu wa 2016/17 akicheza kwa mkopo katika klabu ya Stoke na baadaye akarudi Swansea kipindi cha majira ya joto kilichopita.

**10. Tosun - Pauni milioni 27, Besiktas kwenda Everton**

Wakati Cenk Tosun aliposajiliwa na Everton mwaka jana alisema kwamba, kocha Sam Allardyce alichangia kwa kiasi kikubwa yeye kufanya maamuzi ya kwenda Goodison Park. Tosun alikuwa akianza mara kwa mara chini ya Allardyce na alionyesha ishara nzuri ya kuimarika zaidi, lakini msimu huu amekuwa akitumika akitokea benchi, kwani kikosi cha kwanza anacheza Marco Silva. Kumekuwa na uvumi kwamba anaweza kuondoka Everton, akiwa amefunga mabao mawili tu kwenye msimu huu wa 2018/19.

**USILOLIJUA**

MANCHESTER City haijawahi kupoteza mechi yoyote kati ya 20 ambazo Gabriel Jesus alifunga bao kwenye Ligi Kuu; imeshinda 19 na kutoka sare moja (W19 D1), huku ikishinda zote katika 17 zilizopita.







# Wadai kuporwa eneo lao ekari 87

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WAKAZI wa Kitongoji cha Mdodela Kata Rujewa katika Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wamedai kukosa maeneo ya kulima baada ya mtu mmoja kuwapora eneo walilokuwa wanalima lenye ukubwa wa ekari 87.

Wananchi hao walidai kuwa waliporwa ardhi hiyo tangu mwaka 2015 na kwamba mpaka sasa wanahangaika kupata maeneo kwa ajili ya kuendesha shughuli za kilimo wakati mgogoro huo ukiwa bado kupata ufumbuzi.

Katibu wa Kamati ya ufuatiliaji wa mgogoro huo, Baraka Mwilongo, alisema kuwa licha ya jitihada za kutatua mgogoro huo, lakini kumekuwapo na mizengwe kutoka kwa baadhi ya watendaji wa halmashauri kukwamisha kwa makusudi.

Alisema kuwa mwezi Agosti, mwaka 2015, watalaam sita kutoka Ofisi ya Mkurugenzi na baadhi ya wananchi sita wa kitongoji cha Mdodela pamoja na mtu anayetajwa kupora eneo hilo walikutana na kuafikiana juu ya hatima ya eneo hilo.

Mwilongo alisema katika makubaliano hayo, waliazimia wananchi wapewe ekari 57 ili waendeleze kilimo na kigogo huyo abaki na ekari 30, lakini bado mvamizi huyo hajatekeleza na anaendelea kuyatumia mashamba yote.

"Mmwaka 2018 aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Amos Makalla, aliagiza wananchi wa eneo hili la Mdodela na vitongoji vingine kupewa ardhi iliyoporwa, lakini utekelezaji umekuwa ukisuasua licha ya maagizo ya wilaya kubainisha kuamua tupewe eneo letu," alisema Mwilongo.

Alidai kuwa malalamiko ya wananchi hao kuhusu eneo hilo yanajumuisha vitongoji vitatu ambavyo ni Jangulutu A, Kanisani na Mdodela na kuwa wananchi wengi hususani vijana wamekosa mahali kwajili ya shuguli za kilimo na hivyo kugeuka kuwa vibarua baada ya eneo lao kuporwa.

Mwenyekiti wa Kitongoji wa Mdodela, Steven Lusuva, wamekuwa wakifanya jitihada za kulirejesha eneo hilo, lakini changamoto ni kwamba wananchi hao wanakosa ushirikiano kutoka ofisi za serikali ngazi ya Kata.

"Kuna mambo yanafanyika hata ofisi ya kitongoji haifahamu chochote na kumekuwa na maagizo ambayo yamekuwa hayazingatii taratibu za kiutendaji na hivyo kunifanya mimi nishindwe kusimamia mgogoro huo kwa ukamilifu," alisema.

Akizungumza na gazeti hili Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Ruben Mfune, alikiri kuufahamu mgogoro huo na kuwa amekuwa akishirikiana kwa ukaribu na kamati ya wananchi hao ambao wanafuatilia mgogoro huo.

Alisema kuwa mpaka sasa wananchi hao wameshatoa gharama za kulipima eneo hilo kama wataalamu wa halmashauri hiyo walivyoshauri kabla ya kuwagawia eneo lao kwa mujibu wa makubaliano ambayo yalilenga zaidi kuwanufaisha vijana.

# Watamani kutembea hadi Ikulu kumshukuru JPM

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WANANCHI wa vijiji 32 vya Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya vilivyokuwa vinatakiwa kuondolewa ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, wamesema wanatamani kutembea kwa miguu mpaka Ikulu kwenda kumshukuru Rais Dk. John Magufuli kwa uamuzi alioufanya wa kuzuia visiondolewe.

Waliyasema hayo juzi wakati wa mkutano wa hadhara uliofanyika katika Kijiji cha Mwanavala, Kata ya Imalilo - Songwe kati ya wakulima na wafugaji wa wilaya hiyo kuwa kabla ya uamuzi wa rais walikuwa wanateseka kwa zaidi ya miaka 12.

Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika wa Nguvu Kazi Mwanavala ambao ni wakulima wa Mpunga, Juma Kanyamala, alisema kati ya vijiji na vitongoji 366, alivyovitaja rais na wao wameguswa kwa kiasi kikubwa.

Alisema asilimia kubwa ya wananchi wa wilaya hiyo ajira yao ni kilimo na ufugaji na kudai kuwa endapo serikali ingeendelea na tafsiri ya tangazo lake namba 28 la mwaka 2008 (GN. 28) lililokuwa linafuta vijiji hivyo ajira zao zingekufa.

**Wafugaji walikumbwa na changamoto za kufukuzwa katika maeneo hayo na kwamba awali walikubwa na operesheni iliyokuwa inajulikana kwa jina la 'operesheni ondoa mifugo' ambayo alidai ilisababisha mifugo yao kupotea.**

"Tuna furaha kubwa sana wakulima na wafugaji wa Mbarali na tungekuwa tunaweza tungeandamana kwa miguu mpaka Ikulu tukamshukuru rais wetu, kwa sasa tunasubiri siku akifanya ziara Mbeya tutatembea mpaka eneo atakalokuwa anapokelewa," alisema Kanyamala.

Alimpongeza rais kwa kazi nzuri anayofanya ya kuwatumikia Watanzania huku akisisitiza kuwa wakati mwingine baadhi ya wasaidizi anaowateua ndio huwa wanamdanganya kwa kumpa taarifa za uongo.

Alisema katika skimu ya umwagiliaji ya Mnazi, wakulima wanaolima wapo 460, lakini baadhi ya wasaidizi wa rais walikuwa wanasema wakulima hao hawazidi 50. Mwenyekiti wa Chama cha wafugaji wilaya ya Mbarali, Moses Fute, alisema kabla ya rais kutoa tamko la kutoondolewa kwa vijiji hivyo, wafugaji walikuwa wanaishi kama wakimbizi ndani ya ardhi yao.

Alisema kutokana na mgogoro huo uliodumu kwa muda mrefu, wananchi wa maeneo hayo walipoteza mali zao nyingi, wengine waliumia na wengine walipoteza maisha kwenye harakati za kugombea maeneo hayo.

Alisema wafugaji walikumbwa na changamoto za kufukuzwa katika maeneo hayo na kwamba awali walikubwa na operesheni iliyokuwa inajulikana kwa jina la 'operesheni ondoa mifugo' ambayo alidai ilisababisha mifugo yao kupotea.

Aidha, kiongozi huyo aliwataka wafugaji kuendelea kuheshimu mipaka ya hifadhi mpaka wataalamu watakapoainisha mipaka kama alivyoagiza Rais Magufuli alipokuwa anaongea na mawaziri pamoja na makatibu wakuu.

Kwa upande wake, Meneja wa Ushirika wa Nguvu Kazi Mwanavala, Christopher Uhagire, alisema pamoja na pongezi walizotoa kwa rais, lakini wanaahidi kufanya kwa vitendo ikiwa ni pamoja na kuheshimu sheria zikiwamo za uhifadhi na mazingira.

Aliwataka wakulima kuendelea kuiheshimu dheria inayozuia kufanya shughuli za kilimo ndani ya mita 60 kutoka kwenye kingo za mito na vyanzo vya maji.



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Nape Nnauye (aliyenyoosha mkono), akiwa na baadhi ya wajumbe wa kamati hiyo akiwaonyesha kundi la tembo, walipofanya ziara ya siku mbili ya kikazi ya kukagua utekelezaji wa mradi wa kukuza na kuendeleza utalii Kusini katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha mkoani Iringa mwishoni mwa wiki. **PICHA: WMU**

# CCM Kyela yapania ushindi Serikali za Mitaa

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

VIONGOZI wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, umeaswa kuwaunganisha wanachama ili kuwa na uhakika wa kupata ushindi kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika mwaka huu.

Hayo yalisemwa juzi na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Stephen Mwakajumilo, wakati wa ziara ya kukagua maendeleo ya chama hicho unaofanyika katika wilaya zote za Mkoa wa Mbeya.

Alisema katika baadhi ya maeneo ya wilaya hiyo, chama hicho kina mpasuko ambao unahatarisha uhai wake hasa kuelekea kipindi cha uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu wa 2020.

Aliwataka viongozi wa chama hicho kuwaunganisha wanachama wote wawe kitu kimoja kwa kuondoa makundi yasiyokuwa na tija ambayo yanaweza kukiathiri chama kwenye chaguzi.

"Kama kweli tunataka kupata ushindi ni lazima kila kiongozi ahakikishe anawaunganisha wanachama, wilaya hii ni miongoni mwa zinazotupa wasiwasi kutokana na kuwa na dalili za mpasuko wa wanachama," alisema Mwakajumilo.

Naye Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM Mkoa wa Mbeya, Bashiru Madodi, aliwataka wananchi kujitokeza kujiandikisha kwenye daftari la kudumu la wapigakura muda utakapowadia wa kufanya hivyo kwa mujibu wa sheria.

Alisisitiza kuwa endapo wanachama wa CCM watahamasishwa kujiandikisha itakuwa ni nafasi pia ya kuitumia katika kupata ushindi kwa kuwa wanaoruhusiwa kupiga kura ni wale waliojiandikisha pekee.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kyela, Ally Kinanasi, aliuhakikishia uongozi wa chama ngazi ya mkoa na taifa kuwa chama hicho kiko vizuri na kitapata ushindi kwenye chaguzi zote zinazokuja.





# Wabunge CCM wampongeza JPM

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WABUNGE wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wamempongeza Rais John Magufuli kwa kukutana na wadau wa madini na kuzitaka wizara zingine kuiga jambo hilo lenye maslahi sio kwa wachimbaji tu bali hata kwa taifa kwa ujumla.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wabunge hao walisema kuwa mkutano huo ulikuwa wa kihistoria kwa kuwa zipo njia nyingi za kuzungumza na kusema kuwa rais kuwapo pale ni jambo kubwa.

Mbunge wa jimbo la Iramba Mashariki, Wilaya ya Mkalama, Mkoa wa Singida, Alan Kiula, alisema kuwa wadau walikuwa na mambo mengi ambayo yalikuwa hayajafanyiwa kazi na wizara husika.

"Wadau wamekulia katika sekta hiyo na wanajua inafanya kazi vipi, kwani tunao wasomi wengi ambao wamesomea kazi ya madini, lakini inawezekana walikuwa hawaendi sambamba na wachimbaji wadogo wadogo wa madini," alisema Kiula.

**Hivyo ule mkutano ulikuwa ni wa muhimu uliweka mawazo pamoja na kuchambua, mkileta mawazo ya pamoja mnakuja na suluhisho la pamoja.**

"Hivyo ule mkutano ulikuwa ni wa muhimu uliweka mawazo pamoja na kuchambua, mkileta mawazo ya pamoja mnakuja na suluhisho la pamoja," alisema.

"Rais Magufuli alisema anatambua kuwa Tanzania ni nchi tajiri tuna madini mengi sana ikiwamo vito, lakini ukiangalia takwimu hazionyeshi kuwa nchi yetu ndio wazalishaji, kuna nchi ambazo hazina madini na wanaonekana ni wazalishaji wa madini mengi, kwanini sisi tusiwamo kwenye orodha, inaleta maswali mengi sana kwa rais na watafiti wa mambo ya kiuchumi," alisema.

Pia alisema mara kadhaa rais amekuwa akisema kuwa anataka kuona mchango wa kila sekta, na alisema wananchi wanahitaji maji, dawa, barabara, lakini vyote hivyo vitatekelezwaje kama mchango wa kila sekta hauonekani.

Aidha, alisema kuwa wachimbaji wadogo wakiwekewa mazingira mazuri wakafanya kazi yao ya uchimbaji, kutengenezewa masoko mazuri mchango wao lazima utaonekana.

"Kuna kodi mbalimbali kupitia madini murahaba na hata ajira zinapatikana kupitia madini na kodi nyingine, lazima eneo hili lirasimishwe na kuwa linalo tambulika," alisema.

Mbunge huyo alisema kuwa rais anafanya yote hayo kwa sababu anaamini kuwa kuna fursa kwenye sekta ya madini ambayo haijatumiwa vizuri na wachimbaji wenyewe na serikali haijapata mapato yanayo takiwa.

"Tunatarajia mapendekezo yatakayo tolewa yatajadiliwa na timu ya wataalamu kwa kuwa pamoja na mambo waliyo yazungumza lazima mapendekezo yaliyotolewa yaangaliwe na kujadiliwa kwa mapana yake na yale yanayoweza kutekelezwa naamini rais atayafanyia kazi"alisema.

Hata hivyo, alisema kuwa viongozi wanatakiwa kuwa na jicho la mwewe ili kufanya kazi kwa ukaribu na umakini zaidi.

Kwa upande wake Mbunge wa Jimbo la Nanyambwa, mkoani Mtwara Abdallah Chikota (CCM), alisema kuwa sekta ya madini inachangia pato la taifa, lakini sio kwa kiwango kinacho ridhisha.

Alisema hata wakati wa mjadala bungeni huwa wanaiambia wizara hiyo kuongeza mbinu mbalimbali ili kuhakikisha mapato ya sekta hiyo yanaongezeka.

Alisema kuwa sekta ya madini ikitatuliwa changamoto zilizopo, inaweza kuongeza pato maradufu kuliko hata kinachopatikana kwa sasa.

"Suala ni TRA, Wizara ya Fedha na Madini kujipanga ili kuondoa kero zilizopo, kuondoa tozo nyingi ambazo vyombo mbalimbali vinamtoza mchimbaji mdogo ili aweze kulipa kodi moja au mbili na ambayo inaweza kulipika kwa urahisi," alisema.

"Tukisimamia vizuri na kero zilizopo zikaondolewa na kodi ikawa inalipika kwa urahisi na kwa kiwango amabacho mdau anaweza kukilipa inaweza kuongeza hadi asilimia 25 kwenye pato la taifa," alisema Chikota.

Alisema kuwa sekta zingine zinafanya mikutano na wadau, lakini unapokutana na mkuu wa nchi kuna majibu mengine unayapata papo kwa papo, hivyo wananchi wanapopata nafasi kama hiyo wahakikishe wanaitumia vizuri.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, akiangalia moja ya majalada ya ardhi aliyokagua katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma wakati wa uhamasishaji ulipaji maduhuli ya serikali kupitia kodi ya ardhi, kushoto kwa waziri ni Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, Vumilia Nyamuga na kulia ni Ofisa Ardhi Mteule, Letare Shoo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Kondoa yazindua Baraza la Wafanyakazi

**Na Paul Mabeja,** KONDOA

HALMASHAURI ya Mji Kondoa mkoani Dodoma imezindua Baraza la wafanyakazi ikiwa ni halmashauri ya pili katika Mkoa wa Dodoma kufanya hivyo.

Akizungumza katika uzinduzi wa baraza hilo, Katibu Tawala wa Wilaya ya Kondoa, Andrea Mwani, alisema kuwa uwapo wa baraza hilo utasaidia kuimarisha ushirikiano kati ya watumishi na mwajiri.

"Mnaweza mkaona katika uongozi huu wa awamu ya tano jinsi mheshimiwa rais anavyofanya mabadiliko ya kuiendeleza nchi na wa kuyafanya haya ni sisi wafanyakazi hivyo kila mmoja awajibike katika eneo lake na kujitathimini ili tuendane na upepo uliopo," alisema Mwani.

Aidha, alisisitiza wafanyakazi kufanya kazi na kutimiza majukumu yao walioajiriwa nayo kwa asilimia zote pamoja na melekezo wanayopewa kwa kuwa kwa kufanya hivyo wanamsaidia rais kuwahudumia wananchi.

Mkurugenzi wa Mji wa Kondoa, Msoleni Dakawa, alisema kuwa baraza limeanzishwa baada ya kuona umuhimu wa wafanyakazi kwakuwa ndio mzalishaji na mtekelezaji wa maagizo na ahadi zinazotolewa na serikali.

"Niombe kwa wakati mwingine kwa umoja huu tulioonyesha na vyama vya wafanyakazi tuendelee nao iwe wakati wa shida na raha kwa kuwa lengo ni kuhakikisha mambo yanaenda na tunawajibu wa kupambana kama anavyofanya mheshimiwa rais lengo likiwa kuwahudumia wananchi na kuwapatia haki zao watumishi," alisisitiza Dakawa.

Mwakilishi wa vyama vya wafanyakazi, Katibu wa TUGHE mkoa wa Dodoma, Mchenya John, alisema kuwa baraza la wafanyakazi ni chombo muhimu cha maamuzi kwa halmashauri na kuwataka wajumbe wa baraza kuacha uoga na kujadili mambo yatakayowasaidia kuendesha halmashauri na maslahi ya watumishi.

"Namshukuru sana heshimiwa rais kwa kulitolea maamuzi suala la kikokotoo kwa kuwa liliwakatisha taama wafanyakazi na nilishakuja hapa mwaka jana nikapata fursa ya kuongea na wafanyakazi na nashukuru walinielewa na kuwa watulivu wakati wote wa mpito hadi Rais alipolitolea maamuzi," alisema Mchenya.

# Wateja NMB sasa kutuma na kuweka pesa bila tozo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

BENKI ya NMB imefuta tozo za huduma za kibenki za kutuma na kuweka fedha ili kumrahishishia mteja kuendelea kutumia huduma hiyo bila kuwa na gharama.

Utafiti uliofanywa kuhusu huduma za kibenki umegundua mteja anapata mzigo katika huduma mbalimbali ikiwamo kutoa na kutuma pesa kwenda kwenye akaunti nyingine.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkuu wa kitengo cha malipo wa NMB Mike Lungure, alisema kuanzia Februari mosi, mwaka huu, huduma hiyo itakuwa bure. Alisema wamechukua maamuzi ya kutoa tozo katika huduma hizo kutokana na wateja kushindwa kujiunga na huduma za kibenki kwa kuhofia tozo hizo.

Alisema kutokana na mipango na dhamira waliyopanga kwa mwaka huu ni kuhakikisha kila mteja anapata huduma za kibenki bure.

"Tozo za kila mwezi tumeziondoa hivyo mteja atafanya kila kitu bure, kama mtu alikuwa na akaunti yake ambayo hakuwa anaitumia kwa sasa kufufua ni bure afike kwenye tawi la benki," alisema Lungure.

Alisema kwa sasa mteja yeyote anaweza kufungua akaunti popote alipo kwa kutumia simu yake ya mkononi ili kuondoa usumbufu wa kutumia muda mrefu katika benki kwa ajili ya kufungua akaunti, Lungure alisema kuwa gharama za huduma za ATM zimepanda kwa sasa, lakini kwa upande wao wamemfikiria mteja na kumuwekea huduma za kimtandao bure kwa kuhamisha pesa kutoka akaunti moja kwenda nyingine, kufahamu maelezo ya kina kuhusu akaunti yake na hata kuangalia salio.





# Serikali yasisitiza elimu ya maandalizi vyuo vikuu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Mmanga Mjengo Mjawiri, amesema ili kupata matokeo mazuri ya wanafunzi katika mitihani ya elimu ya juu na vyuo vikuu, juhudi kubwa inahitajika kuimarisha elimu ya maandalizi na msingi.

Alisema maofisa elimu na walimu wakuu wa shule za msingi wanapaswa kuwa wasimamizi na wafuatiliaji wa karibu wa kazi za kila siku za walimu wao ili malengo yaliyowekwa ya elimu yaweze kufikiwa.

Alisema hayo alipokuwa akizindua mradi wa mafunzo ya kuwajengea uwezo walimu wa masomo ya Sayansi, Kiingereza na Hesabati wa darasa la tano na sita wa shule za Unguja ili waweze kutoa msaada kwa wanafunzi na kuongeza ufaulu wao.

**Msimamo wa Wizara ya Elimu kuwa kuanzia sasa inataka kuona mafunzo yanayotolewa kwa walimu wa shule yanaleta mabadiliko na kuongeza ufanisi.**

Alisema imebainika kuwa pamoja na juhudi zinazochukuliwa za kuwapatia walimu mafunzo ya mara kwa mara, suala la ufuatiliaji limekuwa ni tatizo kubwa kwa shule nyingi za Zanzibar.

Alisema kuwa msimamo wa Wizara ya Elimu kuwa kuanzia sasa inataka kuona mafunzo yanayotolewa kwa walimu wa shule yanaleta mabadiliko na kuongeza ufanisi.

Aliwataka walimu wakuu kuwa wabunifu katika kuongoza na kushirikiana na maofisa elimu na viongozi wa halmashauri, hasa wakati huu wa ugatuzi, kubuni mbinu mpya za kuendeleza mbele shule zao.

Aidha, aliwataka walimu wakuu kujitambua na kuthamini nafasi waliyopata huku wakijenga upendo kwa walimu, wanafunzi na kujiepusha kufanya makosa ambayo yanaweza kuwavunjia heshima mbele ya jamii.

Akizungumza katika uzinduzi wa mradi huo katika kampasi ya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar, Mkurugenzi wa Idara ya Mafunzo ya Walimu, Maimuna Fadhil Abass, alisema kwa vile elimu ya msingi imeingizwa katika ugatuzi, viongozi wa wilaya wanatakiwa kuipokea na kuifanyia kazi huku Wizara ya Elimu ikiendelea na wajibu wa kusimamia sera.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Mjawiri, alisema zipo baadhi ya shule zinawalimu wazuri, lakini zimeshindwa kutoa mwanafunzi hata mmoja kwenda michepuo jambo linaloashiria uwajibika mdogo kwa shule hizo.

Alisema lengo la wizara ni kuona kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wa michepuo kinaongeza kila mwaka na wameandaa zawadi maalum kwa shule itakayo ongeza kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wao kwa kila mwaka.



Mchuuzi wa mihogo ya kukaanga, akiandaa kwa ajili ya wateja katika eneo la Mabibo Mwisho, jijini Dar es Salaam jana, huku mazingira yanayomzunguka yakiwa ni hatarishi kwa afya ya walaji. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Waislamu watakiwa kutumia misikiti kuimarisha umoja

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAUMINI wa dini ya Kiislamu wamekumbushwa kuendelea kutumia misikiti kwa ajili ya malezi mazuri ya kidini kwa watoto pamoja na jamii kuimarisha umoja na mapenzi.

Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi, alisema nyumba hizo za Mwenyezi Muungu zinapaswa kuwa nguzo ya ibada, elimu, maarifa na malezi kwa watoto.

Akifungua msikiti salama uliojengwa kwa nguvu za waumini pamoja na misaada ya wahisani huko Maungani Wilaya ya Magharibi 'B', Unguja, Balozi Iddi, alisema waumini wanapaswa kuilinda misikiti kutokana na mitazamo yenye mwelekeo wa kuwagawa waumini, kimadhehebu au kisiasa.

Alisema kumekuwa na ongezeko kubwa la dhuluma na mmong'onyoko wa maadili unaochangiwa na vitendo vya ubakaji, ulawiti, udhalilishaji wa watoto na utumiaji wa dawa za kulevya kwa kiwango cha kutisha.

Aliwakumbusha maulamaa kutimiza wajibu wao kwa kuwahimiza wazazi na walezi kuwaongoza watoto katika maadili na kuwasimamia vyema ili kuhakikisha wanahudhuria kwenye nyumba za ibada.

" Masheikh wetu wajitahidi kuielimisha Jamii juu ya athari ambazo Mja anaweza kuzipata kwa kuendeleza vitendo viovu," alisema.

Akisoma risala kwa niaba ya waumini, Dk. Ali Uki, alisema ujenzi huo ulioanzishwa kwa nguvu za waumini, uliungwa mkono na taasisi moja ya kiserikali.

Msikiti huo wenye uwezo wa kusaliwa na waumini 250, umegharimu zaidi ya Sh. milioni 200.

# Mfuko kuwawezesha vijana nyanja za uchumi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Mfuko wa 'KhalifaFund' Naizar Cheniour, amesema mfuko huo umeazimia kuwawezesha vijana wa Zanzibar katika nyanja mbalimbali za kiuchumi ili kuajiri na kuinua hali zao za maisha.

Alisema hayo wakati alipozungumza na waandishi wa habari, baada ya ujumbe wa Mfuko huo kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume.

Ujumbe huo upo Zanzibar kwa ziara maalum, ikiwa ni mwendelezo wa mazungumzo na serikali, yenye lengo la kufanikisha utekelezaji wa programu mbalimbali katika sekta za biashara, ujasiriamali, miundombinu na nyengine.

Alisema mfuko umelenga kuwawezesha vijana wa Zanzibar , upatikanaji wa rasilimali fedha, utaalamu na masuala ya kiufundi ili waweze kujiajiri kupitia shughuli za ujasiriamali na hivyo kuweza kujitegemea.

Aliwataka vijana na Wazanzibari kwa ujumla kutarajia mafinikio makubwa kutokana na programu mbalimbali zitakazotekelezwa kupitia Mfuko huo.

Alisema mfuko wa KhalifaFund, una uzoefu mkubwa katika utekelezaji wa programu za maendeleo na shughuli za kiuchumi na umekuwa ukifanya kazi hizo katika nchi mbalimbali duniani.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara na Viwanda, Dk. Juma Ali Juma, alisema ujio wa viongozi wa Mfuko huo umelenga kukamilisha mazungumzo yaliofikiwa katika kikao kilichopita ili kuwa tayari kwa utekelezaji wa yale yalioafikiwa.

Alisema mfuko huo wa kifedha, wenye makao makuu yake Abu Dhabi , UAE, utatowa msukumo mkubwa katika utekelezaji wa programu mbali mbali za kimaendeleo na kiuchumi, sambamba na kuwawezesha vijana kupitia kazi za ujasiriamali.

Alisema wakati ukiwa Zanzibar utakutana na kufanya mazungumzo na taasisi mbalimbali za serikali pamoja na kutembelea maeneo tofauti.

Hii ni mara ya pili kwa viongozi wa Mfuko wa KhalifaFund kufika Zanzibar kwa ajili hiyo, kabla ulipata fursa ya kutembelea sekta tofauti za maendeleo na kiuchumi Unguja na Pemba.

# RATIBA

## CAPITAL TELEVISION

**Mon 28 Jan**
06:00 Al jazera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the spotlight rpt:
12:30 Drive it rpt
13:00 Series rpt :
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Usafiri wako rpt
15:00 Cookery rpt: Culinary Delight
15:30 Toyota world of wildlife rpt
16:00 CNN International
17:00 Eco@Africa rpt
17:30 Meza huru
19:00 The Décor rpt
19:30 Business edition
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 The Monday Agenda
21:30 Capital Prime News
22:00 Kipima Joto
00:00 Al Jazeera

**Tues 29 Jan**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 The Decor rpt
12:30 Mizengwe rpt
12:45 Aibu Yako
13:00 Series rpt: Grapes of justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:15 Local pgm rpt: Business Edition
15:00 Bundesliga kick off
15:30 Out and About rpt
16:00 Capchat rpt
17:00 Ripoti Maalum rpt
17:30 Meza huru
19:00 Innovation
19:30 Ripoti Maalum
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime
22:00 Turning the Spotlight rpt
22:30 Iron Chef rpt
23:30 Al Jazeera

**Wed 30 Jan**
06:00 Al jazeera
08:00 CNN International News
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the Spotlight rpt
12:30 Culinary delight rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Local Pgm: The Monday Agenda Rpt
15:15 Capchat rpt
16:15 CNN International
17:00 Innovation rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Sports Gazette
19:30 Business edition rpt
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Dakika 45:
22:45 The Décor
23:15 Al Jazeera

**Thurs 31**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Sports Gazette
12:30 Out n' about rpt:
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Business Edition rpt
15:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
16:00 Dakika 45 rpt
17:00 In good shape
17:30 Meza Huru
19:00 Turning the spotlight
19;30 Usafiri wako
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Capchat rpt
23:00 Al Jazeera

**Frid 01 Feb**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Innovation rpt
12:30 The Decor rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Ripoti Maalum rpt
15:00 Korean Dram rpt: Emperor of the sea
16:00 CNN International
16:30 The Monday Agenda rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Drive it
19:30 Eco@Africa
20:00 Aibu yako
20:15 Local Pgm: Business Edition
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Malumbano ya hoja rpt
00:00 Al Jazeera

**Sat 2 Feb**
08:00 CNN International
09:00 Drive It rpt
09:30 Turning the Spotlight rpt
10:00 Culinary delight rpt
10:30 Innovation rpt
11:00 Out n'about rpt
11:30 Sports Gazette rpt
12:00 Usafiri wako rpt
12:30 Eco@Africa rpt
13:00 Business edition rpt
13:30 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
14:30 Telenovela rpt: Ode To Joy
17:15 Ripoti Maaalum rpt
17:45 Bundesliga kick off
18:15 Capchat rpt
19:15 Mizengwe
19:30 The Decor
20:00 Iron Chef.
21:00 Out n' about
21:30 Movie: Fangs
23:00 The other side rpt
01:00 Al Jazeera

**Sun 03 Jan**
08:00 CNN International
09:00 In good shape
10:00 Capchat rpt
11:00 Sports Gazette rpt
11:30 Iron chef rpt
12:00 Out n about rpt
12:30 Bundesligga Kick Off rpt
13:00 Ripoti Maalum
13:30 Series rpt: Grapes of Justice Inkulo
15:15 Aibu yako
15:30 Drive it rpt
16:00 Dakika 45 rpt
16:45 Mizengwe rpt
17:00 The Decor rpt
17:30 Meza huru
19:00 Turning the Spotlight rpt
19:30 Cookery pgm:Culinary Delights
20:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
21:00 Shift
21:15 Capchat live
22:15 Telenovela: Ode To Joy
00:00 Al Jazeera

## ITV Daima WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY 28 Jan**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Hatua
10:55 Habari za saa
11:00 Kimya Milele
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jungu kuu rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:10 Aibu yako rpt
18:15 Huduma ya kwanza
18:30 Shamba shape up
19:00 Afya ya Jamii
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Dakika 45
22:00 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**TUESDAY 29 Jan**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:15 Igizo: Mtego
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Afya ya jamii rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Uchumi na biashara
13:30 Kipindi Maalum rpt : TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Huduma ya kwanza
14:15 Telenovela: Destiny (Destino) rpt:
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Korean drama rpt: The Great Queen Seonduk
19:00 Jarida la wanawake
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Documentary: Living on the edge
21:30 Kipindi maalum:
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**WEDNESDAY 30 Jan**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Shamba shape up
10:55 Habari za saa
11:00 Korean: The Great Queen Seonduk
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jarida la wanawake rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Dakika 45
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino):
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi rpt
18:30 Ijue Sheria
19:00 Kipindi Maalum: TFDA
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Biko Draw
21:05 Aibu Yako! Hata wewe?
21:10 Kipindi Maalum : Tanesco
21:40 Kipindi Maalum
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**THURSDAY 31 Jan**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Hatua
10:55 Habari za saa
11:00 Igizo: Hatua
11:15 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al jazeera
12:30 Ijue Sheria
12:55 Habari za saa
13:00 Living on the edge rpt
13:30 Jungu Kuu
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Huduma ya kwanza rpt
18:30 Kipindi Maalum: Ewura
19:00 Usafiri wako
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Malumbano ya hoja
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**FRIDAY 01 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:20 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Kipindi Maalum rpt: TCRA
12:55 Habari za saa
13:00 Kipindi maalum: Tanesco
13:30 Kipindi Maalum rpt
13:55 Habari za saa
14:00 Mapishi
14:15 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
17:30 Ibada ya kiislamu
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Mizengwe
18:30 Uchumi na biashara
19:00 Kipindi maalum: TCRA
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Kipima joto
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**SATURDAY 02 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al Jazeera
09:00 Watoto wetu
10:00 Mjue Zaidi rpt
11:00 Jungu kuu rpt
11:30 Usafiri wako
12:00 Shamba Shape up
12:30 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:45 Igizo rpt: Riziki
15:15 Igizo rpt: Hatua
15:45 Igizo rpt: Mizengwe
16:00 Igizo rpt: Kimya Milele
16:30 Igizo: Mtego rpt
17:00 Shamsham za Pwani
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Igizo: Riziki
19:00 Sanaa na wasanii
19:30 Jungu Kuu
20:00 Habari
21:00 Igizo: Kimya Milele
21:30 Hawavumi lakini wamo
22:30 Isidingo rpt
01:00 CNN International

**SUNDAY 03 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al jazeera
09:00 Watoto Wetu
10:00 Isidingo
11:45 Aibu Yako
11:50 Hawavumi lakini wamo rpt
12:50 Bongo Movie rpt: Fundi Rama
14:00 Tamasha la Michezo
15:00 Mwangaza
16:00 Korean drama: The great queen Seonduk
16:45 Mjue zaidi
17:30 Kipindi cha kikristo
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Mizengwe rpt
18:45 Matukio ya wiki
19:30 Igizo: Mtego
20:00 Habari
21:00 Biko draw
21:05 Mizengwe
21:30 3Mzuka
22:00 Bongo Movie: Fundi Rama 2
23:15 Telenovela rpt: Destiny (Destino)


EATV


LEO USIKU SAA 3:00

*Ujenzi Fahamu mambo mbalimbali kuhusu ujenzi, mapambo ya nyumba nje na ndani, mitindo na teknolojia tofauti zitumikazo kwenye ujenzi.*

JUMATATU
11:00 DADAZ (live)
15:00 FUNGUKA
16:00 UTAKE
16:30 #HASHTAG
17:00 5SELEKT
17:55 KURASA
18:00 eNewz
18:30 Music
19:00 EATV SAA 1
19:30 MJADALA
21:00 UJENZI
21:30 5SPORTS LIVE
22:30 BONGO HITS

eastafrica RADIO
05:00 EA Breakfast
09:00 Supamix
12:00 Kipenga Xtra
13:00 Planet Bongo
16:00 EA Drive
20:00 Kipenga
21:00 The Cruise
88.1FM DAR ES SALAAM


## RADIO One WEEKLY-SCHEDULE

| TIME | MONDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | RADIO ONE DOCTOR |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DAKIKA 45 |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 -03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | DK 45 ( MARUDIO ) |
| 23.00 HRS | |

| TIME | TUESDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA SHERIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 - 03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | WEDNESDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA MICHEZO |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | THURSDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA UKIMWI |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | MALUMBANO YA HOJA |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | FRIDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | HIZI NAZO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18:30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.0O HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05HRS | KIPIMA JOTO |
| 23.00 HRS | WEEKEND SHOW |
| 01:00 - 03:00HRS | HIZI NAZO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | SATURDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA KISWAHILI |
| 09.00 AM | WATOTO SHOW |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | MIWANI YA MAISHA |
| 11:00 AM | MTAA WA MAGOMA |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | CHAGUO LAKO |
| 15:00 HRS | MUZIKI NA MICHEZO |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.15 HRS | MIDUNDO MOTOMOTO |
| 18:00 HRS | BONGO TEN |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.15 HRS | CHEMSHA BONGO |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | WEEK END SHOW I |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | WEEK END SHOW II |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | WEEK END SHOW III |
| 01:00-03:00HRS | KISWAHILI ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | MUZIKI & MICHEZO ( MARUDIO ) |

| TIME | SUNDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA - FAMILIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | SUNDAY SPECIAL |
| 11: 00 HRS | TOP 20 |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13.30 HRS | NANI ZAIDI |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | MAMBO YA PWANI |
| 18:00 HRS | AFRICAN PANORAMA |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20:10 HRS | MBAVU ZANGU |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | MAMBO MSETO |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | RAFIKI I |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | RAFIKI II |
| 01:00 - 03:00 | FAMILIA ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00 HRS | RED CARPET ( MARUDIO ) |

## CAPITAL RADIO

### CAPITAL RADIO 2017 101.3 FM
### FAHARI YA MSIKILIZAJI/THE LISTENERS PRIDE

**MONDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-20:00HRS BOZOUK TIME
20:00-21:00HRS HALI HALISI
21:00-22:00HRS SPORTS
22:00-01:00HRS LADHA LAINI

**TUESDAY - FRIDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-21:00HRS BOZOUK TIME
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI
01:00-05:00HRS MUSIC & JINGLES

**SATURDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS DK 90 DUNIANI
09:00-10:00HRS MUZIKI
10:00-12:00HRS KADOGOO
12:00-13:00HRS BONGO HITS 1
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS BONGO HITS 2
15:00-16:00HRS ZAIDI YA UMJUAVYO
16:00-18:00HRS THE SPLASH
18:00-21:00HRS LAID BACK
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS AK 47 LIVE
01:00-05:00HRS MUSIC

**SUNDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS GOSPEL MUSIC
09:00-11:00HRS THE SUNDAY
11:00-13:00HRS TOP TWENTY
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS CAPITAL MICHEZONI
15:00-16:00HRS UKURASA WA MBELE
16:00-18:00HRS UNLIMITED REQUEST
18:00-21:00HRS JIACHIE
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI

HABARI KIMATAIFA

# Mlipuko: Polisi waonya Wakenya kuwa waangalifu

**NAIROBI,** Kenya

KUFUATIA tukio la bomu lililolipuka katikati ya jiji la Nairobi siku ya Jumamosi usiku, idara ya polisi sasa imewatahadharisha Wakenya kuwa waangalifu wakati huu na kuripoti mtu ama tukio lolote lisolo la kawaida miongoni mwao.

Katika chapisho lake katika mtandao wa Twitter, huduma hiyo ya kitaifa ya polisi imewaomba raia kusaidia vikosi vya usalama kukabiliana na tishio lolote kupitia kutoa habari muhimu.

Vilevile imewataka Wakenya kuendelea na shughuli zao za kwaida ikisema kuwa waathirika wawili wa mlipuko huo waliopata majeraha madogo, walipata matibabu na kwenda nyumbani.

Wamesema kwamba polisi imeanza uchunguzi kupitia kutazama picha za kamera za CCTV ili kumnasa mmiliki wa kilipuzi hicho aliyedaiwa kutoroka.

Siku ya Jumamosi usiku shambulio la bomu lilitokea katikati ya Jiji la Nairobi na kuwajeruhi watu wawili, kwa mujibu wa maafisa wa polisi .

Walioshuhudia wanasema kuwa mlio mkubwa ulisikika katika eneo la Odeon, moja ya viunga vyenye shughuli nyingi na mikusanyiko ya watu wengi katikati ya Jiji la Nairobi.

Habari zinasema kwamba bomu hilo lilikuwa limefichwa ndani ya begi na kusukumwa kwa mkokoteni.

Mkuu wa polisi wa Jiji la Nairobi, Philip Ndolo, aliambia wanahabari kuwa, mtu mmoja mwenye asili ya Kisomali alikodi mkokoteni na kupakia begi lake, na walipofika eneo la tukio, kwenye makutano ya barabara za Tom Mboya na Latema mmiliki huyo wa begi alitoweka.

"Alimhadaa mwenye mkokoteni kwa kumwambia amsubiri akafuate kitambulisho chake ambacho alikisahau... hakurudi na baada ya muda mfupi kilipuzi kilichokuwamo ndani ya begi hilo kililipuka," amesema bwana Ndolo.

Mlipuko huo umewajeruhi mwendesha mkokoteni na mfanyabiashara ndogo ndogo aliyekuwapo karibu na mkokoteni. Mlio mkubwa wa bomu hilo ulizua taharuki kubwa kwenye eneo hilo lenye stendi nyingi za mabasi ya abiria.

Shambulio hilo linakuja siku chache toka viunga vya hoteli ya kifahari ya DusitD2 kushambuliwa na kupelekea vifo vya watu 21.

Tayari eneo hilo limefungwa na polisi na vikosi vya kutegua mabomu vimeshawasili eneo la tukio.

Mlipuko huo unajiri huku maafisa wa polisi wakitoa tahadhari ya kiusalama kwa Wakenya. **BBC**



Polisi wakiwa wameimarisha usalama jijini Nairobi, baada ya mlipuko wa bomu Jumamosi usiku. **PICHA BBC.**



## Makaburi zaidi ya 50 yagundulika Congo

**KINSHASA,** Congo

MASHIRIKA ya haki za binadamu yanasema makaburi zaidi ya 50 ya umati yamegunduliwa magharibi mwa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) kufuatia matukio kadhaa ya mauwaji katika eneo hilo."Kuna zaidi ya makaburi 50 ya umati wa watu, na mengine ya kawaida ambayo yamegundulika Yumbi-magharibi mwa mkoa wa Mai-Ndombe.

Hayo yalibainishwa na mkurugenzi wa ofisi ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia masuala ya haki za binaadamu, Abdel Aziz Tjioye (pichani juu), baada ya uchunguzi wa pamoja kwa ushirikiano pamoja na maafisa wa serikali wa eneo hilo.

"Hali hiyo inaashiria idadi ya waliouawa ni kubwa zaidi kwa sababu watu watano, kumi au zaidi wanaweza kuzikwa ndani ya kaburi la jumla," alisema.

"Pengine kuna maiti mia moja au mara nne zaidi ya hao. Mkuu wa vikosi vya wanajeshi katika eneo hilo la magharibi," alisema Jenerali Fall Sikabwe ameliambia shirika la habari la Ufaransa AFP uchunguzi umeanza kuhusu tukio hilo. **DW**

# Milipuko ya yatikisa Kanisa

**MANILA,** Ufilipino

WATU wasiopungua 27 wameuawa katika milipuko mwili ya mabomu Kanisani wakati wa misa ya Jumapili kusini mwa Ufilipino. Serikali imeapa kuwasaka "magaidi" waliohusika na shambulio hilo katika mkoa wenye Waislamu wengi.

Mabomu mawili yamelipuka nje ya Kanisa wakati wa Misa ya Jumapili kusini mwa Ufilipino, na kuua watu 18 na kuwajeruhi wengine 77, maafisa wamesema. Bomu la kwanza liliripuka nje ya Kanisa Katoliki la Kirumi kwenye kisiwa cha Jolo katika mkoa wa Sulu, na la pili liliripuka dakika moja baadae karibu na lango kuu la kuingilia kanisani hapo.

Picha kutoka eneo la tukio zilionyesha mlango, mabenchi ya kanisani na madirisha ya vioo vya Kanisa la Mount Camel vikiwa vimevunjwa vunjwa, na miili ikiwa imetapakaa chini, alisema mpiga picha wa shirika la habari la Ufaransa AFP.

Msemaji wa Rais Rodrigo Duterte amelaani tukio hilo alilolitaja kuwa "kitendo cha ugaidi na mauaji." "Lengo kwa uhakika ni .... ugaidi. Hawa ni watu wasiopenda amani," msemaji wa jeshi kwenye mkoa huo Luteni Kanali Gerry Besana aliliambia shirika la habari la AFP.

Alisema wachunguzi walikuwa wanajaribu kubaini aina ya vilipuzi vilivyotumiwa katika shambulio hilo ili kusaidia kuwabaini washukiwa. Hakuna kundi lililodai kuhusika na shambulizi hilo ambalo limegharimu maisha ya wanajeshi na pia raia.

Maafisa wa polisi na jeshi wakiwa mbele ya Kanisa Katoliki ambako milipuko ya mabomu ilitokea, kijiji cha Jolo, mkoani Sulu kwenye kisiwa cha kusini mwa Ufilipino cha Mindanao.

Milipuko hiyo pacha imetokea karibu wiki moja baada ya Waislamu wachache katika taifa hilo lenye Wakatoliki wengi, kupiga kura kuunga mkono utawala wa ndani katika mkoa wao kusini mwa Ufilipino.

Kuundwa kwa mkoa wa Bangsamoro wenye utawala wake wa ndani kwa Waislamu wa Mindanao, ilikuwa sehemu ya makubaliano ya amani ya 2014 kati ya serikali ya Ufilipino na kundi la wapiganaji wa chini kwa chini la Moro Islamic Liberation Front (MILF), ambalo ndilo kundi kubwa zaidi la waasi.

Ingawa maeneo mengi zaidi ya Waislamu yaliidhinisha makubaliano hayo ya kuwa na utawala wa ndani, wapigakura katika mkoa wa Sulu, iliko Jolo waliyakataa. Kisiwa cha Jolo kimekuwa ngome ya Abu Sayyaf, kundi la Kiislamu lenye itikadi kali lililoorodheshwa kama kundi la kigaidi na Marekani na Ufilipino.

Kundi hilo linafahamika kwa kufanya mashambulizi ya mabomu, mauwaji na utekaji nyara. Waziri wa ulinzi Delfin Lorenzana ameamuru usalama uimarishwe mkoani kote, wakati kukiwa na wasiwasi wa kutokea mashambulio zaidi.

"Nimeviagiza vikosi vyetu kuzidisha hali ya tahadhari, kuweka ulinzi kwenye maeneo yote ya ibada na ya umma mara moja, na kuanzisha hatua madhubuti za kiusalama ili kuzuwia mipango ya uadui." **DW**

# Maelfu watishiwa magonjwa ya mlipuko

**Na Ibrahim Yassin,** SONGWE

WANANCHI wa vijiji vilivyopo Kata ya Mwambani na sehemu ya Kata ya Mwajuni mkoani Songwe wanaokadiliwa kuwa zaidi ya 8,000 wapo hatarini kukumbwa na magonjwa ya milipuko hasa homa za matumbo pamoja na kipindupindu baada ya kunywa maji ya kwenye chanzo hatarishi.

Wilaya ya Songwe ilitenga sehemu ya muda ya kutupa taka ngumu na laini maeneo ya juu ya mlima ambapo chini yake kuna chanzo cha maji ambayo yanategemewa kwa matumizi ya kibinadamu na wakazi hao.

Maisha Masoud, mkazi wa Mwambani, alisema anashangazwa na kitendo cha viongozi wa halmashauri hiyo kutenga eneo hilo kwa ajili ya kutupa taka licha ya kuwapo maji machafu yatokayo kwenye taka hizo yanayotiririka kwenda kwenye chanzo hicho cha maji.

Alisema mwaka jana wilaya hiyo ilikumbwa na kipindupindu kilichopelekea wawtu 700 kuugua, huku wanne walifariki dunia kilichodumu kwa miezi 18.

Chrispin Gerad, mkazi wa Mwambani, alisema ipo haja kwa serikali kuhamisha dampo hilo,kwa kuwa taka zinatupwa juu ya mlima na chini yake ndiko serikali ilipojenga chanzo kikubwa cha maji.

Alisema uchafu wa maji yatokayo kwenye dampo hilo yanatiririka kwenda kwenye maji hayo yanayotumiwa na watu, hivyo kunahofu ya kuibuka upya kwa ugonjwa huo kama hatua za makusudi hazitachukuliwa.

Diwani wa Mwambani, Noward Pattern, ,alisema utaratibu uliowekwa na halmashauri kuweka dampo hapo si sahihi na unahatarisha maisha ya watu, hivyo ipo haja ya kulihamisha kuokoa maisha ya watu.

Abraham Sambila, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, alisema amekuwa akifuatwa na watu mbalimbali wakimuomba wahamishe dampo kwa madai taka zote zinazozalishwa sokoni zinatupwa eneo hilo la chanzo cha maji.

"Tayari tumetenga shilingi milioni 30 kwa ajili ya kujenga dampo la kutupia taka, hivi sasa taratibu za manunuzi zinafanyika na tumempata mkandarasi atakayejenga dampo hilo," alisema Sambila.

Kaimu Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Anthony Mwambeni, alisema wametenga fedha kwa ajili ya kulihamisha na kuwaomba wananchi kuwa watulivu wakati wanahangaikia kulihamisha.

## Baraza laamuru soko kuvunjwa

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

BARAZA la Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi wilayani Shinyanga mkoani Shinyanga, limeamuru kuvunjwa kwa soko lililojengwa na serikali ya kijiji cha Mhungula wilayani Kahama ili kuwakabidhi wamiliki halali wa eneo hilo Hadija Ramadhani na Halfani Rajabu.

Amri hiyo ilitolewa kipindi cha Januari 18 mwaka huu na Mwenyekiti wa baraza hilo Wilaya ya Shinyanga, Edward Masao, ambapo jukumu la kutekeleza amri hiyo alipewa Abdallah Subira, mkurugenzi wa kampuni ya Subia General Supplies ltd yenye makao yake makuu mjini Shinyanga.

Katika utekelezaji huo kipindi cha Januari 18, mwaka huu barua Ref.No./SHY/LHT/Misc.App. NO.65/2015, Masao alimwandikia barua hiyo Kamanda wa Polisi Wilaya ya Kahama, Sophia Jongo ya kumtuma kwake dalalali wa Baraza hilo, Subira ili ampatie askari polisi wanne kusimamia amani kipindi cha zoezi la ubomoaji wa vibanda sokoni.

Aidha, lengo la dalali kupewa askari hao ni kuhakikisha kunakuwapo na amani na utulivu wakati wa zoezi la kuwakabidhi ndugu Hadija Ramadhani na Halfani Rajabu na kuwaondoa wapangaji na kubomoa vibanda vilivyopo kwenye eneo husika ili wakabidhiwe eneo hilo likiwa tupu.

Kwa mujibu wa barua hiyo, vibanda hivyo vya biashara vilijengwa na Serikali ya Kijiji cha Mhungula na kuahidi kuwalipa fidia washindwa tuzo ambapo washinda tuzo walistahili kulipwa Sh. milioni 13 kama fidia ya eneo lao lililochukuliwa na Serikali ya kijiji ya kujengwa vibanda husika.

Pamoja na kwamba mshindwa tuzo ameahidi mara nyingi kulipa fidia hiyo, hajafanya hivyo mpaka sasa.

Kwa upande wake mwanasheria wa shirika la kutetea haki za binadamu, Pius Mpondi, akizungumza jana na gazeti hili kutokana na tukio hilo, alisema sheria ya ardhi No.5 na 4 ya mwaka 1996 imeweka bayana kwamba ardhi itakayotwaliwa na serikali kwa ajili ya matumizi ya umma masharti ya fidia lazima yazingatiwe.



Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Juma Aweso (wa pili kushoto mwenye kofia), aliangalia namna mafundi wanavyounganisha bomba za maji katika mradi unaopeleka maji katika Kata ya Sopeko katika kijiji cha Lendikinya wilayani Monduli mkoa wa Arusha juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# Madiwani waagiza watendaji kukamatwa tuhuma za milioni 9/-

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

BARAZA la madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga mkoani Rukwa limeagiza kukamatwa maofisa watendaji wawili wa kata mpaka hapo ndugu zao watakapo rejesha shilingi milioni 9, wanazotuhumiwa kufanya ubadhirifu.

Bila kufanya hivyo, baraza limetaka wafunguliwe mashitaka ili kujibu tuhuma zinazowakabili.

Watendaji hao ni Benson Pirula wa Kata ya Kalambanzite na Nicas Kalolo wa Kata ya Lusaka ambao wanatuhumiwa kutumia fedha za makusanyo ya mapato pamoja na michango ya wananchi kwa matumizi yao binafsi.

Mwenyekiti wa baraza hilo, Kalolo Ntila, alitoa agizo hilo katika kikao cha robo ya pili ya mwaka kwa lengo kupitia utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2018/19 na kupitisha bajeti ya mwaka 2019/20.

Alisema watendaji hao wanatuhumiwa kutumia fedha hizo ambazo ni za wananchi zilizochangwa na kukusanywa kutokana na tozo mbalimbali kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo katika kata zao.

Ntila alisema mtendaji wa Kata ya Kalambanzite, Pirula anatuhumiwa kutumia shilingi milioni 3 ambazo alikusanya kutoka katika tozo za ushuru wa kata hiyo kwenda kununua ng'ombe wake binafsi.

Alisema mtendaji Kalolo wa Kata ya Lusaka, anatuhumiwa kuchukua shilingi milioni sita ambazo zilichangwa na wananchi kwa ajili ya ujenzi wa choo cha shule ya sekondari ya kata hiyo na kuamua kuzitumia kwa matumizi binafsi, kitendo kilichosababisha shule hiyo kuendelea kkosa vyoo vya wanafunzi.

Mwenyekiti huyo alisema hivi sasa hakuna sababu ya kubembelezana na watendaji hao kwa kuwa waliitwa na kuhojiwa na kukiri ,hivyo wakamatwe washikiliwe mpaka ndugu zao watakapozirejesha fedha hizo, kisha wafunguliwe mashtaka.

"Baraza linaagiza watendaji hao wakamatwe haraka sana ndani ya wiki hii, hakuna sababu ya kuzunguka, haiwezekani watu wakachezea fedha za wananchi wanavyotaka halafu tukaendelea kuwaangalia,wakamatwe maana tumechoka na vitendo hivi," alisema.

Mkuu wa wilaya ya Sumbawanga, Dk. Halfan Haule, aliwaomba madiwani hao kuwaelimisha wafanyabiashara wadogo wajitokeze kuchukua vitambulisho vilivyotolewa na Rais John Magufuli kwa ajili yao kwa kuwa mpaka sasa waliojitokeza ni wachache tofauti na matarajio.

ITV
AFYA YA JAMII SAA 1:00 USIKU
JE, UNAFAHAMU MAKUZI KWA WATOTO NI NINI, MAKUZI HAYO YANAPASA KUWAJE, NANI WAHUSIKA WA MAKUZI KWA WATOTO?. MTAALAM WA SAIKOLOJIA EDWARD MWENDAMSEKE KUTOKA ELIMISHA INITIATIVE ATAELEZEA HAYA KIUNDANI.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## HUDUMA MBALIMBALI

**MKOPO WA HARAKA NA NAFUU** Pata mkopo wa dharura ndani ya siku 2. Kwa wafanyakazi na Wafanyabiashara kutoka ENTERPRISE FINANCE LIMITED (EFL). Kwa mawasiliano Zaidi piga: 0768 928516 / 0653 258662. KARIBU EFL.

## ELIMU/MAFUNZO

**NAFASI ZA MASOMO:** Tanzania research and Career development institute. Reg pwf/041.Certificate na diploma za kilimo,mifugo, na maendeleo ya jamii. Mawasiliano:0767574701/0758753063. www.tracdi.ac.tz

## NAFASI ZA KAZI

**TUNAAJIRI WASICHANA WA MAUZO (SALES).** SIFA KIDATO CHA NNE. UMRI KUANZIA MIAKA 25 – 38 AWE MTANZANIA. MASLAHI MAZURI. PIGA SIMU NAMBA 0714 634046.


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU


**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF DODOMA**

**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO…8.. OF 2018**

**In the matter of the Estate of the late PROTASIA BERNARD NDIMBO of Chinyoya within Dodoma Region.**

**AND**

**In the matter of the Application for letters of Administration by LOTARY ERICK NDIMBO**

**GENERAL CITATION**

**RULE 75 OF PR0BATE RULES GN 369 OF 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made to the above named petitioners.

Objections to the grant should be filled on or before the 8th Day of February 2019.
Dated at Dodoma this 29th day of November 2018

……………………………………
**PETITIONER**
**Presented for filing this 12th day of November 2018**
**RESIDENT MAGISTRATE**

115027602

**FORM II**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya HIMO**

**Usimamizi wa Mirathi No. 04/2019**

**Ombi la MKOJERA PHILEMON MKOJERA kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu EVARIST AUGUST MKOJERA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 01/02/2019. kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 22/01/2019.

SAHIHI YA HAKIMU

115027402


Uza,

Chenye Thamani Kubwa

Kwa Kutangaza Nasi

Kwa Bei Poa

Tupigie 0767 223311

JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

Nipashe

NI JIBU LAKO,

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz au piga simu: 0767223311


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Inter yakamilisha usajili wa Cedric

**MILAN,** Italia

KLABU ya Inter Milan imetangaza kumsajili kwa mkopo beki wa Southampton, Cedric Soares (pichani chini).

Beki huyo raia wa Ureno nafasi yake katika kikosi cha kwanza msimu huu imechukuliwa na kijana Yan Valery na sasa ametua Inter kwa mkopo ambapo majaliwa yake yatajulikani kipindi cha majira ya joto.

Ripoti zimebainisha kwamba alifanyiwa vipimo Ijumaa, na sasa Inter wamethibitisha kupitia mitandao ya kijamii kwamba wamemsajili mchezaji huyo kwa mkopo hadi mwishoni mwa msimu huu.

"Cedric Soares ni mchezaji mpya wa Inter. Beki huyo mwenye umri wa miaka 27, anajiunga na Nerazzurri kwa mkopo kutoka Southampton FC ambapo kuna kipengele cha kumsajili kwa mkataba wa kudumu," ilianza kusema taarifa hiyo.

"Mwaka 2016, alikuwa mmoja wa wachezaji walioanza kwenye fainali ya Ulaya wakati Ureno ilipoifunga Ufaransa na kutwaa kombe hilo. Alikuwa mchezaji muhimu kwa Ureno kwenye Kombe la Dunia mwaka jana nchini Urusi chini ya kocha, Fernando Santos ambapo kikosi hicho kilifuzu raundi ya 16 kabla ya kuondolewa na Uruguay.

"Na sasa Inter Milan ipo tayari kumkaribisha Cedric Soares. Tunamtakia kila la heri katika maisha yake mpya hapa Nerazzurri!"

Uhamisho huo sasa utamfanya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 kubakia hapo kwa miamba hao wa Serie A hadi mwishoni mwa msimu, na Inter wana kipengele cha kulipa pauni milioni 9.5 kama wakitaka kumsajili kwa mkataba wa kudumu.







# SOLARI

## *amsifia Benzema, ampa majukumu Real*

**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Real Madrid, Santiago Solari amepaza sauti kumsifia nyota wake, Karim Benzema kwa kutokuwa mbinafasi na kumsifu kama "mchezaji bora zaidi" duniani.

Baada ya kuondoka kwa Cristiano Ronaldo wakati wa majira ya joto, mzigo wa kufunga mabao ya Madrid aliachiwa Benzema.

Ingawa amefunga mara saba tu katika mechi 20 za La Liga, Mfaransa huyo ndiye mfungaji bora wa Madrid msimu huu.

Solari ameyaangalia mabao yake ya nyuma, hata hivyo amemsifia kuwa na uhusiano mzuri na wachezaji wenzake.

"Benzema amekuwa na muda mrefu kwenye maisha ya soka, amepanda na kushuka," amesema Solari akiwaambia waandishi wa habari kabla ya mchezo wao dhidi ya Espanyol jana Jumapili.

"Kwa kawaida ni mchezaji mzuri kwa sasa. Ni mchezaji wa kiwango cha juu kwa sasa, na amekuwa na mwaka mzuri. Mara zote nimekuwa nikisema ni mchezaji wa aina yake kwa sababu siku zote anatengeneza pasi kwa wachezaji wenzake.

"Anawafanya wachezaji wote wanaomzunguka kuwa bora zaidi na amekuwa akifanya kazi kubwa. Amecheza karibia kila mechi msimu huu na sasa anakaribia kupona kidole alichovunjika."

## Morata afanyiwa vipimo kujiunga Atletico Madrid

**MADRID,** Hispania

ALVARO Morata (pichani), jana Jumapili alifanyiwa vipimo vya afya yake katika Klabu ya Atletico Madrid ili kukamilisha usajili wake wa mkopo kutoka Chelsea.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, alikuwa akihusishwa kwa wiki kadhaa na mpango wake wa kuondoka Stamford Bridge baada ya kushindwa kupata namba kwenye kikosi hicho chini ya kocha Maurizio Sarri.

Na sasa ameamua kurudi kwenye nchi yake ya kuzaliwa, na Sky Sports imethibitisha kwamba amewasili huko kwa ajili ya kukamilisha usajili wa kutua hapo Atletico.

Anatarajia kucheza chini ya kikosi hicho kinachonolewa na kocha, Diego Simeone hadi mwishoni mwa msimu huu, na dili hilo lina kipengele cha kumnunua moja kwa moja kama akionyesha kuimarika kwa kiwango chake.

Kuondoka kwa Morata pale Blues kutaonekana kama kupoteza muda kwa pande zote mbili, mchezaji na klabu baada ya kuanza msimu wake vizuri zaidi hapo London.

Alifunga mabao saba katika mechi zake nane za kwanza kwa klabu hiyo, lakini kiwango chake kilishuka wakati wa nusu ya pili ya msimu uliopita akimaliza akiwa na mabao 11 tu kwenye Ligi Kuu.

Ingawa hilo linaweza kuwa sio tatizo kwa wengine, hasa kutokana na ukweli kwamba mchezaji huyo alinunuliwa kwa ada iliyoweka rekodi klabuni hapo ya pauni milioni 57 kutoka Real Madrid.



# VALVERDE ajitetea Messi kusugua benchi Barcelona

**BARCELONA,** Hispania

ERNESTO Valverde hajutii maamuzi yake ya kumpumzisha Lionel Messi (pichani chini), kwenye mchezo wa Kombe la Mfalme ('Copa del Rey') ambapo Barcelona walifungwa na Sevilla.

Messi, ambaye alitokea benchi na kufunga katika ushindi wa 3-1 kwenye La Liga dhidi ya Leganes Jumapili iliyopita, hakuwapo kabisa kwenye kikosi wakati Sevilla wakiibuka na ushindi 2-0 katika mchezo wa kwanza wa robo fainali.

Huku Valverde akimuacha nyota huyo nje, alijikuta akipata shutuma nyingi, lakini alitetea uamuzi wake huo, kwani alimuacha kwa ajili ya mchezo wa jana Jumapili dhidi ya majirani zao wa Katalunya, Girona.

"Haya mambo yapo chini ya maamuzi ya kocha, ambaye ndiye anayejua wachezaji gani wapo kwenye kiwango na wanaotakiwa kucheza," alisema.

"Naweza kusema kidogo. Taarifa nilizonazo juu ya wachezaji wangu hakuna mwingine anayeweza kuwa nazo, ni sisi tu ndani ya klabu.

"Nafanya kile ambacho ni bora kwa upande wetu na timu yetu. Kuna mazungumzo ya kubadilishana wakati tunapofungwa."

Valverde alipoulizwa kuhusu usajili wa mchezaji mpya, Frenkie de Jong kwamba alizungumza kwanza na kocha wa Manchester City, Pep Guardiola kabla ya kinda huyo wa Ajax kuamua kuichagua Barca.

Kocha huyo wa zamani wa Athletic Bilbao alijibu kirahisi tu: "Huwezi kumzungumzia mchezaji ambaye ana mkataba. Hiyo siyo tabia yangu. Kila mmoja ana namna ya kuendesha mambo yake. Sina cha zaidi cha kuzungumza."





# SIMEONE awakubalia mashabiki kwa Morata

**MADRID,** Hispania

DIEGO Simeone amesema maoni ya mashabiki wa Atletico Madrid yanatakiwa kuheshimiwa baada ya baadhi yao kupinga mpango wa kusajiliwa kwa, Alvaro Morata.

Mshambuliaji huyo wa Hispania jana alitarajiwa kukamilisha mipango ya kujiunga na miamba hao wa La Liga kwa mkataba wa awali wa mkopo baada ya Gonzalo Higuain kuhamia Chelsea akitokea Juventus.

Mashabiki wa Atletico walipaza sauti zao Jumamosi wakitaka dili la kumsajili mchezaji huyo wa zamani wa Real Madrid kusitishwa, huku wengi wakiimba 'Less Morata na zaidi Borja Garces' wakati timu hiyo ikiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Getafe.

Garces anachukuliwa kama kinda la Atletico linalokuja juu, na amekuwa akilinganishwa na kipenzi cha mashabiki wa timu hiyo, Fernando Torres, baada ya kufunga bao lake la kwanza la ligi dhidi ya Eibar, Septemba mwaka jana.

Wakati alipoulizwa kuhusu kelele hizo za mashabiki, Simeone aliwaambia waandishi wa habari: "Maoni ya mashabiki mara zote yanatakiwa kuheshimika. Naangalia wachezaji ambao wanaisaidia klabu."

Nikola Kalinic alipewa heshima ya mashabiki kusimama na kumpigia makofi wakati alipotolewa nje kwenye mchezo huo wa Jumamosi, ambapo raia huyo wa Croatia alitarajiwa kuondoka Atletico wakati anapowasili Morata. Hata hivyo, Simeone hakukataa wala kukubali kama mshambuliaji huyo ataondoka au kubakia hapo.

"Mara zote nimekuwa nasema ninachofikiri kuhusu Kalinic," alisema. "Amekuwa hana tatizo akiwa na wachezaji wenzake na amejitoa kwa kila kitu. Amekuwa akiwajibika wakati timu ikimhitaji."

Kulikuwa na hofu kwamba, Diego Godin alishindwa kucheza kipindi cha pili kutokana na majeraha ya nyama za paja, lakini Simeone hafikirii kama ni majeraha makubwa.

"Mashabiki wanampenda zaidi," alisema kuhusu beki huyo wa kati. "Amekuwa na mapenzi na mashabiki wa klabu."

Mabao kutoka kwa Antoine Griezmann na Saul Niguez yaliiwezesha Atletico kupata ushindi huo, na sasa wamepitwa pointi mbili na vinara wa ligi, Barcelona ambao jana Jumapili walikuwa dimbani.

# Neymar Sr ashutumu matibabu ya mwanawe

**PARIS,** Ufaransa

BABA wa Neymar ameshutumu matibabu mabaya ambayo amekuwa akiyapata mwanae ndani na nje ya uwanja baada ya nyota huyo wa Paris Saint-Germain kupata majeraha hivi karibuni.

Mshambuliaji huyo wa Brazil aliumia Jumatano iliyopita wakati wa mchezo wa ushindi wa Coupe de France dhidi ya Strasbourg baada ya kuchezewa rafu na Moataz Zemzemi.

Baadaye ilithibitishwa kwamba, Neymar (pichani), ambaye aliondolewa uwanjani, alitonesha mguu wake alioumia mwaka jana ambao ulimfanya akae nje ya dimba kwa karibia miezi mitatu.



Na baba yake Neymar Santos Sr aliandika kwa hasira kwenye mtandao wake wa Instagram akiwashutumu wale wote waliosema mwanawe aliwachokoza wale waliomuumiza.

Alikumbukia jinsi beki wa Colombia, Juan Zuniga ambaye alimchezea Neymar vibaya na kumfanya ashindwe kucheza nusu fainali ya Kombe la Dunia mwaka 2014.


Aidha, Neymar Santos Sr alisema kwamba wakati mwanawe anapodondoka uwanjani anatakiwa kupata matibabu ya uhakika.

Aliongeza: "Tusipige chenga? Hatuna haki ya kuwa na vipaji?

"Hili haliweze kukubaliwa, Neymar anapewa matibabu mabaya ndani na nje ya uwanja na ndio maana anaumia kila wakati. Lazima jambo hili liangaliwe kwa umakini mkubwa," alisema.

Neymar anatarajiwa kuwa nje ya uwanja kwa muda wa zaidi ya wiki tatu.

# DONDO … OKA MAGAZE … AYA



# SOLSKJAER KAFUTA NDOTO ZA POGBA JUVE- ALLEGRI

**TURIN,** Italia

MASSIMILISNO Allegri ameweka wazi kuwa ni "vigumu sana" kumuona kwa mara nyingine Paul Pogba akiichezea Juventus kutokana na kuonekana kuzoea maisha Manchester United tangu Jose Mourinho atimuliwe na timu hiyo kuwa chini ya mshambuliaji wa zamani wa miamba hiyo ya Old Tafford, Ole Gunnar Solskjaer.

Pogba alijiunga na Juventus akitokea United akiwa kinda mwaka 2012 na kufurahia maisha ya mafanikio kwa kipindi cha miaka minne hapo Turin, akitwaa mataji ya Serie A kwa kipindi chote.

Kiwango chake akiwa Juve, kiliifanya United kumrejesha tena Old Trafford kwa ada ya uhamisho iliyoweka rekodi ya dunia mwaka 2006 ambayo iliripotiwa kuwa pauni milioni 89.3.

Wakosoaji walidai kuwa Pogba amepotea tangu aliporejea United, wakati pia uhusiano wake na Mourinho ukiwa chanzo cha utata huo, na mara kadhaa tetesi zimekuwa zikimhusisha na Barcelona, Paris Saint-Germain na Juve.

Lakini Pogba ameibuka na kuonyesha ubora wake United tangu Mourinho alipotimuliwa mwezi uliopita, jambo ambalo limemfanya kocha wa Juve, Allegri kukiri kuna nafasi ndogo kwake kurudi kwa 'Kibibi Kizee' hicho cha Turin.

"Ni vigumu sana kumuona tena Juventus," Allegri alisema katika mkutano na wanahabari Jumamosi.

Allegri pia aliulizwa kuhusu uwezekano wa kumtoa kwa mkopo Moise Kean, lakini kocha huyo anataka kumbakisha mshambuliaji huyo ili aelekeze jicho kwake.

"Lazima abaki Juventus na kujifunza kila kitu," Allegri alisema. "Ana bahati kuwa katika klabu kama Juventus.

"Anaweza kucheza dakika chache zaidi katika klabu nyingine yoyote, lakini anaweza kupoteza muelekeo wake wa kukua kisoka."

## KWA UFUPI

### KUIONA LIVERPOOL MIL. 18/-

TIKETI za kuiona mechi ya Liverpool ya kufunga msimu wa Ligi Kuu England, tayari zimeanza kuuzwa kupitia tovuti yao kwa pauni 6,000 sawa na Sh. milioni 18.2 za Tanzania. **(Sunday Mirror)**

### BAYERN YATUA CHELSEA

BAYERN Munich inajiandaa kutoa ofa ya pauni milioni 40 Chelsea ili kumnasa Callum Hudson-Odoi, wakati RB Leipzig nayo pia ikivutiwa na winga huyo mwenye umri wa miaka 18. **(Mail on Sunday)**

### ARSENAL YAMKOMALIA MALCOM

ARSENAL ipo tayari kumsajili mshambuliaji wa Barcelona, Mbrazil Malcom, 21, na inatumai kukamilisha dili hilo kabla ya dirisha dogo kufungwa Alhamisi. **(Sun)**

### UNITED YATOA NENO PSV

MANCHESTER United imeitaka PSV Eindhoven kuendelea kuieleza endapo kutakuwapo na mpango wa kumuuza winga Mholanzi Steven Bergwijn, 21, baada ya Bayern Munich kujiunga katika mbio a kumsajili. **(Sunday Mirror)**

### MORATA KIMEELEWEKA ATLETICO

STRAIKA wa Chelsea, Alvaro Morata jana alitarajiwa kupimwa afya Atletico Madrid kuelekea kukamilisha mkataba wake wa mkopo. **(Sky Sports)**

### AURIER AMVUTA RABIOT SPURS

BEKI wa pembeni wa Tottenham, Serge Aurier, amefunguka kuwa mchezaji mwenza wa zamani wakati akiwa PSG, Adrien Rabiot anakaribia kujiunga naye hapo London. **(Tribal)**

### HAZARD AKUBALIKA REAL

MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Eden Hazard, 28, ni windo kuu la Real Madrid kuelekea dirisha la majira ya joto baada ya washindi hao wa Ligi ya Mabingwa Ulaya kuhitimisha mpango wao wa kumsajili kiungo Mdenmark Christian Eriksen, 26, kutoka Tottenham. **(AS)**

### MAJERAHA YAMTIBULIA KOMPANY

BEKI wa Manchester City, Vincent Kompany, 32, matamanio yake ya kusaini mkataba mpya yamekuwa yakivurugwa na kuwa fiti kufuatia Mbelgiji huyo kuandamwa na majeraha. **(Sunday Mirror)**

### EMENALO YAMKUTA YA HENRY

MONACO imemtimua Mkurugenzi wa Ufundi wa zamani wa Chelsea, Michael Emenalo, 53, katika nafasi yake ya ukurugenzi siku moja baada ya Thierry Henry kutimuliwa kuinoa timu hiyo. **(Mail on Sunday)**

### ALLISON KUONGEZA FAMILIA

KIPA wa Liverpool, Allison ametangaza yeye na mkewe, Natalia, wanatarajia kupata mtoto wa pili. **(Instagram)**

### ALBA KUBAKI BARCELONA

JORDI Alba ameweka wazi kuwa kipaumbele chake ni kubaki Barcelona. Beki huyo wa pembeni bado ana subiri mkataba mpya hapo Camp Nou. **(Tribal)**

### ARSENAL YAMTAKA PABLO

ARSENAL inamtolea jicho kiungo wa Villarreal, Mhispania Pablo Fornals, 22. **(Sport via Sun)**

HABARI MICHEZO

# SIMBA IMEKOSA BAHATI TU SPORTPESA CUP-TSHABALALA

Na Faustine Feliciane

NAHODHA msaidizi wa Simba, Mohammed Hussein 'Tshabalala', amesema timu yao haina bahati na mashindano ya SportPesa yaliyomalizika jana jijini Dar es Salaam kwa timu hiyo kushika nafasi ya tatu baada ya kuichapa Mbao FC kwa mikwaju ya penalti 5-3 kufuatia sare tasa ndani ya dakika 90.

Simba kwa Mara ya tatu mfululizo imeshindwa kufanya vizuri katika mashindano hayo ambapo mara moja, mwaka jana ilifika fainali nchini Kenya, na mwaka huu imeishia hatua ya nusu fainali.

Akizungumza na Nipashe kabla ya mchezo wa jana dhidi ya Mbao FC wa kutafuta mshindi wa tatu wa michuano hiyo, Tshabalala alisema wamekosa bahati kwenye michuano hiyo licha ya kupania kufanya vema.

"Tulipania kuchukua ubingwa lakini bahati haikuwa kwetu..., tumekosa bahati kwenye mashindano haya, kwa sasa tunaelekeza nguvu kwenye Ligi Kuu na michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema Tshabalala.

Aidha, alisema kufungwa mabao 5-0 kwenye mchezo wa Kundi D wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya AS Vita ya DR Congo, bado hawajakata tamaa ya kufanya vizuri.

"Tumecheza michezo miwili kwenye kundi letu, tumeshinda mmoja na kufungwa mmoja, ukiangalia bado tuna nafasi ya kufanya vizuri, kikubwa ni kujipanga na kujituma kwenye michezo iliyobaki," alisema Tshabalala.

Mchezo unaofuata Simba itacheza na Al Ahly ya Misri Jumamosi wiki hii kabla ya kurejea Dar es Salaam kuwasubiri AS Vita kwenye mchezo wa marudiano.

Katika kundi lao, Simba inashika nafasi ya tatu ikiwa na pointi tatu sawa na AS Vita inayoshika nafasi ya pili nyuma ya vinara Al Ahly wenye pointi nne, JS Saoura wenyewe wanaburuza mkia wakiwa na alama moja.



Beki wa Royal Excel Mouscron, Mcameroon Frank Boya, akiteleza mbele ya mshambuliaji wa KRC Genk, Mtanzania Mbwana Samatta, wakati akijitahidi kuucheza mpira kwenye mechi ya Ligi Daraja la Kwanza A nchini Ubelgiji iliyopigwa Uwanja wa Luminus Arena juzi. Royal Excel Mouscron ilishinda 2-1. PICHA: BIN ZUBEIRY

# Tambwe: Zahera ana mbinu za ubingwa

Na Mwandishi Wetu

MSHAMBULIAJI wa Yanga, Amissi Tambwe, amesema mbinu tofauti katika kila mechi wanazozipata kutoka kwa kocha wao, Mwinyi Zahera, zinampa matumaini makubwa ya kutwaa ubingwa msimu huu.

Aidha, amesema kama kocha wake ataendelea kumpa nafasi ya kucheza ana uhakika wa kuendelea kuifungia mabao mengi timu hiyo.

Alisema pamoja na ugumu wa ligi na kupoteza mchezo uliopita bado wanauweza wa kuendeleza makali yao msimu huu.

"Naiona nafasi ya timu yangu kufanya vizuri msimu huu, tumepoteza mchezo mmoja lakini tunaendelea kukaa kileleni mwa msimamo wa ligi..., tunaweza kuendeleza makali yetu," alisema Tambwe.

Alisema Zahera, ana mbinu nyingi zinazoweza kuwapa ubingwa msimu huu.

"Tuna kocha mzuri, ana mbinu nyingi ambazo tunauhakika zitatusaidia kutwaa ubingwa msimu huu, kila mchezo kocha amekuwa akitupa mbinu za kushinda," alisema.

Yanga sasa inajiandaa na mchezo wa Kombe FA dhidi ya Biashara ya Mara ambao utachezwa Alhamisi wiki hii kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

**MSIMAMO LIGI KUU BARA**

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.Yanga | 20 | 17 | 2 | 1 | 38 | 14 | 53 |
| 2.Azam | 20 | 14 | 5 | 1 | 29 | 9 | 47 |
| 3.KMC | 22 | 8 | 10 | 4 | 29 | 16 | 34 |
| 4.Simba | 14 | 10 | 3 | 1 | 28 | 5 | 33 |
| 5.Lipuli | 22 | 8 | 9 | 5 | 17 | 13 | 33 |
| 6.Mbao | 23 | 8 | 9 | 6 | 16 | 19 | 33 |
| 7.C. Union | 21 | 6 | 10 | 5 | 20 | 21 | 28 |
| 8.K. Sugar | 21 | 6 | 10 | 5 | 19 | 20 | 28 |
| 9.Alliance | 23 | 7 | 7 | 9 | 18 | 26 | 28 |
| 10.Mtibwa | 19 | 8 | 3 | 8 | 19 | 15 | 27 |
| 11.Mbeya City | 21 | 7 | 5 | 9 | 24 | 26 | 26 |
| 12.JKT | 23 | 5 | 11 | 7 | 9 | 14 | 26 |
| 13.Stand Utd | 23 | 7 | 4 | 12 | 21 | 31 | 25 |
| 14.R. Shooting | 23 | 6 | 7 | 10 | 19 | 31 | 25 |
| 15.Mwadui | 23 | 6 | 6 | 11 | 24 | 22 | 24 |
| 16.S. United | 21 | 6 | 6 | 9 | 15 | 20 | 24 |
| 17.Ndanda | 21 | 5 | 7 | 9 | 12 | 25 | 22 |
| 18.Biashara Utd | 23 | 4 | 8 | 11 | 14 | 23 | 20 |
| 19.African Lyon | 23 | 4 | 7 | 12 | 15 | 27 | 19 |
| 20.TZ Prisons | 22 | 2 | 11 | 9 | 12 | 21 | 17 |

## Wawekezaji sanaa za maigizo shida Zanzibar

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

KUTOKUWAPO kwa uwekezaji katika soko la filamu ni changamoto kubwa inayowakabili wasanii wa maigizo ('Zenj movie') visiwani hapa.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu wa Chama cha Wasanii Waigizaji Zanzibar, Salum Stika, alisema ili kuwapo na soko la filamu nchini, lazima wajitokeza wawekezaji watakaonunua kazi za wasanii ili kukuza soko hilo na kuleta ushindani.

Alisema kwa sasa Zanzibar hakuna soko la filamu kama ilivyo kwa nchi nyingine na hii inatokana na wasanii kukosa fedha za kutengeneza filamu zenye ubora na kuingia katika ushindani kama ilivyo katika nchi nyingine zinazoendelea.

Stika alisema ili kukuza tasnia ya filamu nchini lazima kuwapo na uwekezaji mkubwa ambao utawekeza kuendana na kasi ya soko la filamu lililopo hivi sasa na kupenya hata kimataifa.

"Wasanii wa filamu Zanzibar wanajitahidi kutengeneza pamoja na kucheza filamu nzuri ambazo zinaendana na utamaduni wa Zanzibar, lakini hii chanamoto ya wawekezaji ndio tatizo linalowarejesha nyuma, utakuta hata idadi ya filamu zinazotengenezwa Zanzibar bado ni chache,"alisema.

Aidha, alisema Zanzibar kumebarikiwa vipaji vya sanaa mbalimbali, lakini uhaba wa fedha unachangia wasanii wa visiwani hapa wengi wao kutojulikana na wachache wanaojulikana pia wamekuwa wakipambana ili kuhakikisha wanaitangaza Zanzibar vema na kuvuta wawekezaji.

Alisema endapo suala la kukuza soko la filamu litafanyiwa kazi, Zanzibar itaendelea kufanya vizuri katika filamu zake ikilinganishwa na hivi sasa ambapo imejitahidi nafasi ya baadhi ya filamu kushiriki katika tuzo mbalimbali zinazoandaliwa ndani na nje ya Zanzibar.

Hata hivyo, alisema Chama cha Waigizaji Zanzibar kinaangalia utaratibu wa kutafuta wawekezaji hasa wafanyabiashara waliopo ili kuwashawishi kuona namna gani wataweza kusaidia sanaa hii ya uigizaji visiwani hapa.

# Michezo

Jumatatu Januari 28, 2019

Nipashe


## Solskjaer kafuta ndoto za Pogba Juve- Allegri



HABARI UK. 30

MILIKI...



Mchezaji wa Mbao FC, Herbet Lukindo, akimiliki mpira dhidi ya beki wa kati wa Simba, Pascal Wawa wakati wa mechi ya kusaka mshindi wa tatu wa michuano ya SportPesa, iliyopigwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: HALIMA KAMBI**

# SIMBA YAKATISHA TAMAA VS AL AHLY

### Mashabiki sasa waachana na amshaamsha ya ushindi waizomea mwanzo mwisho, Kariobangi mabingwa...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI wawakilishi pekee wa Afrika Mashariki na Kati kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba wametumia michuano ya Kombe la SportPesa kujiandaa na mechi ya hatua ya makundi dhidi ya Al Ahly, mashabiki wa timu hiyo wameonekana kukata tamaa na kiwango kilichoonyeshwa na timu hiyo.

Simba ambayo Jumamosi itashuka dimbani jijini Cairo, Misri kuvaana na Al Ahly, jana iliendeleza kiwango chao kibovu katika michuano hiyo ambayo Kariobangi Sharks ya Kenya iliibuka mabingwa kwa kuwafunga ndugu zao Bandari FC ya Mombasa kwa bao 1-0 katika mechi ya fainali iliyopigwa Uwanja wa Taifa.

Licha ya ushindi wa penalti 5-3 walioupata Simba kwenye mchezo wa kuwania nafasi ya tatu katika michuano hiyo ya SportPesa dhidi ya Mbao FC jana, mashabiki wa Simba walishindwa kuvumilia kiwango cha chini kilichoonyeshwa na wachezaji wake kwenye mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Taifa.

Simba ilipewa nafasi kubwa ya kufanya vizuri kwenye michuano hiyo, lakini ilijikuta ikiondolewa kwenye hatua ya nusu fainali na Bandari FC na kuangukia kucheza mchezo wa kusaka mshindi wa tatu wa kinyang'anyiro hicho ambacho tangu kianzishwe huu ukiwa mwaka wa tatu, timu za Kenya zimekuwa zikitwaa ubingwa huo.

Katika mchezo wa jana, Simba ililazimishwa suluhu ndani ya dakika 90 licha kupoteza nafasi nyingi za kufunga kupitia kwa Hassan Dilunga, Emmanuel Okwi na Rashidi Juma.

Mbao walionekana kuwabana vilivyo Simba kabla kuanza kuishiwa nguvu dakika 10 za mwisho ambapo Simba ilifanya mashambulizi mengi mfululizo, lakini washambuliaji wake walipoteza umakini.

Okwi, Clatous Chama na Rashidi kwa nyakati tofauti waligongesha mwamba katika harakati za kutaka kufunga.

Kabla ya kuanza kwa mchezo huo, mashabiki wa Simba waliwazomea wachezaji wao wakati wakiingia uwanjani tayari kwa mchezo huo kutokana na kukerwa na kiwango ambacho kimekuwa kikionyeshwa na timu yao.

Kocha wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems, alimpumzisha golikipa namba moja wa timu hiyo Aishi Manula na kumuanzisha Deogratius Munishi 'Dida' ambaye alicheza vizuri.

Penalti za Simba kwenye mchezo wa jana zilifungwa na Okwi, Nicolaus Gyan, Pascal Wawa na Dida huku Mbao wakikosa penalti moja na kutoa nafasi kwa Simba kutwaa nafasi ya tatu ya michuano hiyo.

Kwa kushika nafasi hiyo ya tatu, Simba wamepata zawadi ya dola 7,500 za Marekani ambazo ni sawa na Sh. milioni 17.2 za Tanzania huku Mbao waliomaliza nafasi ya nne wakiibuka na dola 5,000 (Sh. milioni 11.5).

Bingwa wa michuano hiyo, Kariobangi Sharks, ameibuka na dola 30,000 (Sh. milioni 69.2), wakati mshindi wa pili Bandari FC akilamba dola 20,000 sawa na Sh.milioni 46.1 za Tanzania.

# Zahera: Siiangalii Simba ubingwa

**Na Faustine Feliciane**

KOCHA wa Yanga, Mwinyi Zahera, amesema haangalii michezo ya wapinzani wao na anachokifanya ni kuhakikisha wanafanya vizuri kwenye mechi zinawakabili kwa sasa.

Akizungumza na Nipashe jana, Zahera, alisema anafahamu wamecheza michezo mingi zaidi ukilinganisha na watani zao, Simba, lakini hilo halimpi shida kwani anachokitaka ni kuhakikisha anashinda kwenye michezo yao.

**"Michezo ya timu nyingine sisi haituhusu, hatuwaangalii wenzetu, nafahamu ili tuchukue ubingwa tunapaswa kushinda katika kila mchezo..., na tunatakiwa kufanya hivyo," alisema Zahera.**

Alisema msimu huu lengo lao ni kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu, lakini pia kuchukua ubingwa wa Kombe la FA.

"Tuna mchezo wa Kombe la FA, nguvu zetu kwa sasa tunazielekeza huko, baada ya mchezo huo tutarejea tena kwenye ligi..., hatupswi kudharau mchezo hivyo tunajipanga kukabiliana na Biashara United kwenye mechi yetu ya FA," alisema Zahera.

Aidha, alisema anawaamini wachezaji wake na anashukuru kwa namna wanavyopokea maelekezo yake.

"Kila mmoja anafahamu majukumu yake, wachezaji wangu wamekuwa wakinisapoti kwa kufanya kile ninachowaelekeza, ni jambo zuri kuwa na wachezaji wanaokuelewa na kufanya kile unachotaka," alisema.

Yanga inaendelea kuongoza ligi kwa kuwa na pointi 53 wakifuatiwa na Azam wenye alama 47 baada ya timu hizo mbili kila moja kucheza mechi 20 wakati huu Simba ikiwa nyuma mechi sita na pointi zake 33.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >